**8 FEBRUARI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

__________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

__________

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Saba – Tarehe 8 Februari 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2022.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Katibu tuendelee.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Mheshimiwa Martha Festo Mariki, aulize swali lake.

Na. 104

**Changamoto ya uhaba wa walimu shule za pembezoni**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kutatua changamoto ya uhaba wa walimu katika shule za pembezoni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa ajira ili kukabiliana na upungufu wa walimu shuleni, unaotokana na walimu kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa, kufariki na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa. Tangu mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2021/2022, Serikali imeajiri

jumla ya walimu 26,598 wakiwemo walimu 16,640 wa shule za msingi na walimu 9,958 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina hakikisha walimu wanaajiriwa na kupangwa katika shule zenye uhitaji zaidi, hususan zilizoko maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliboresha mfumo maalum wa maombi ya ajira na upangaji wa walimu ujulikanao kama *Teachers Allocation Protocol.* Kupitia mfumo huo, shule zenye upungufu mkubwa wa walimu hususan zilizoko vijijini hubainishwa, ambapo walimu huomba ajira moja kwa moja kwa kuchagua shule husika iliyopo katika mfumo. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara kufanya msawazo wa walimu kutoka shule zenye ziada na kuwapeleka katika shule zenye upungufu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri walimu kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha ili kukabiliana na uhaba wa walimu hususani katika maeneo ya pembezoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini bado kumekuwa kuna changamoto kubwa hususan kwa shule shikizi ambazo zilipata msaada kupitia maswala la *UVIKO* pamoja na kupitia Kapu la Mama.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na shule hizo kupatiwa walimu ikiwa shile hizo zimesajiliwa lakini nyingi zina mwalimu mmoja mmoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, pamoja na kuonekana kwamba kada ya walimu imekuwa ikiajiri sana walimu wakike lakini kwa Mkoa wa Katavi imekuwa ni tofauti. Katika Mkoa wetu wa Katavi kuna changamoto kubwa sana ya walimu wa kike katika shule za Sekondari; mfano katika shule ya Majalila, shule ya Mwamapuli ambapo shule hizo zimekuwa hazina kabisa walimu wa kike.

Je, Serikali inatoa tamko gani ili Watoto wetu waweze kupata mahitaji ambayo mtoto wa kike anayapata akiwa na mwalimu wa kike shuleni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua uwepo wa vituo shikizi ambavyo vinasaidia shule mama. Tulishatoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wote mikoa nchini kuhakikisha kwamba wanafanya msawazo na sehemu ya msawazo huo ni pamoja na kupeleka walimu kwenye hivo vituo. Kwa hiyo nirudie tena jmabo hili litekelezwe kama ambavyo Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais- TAMISEMI amekwishalitolea maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu walimu wa kike Mkoa wa Katavi kukosekana, tumelipokea ili tulifanyie kazi kwa kuongeza idadi ya waalimu katika ajira zinazofuatia, na katika maeneo ambayo kuna walimu wengi tutafanya msawazo vilevile kuwapeleka katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaingia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, mbunge wa tabora mjini aulize swali lake.

Na.107

**Kuimarisha uwajibikaji wa TAKUKURU**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha Taasisi ya TAKUKURU katika uwajibikaji wake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha Wananchi wa Tanzania wanakuwa na maendeleo endelevu, Serikali imefanya yafuatayo katika kuimarisha uwajibikaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

i. Kuongeza idadi ya watumishi wa Taasisi ya TAKUKURU ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya uwajibikaji wa watumishi waliopo;

ii. Kuongeza bajeti ya matumizi mengineyo *(OC)* ya TAKUKURU kwa asilimia 51.7 kutoka shilingi bilioni 20.54

mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 31.16. Aidha, bajeti ya maendeleo nayo imeongezeka kwa asilimia 33.3 kutoka bilioni 1.5 kwa mwaka 2021/2022 hadi bilioni mbili kwa mwaka 2022/2023;

iii. Kuwajengea uwezo watumishi 984 wa TAKUKURU ambapo watumishi 976 walipata mafunzo ndani ya nchi na watumishi nane nje ya nchi;

iv. Kutoa fedha za ujenzi wa majengo ya TAKUKURU katika mikoa na wilaya ambazo hazina majengo kulingana na bajeti itakavyo ruhusu.

v. Kuanzisha program za kusaidia kuzuia zaidi rushwa kama TAKUKURU Rafiki

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hii inalenga zaidi kuisaidia TAKUKURU kuzuia zaidi rushwa na pale inapo bidi itaendelea kupambana na vitendo vya rushwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja kwa niaba ya Mheshimiwa Adamson Mwakasaka.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nishukuru majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali bado tuna changamoto nyingi hasa kwenye upande wa magari katika taasisi hii ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kurahishisha kazi zao;

Je, Serikali ina mpango gani kuhusiana na masuala mazima ya magari ya usafiri kwa Taasisi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili;

Je, Seriikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi katika Taasisi hii, ambao bado maeneo mengi tuna changamoto kubwa ya watumishi kwenye taasisi hii, ili

waweze kufanya kazi vizuri na tukiangalia Taasisi hii ina - *deal* na masuala ya rushwa na bado tuna changamoto nyingi sana katika nchi hii kuhusu suala la rushwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya usafiri, hili linachukuliwa umuhimu wa pekee, na hata kwenye bajeti ijayo tunaomba nafasi ya kuongeza vyombo vya usafiri, ili kuwasaidia maafisa wetu wa TAKUKURU kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile suala la kuongeza watumishi tunaendelea nalo ni zoezi endelevu. Kwa ushahidi Waheshimiwa Wabunge wote mnajua hata mwaka huu TAKUKURU ilipata nafasi na mpaka sasa kwenye kipindi hiki, bado wanaendelea na mchakato. Tangazo lao la mwisho lina kama wiki mbili hivi bado wanaendelea kufanya mchakato wa kupata watumishi zaidi. Kwa hiyo hili zoezi la kuongeza watumishi ni zoezi endelevu kulinganna na upatikanaji wa fedha na namna Serikali itakavyopata nafasi ya kuongeza nafasi zaidi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Na. 105

**Kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ili kuondoa migogoro ya Wakulima na Wafugaji katika Wilaya ya Kilwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina jumla ya vijiji 90 na kati ya vijiji hivi, vijiji 56 vina Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi mpaka kufikia mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa na kumaliza kabisa migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara, Serikali imejipanga kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji sita kwa kila mwaka. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vitatu vya Nandete, Kiranjeranje na Ruhatwe na kufanya urejeaji wa mipango ya matumizi ya ardhi iliyokwisha muda wake katika Vijiji vya Kandawale, Likawage na Nanjilinji B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, halmashauri zote za wilaya nchini zimeelekezwa kutenga fedha kila mwaka katika bajeti zao kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yote ya vijiji ikiwa ni pamoja na kuweka alama zinazoonekana kwa urahisi ili kuwezesha maeneo hayo kulindwa na kuzuia mwingiliano wa kimatumizi unaofanywa na wananchi. Hatua hii itawezesha kumaliza migogoro ya ardhi inayohusisha wakulima na wafugaji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunijibu swali langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri; kwamba kutokanana changamoto kuwa kubwa ya migogoro ya wakulima na wafugaji kila kukicha ambayo imesababisha watu mbalimbali kupambana na kufa wengine, wengine wamepata ulemavu.

Je, haioni kwamba kuna uhitaji sasa wa kuharakisha huu mpango wa matumizi bora ya ardhi, ili vijiji bora 34 vilivyobaki viweze kumalizwa kupangwa katika huu mpango wa matumizi bora ya ardhi mwaka 2023/2024?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalli la pili. Katika kipindi cha miaka 10 Takwimu za Sensa zimeonesha katika Wilaya ya Kilwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wananchi. Mwaka 2012 tulikuwa na wananchi 190,744, mwaka 2022 takwimu za sensa zinaonesha kwamba wananchi wa Wilaya ya Kilwa wameongezeka hadi kufikia 297,676 sawa na ongeezeko la watu 106,932 sawa na asilimia 52 ya ongezeko. Kutokana na ongezeko hili ni wazi kwamba sehemu kubwa ya watu walioongezeka ni jamii ya wafugaji...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuweza kuwahamisha baadhi ya wafugaji kutoka Wilayani Kilwa kwenda maeneo mengine ya nchi kama ilivyofanya katika Bonde la Ihefu na katika Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna changamoto ya mogogoro kati ya wafugaji na wakulima katika Halmashauri ya Kilwa, lakini pia katika baadhi ya halmashauri hapa nchini. Serikali imeendelea kuchukua hatua, na hatua moja muhimu ni kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji ili kuwa na maeneo mahsusi kwa ajili ya kilimo, pamoja nakuwa na maeneo mahsusi kwa ajili ya ufugaji lakini pia kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika Halmashauri ya Kilwa kama nilivyotangulia kusema tayari bajeti imeandaliwa ya milioni 60 kwa ajili ya kupitia mipango bora ya ardhi. Zoezi hili ni endelevu mpaka tutakapokamilisha vijiji vingine vilivyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kuhusiana na ongezeko la wananchi ni kweli wafugaji wengi wamehamia Kilwa na Mkoa wa Lindi kwa ujumla na baadhi ya mikoa mingine. Serikali inaendelea kufanya tathmini na kuona

maeneo yale ambayo yana wafugaji wengi basi tuweze kuweka mgawanyo sahihi ili kulinda mazingira lakini kuepusha migogoro, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini.

Na. 106

**Ujenzi wa barabara ya Mbinga Luwaita kwa kiwango cha lami**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mbinga Luwaita kupitia Mradi wa *Agri-connect* kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda Mbunge wa Mbinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Agri-connect* ni programu inayofadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ambapo inahusisha ujenzi wa barabara kwa lengo la kusafirisha mazao kutoka shambani au sehemu za uzalishaji kwenda kwenye masoko, viwanda na maghala. Aidha, utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa awamu Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti barabara ya Luwaita ipo katika Awamu ya Tatu ya programu ya *Agri-connect* itakayoanza

mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa sasa, awamu ya tatu ipo kwenye hatua ya uainishaji, uhakiki na upangaji wa vipaumbele vya barabara katika mikoa sita, ambayo ni Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Katavi na Songwe kwa kusimamiwa na Wizara ya kilimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nishukuru sana kwa majibu ya Serikali lakini nilikuwa na ombi. Naiomba Serikali kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa mapema kwa sababu ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa kata ya Luwaita kwa ajili ya kusafirisha mazo yao kwenda kwenye maeneo ya soko, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea tutafanya hivyo, kwa sababu awamu ya kwanza na ya pili ziko katika utekelezaji kwa hito na hii ya tatu tutaitekeleza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimemuona Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa menyekiti, ahsante kwa swali lanyongeza. Barabara ya kutoka Mapera kuelekea Ilela iliyopo Mbinga Vijijini imeharibika sana na kukwamisha shughuli za maendeleo za wakazi wa Kata za Mapera, Kambarage pamoja na Mikaranga.

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura kwa ajili ya kurekebisha barabara hii ili wakazi wa maeneo haya shughuli zao za maendeleo ziweze kuendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI) (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Judith Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, niagize tu *TARURA* mkoa wake waende waipitie hii barabra ya Mapera mpaka Ilela waangalie uharibifu ambao upo na watoe tathmini ili tutafute fedha iweze kurekebishwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde. Kwa sababu maalum tunaanza swali la Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, aulize swali lake.

Na. 117

**Hitaji la umeme Kata za Jimbo la Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza: -

Je, ni lini Kata za Mtungulu, Mwamashiga, Isakamaliwa, Kining'inila na Kinungu zitapatiwa umeme?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Mtungulu, Mwamashiga, Isakamaliwa, Kining'inila na Kinungu zote zipo kwenye Mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unaoendelea. Mkandarasi anayetekeleza mradi huo anaitwa M/S CEYLEX ameshafika kwenye maeneo hayo. Kwa Kata ya Mtunguli, katika vijiji viwili kati ya vijiji vitatu ambavyo ni Maguguni na Mtungulu, kazi ya kusambaza umeme imekamilika na umeme umeshawashwa, isipokua Kijiji cha Mwajijambo ambacho kazi ya kuvuta nyaya inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa Kata za Mwamashiga, Isakamaliwa, Kining'inila na Kinungu kazi ya uchimbaji mashimo na usimikaji nguzo inaendelea. Utekelezaji wa miradi hii yote unategemewa kukamilika ndani ya kipindi cha mkataba ambacho kinaishia mwezi Aprili, 2023.

Mheshimiwa mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Awali matarajio ya Serikali ilikuwa ni kuhakikisha maeneo haya ya vijiji vinawaka umeme ilipofika mwezi wa 12 mwaka jana, mwaka 2022, na ambapo ndio muda wa mkandarasi kukaa *site* ulikuwa unakamilika. Hata hivyo, mpaka ninapoongea hivi sasa, hivi vijiji maeneo mengi mashimo yamechimbwa na nguzo zimelazwa chini bado hazijasimamishwa.

Je, naomba kujua kauli ya Serikali; ni lini, hivi vijiji vitawashwa umeme kwa kuwa na muda wa mkataba wa mkandarasi umeshakwisha?

**MWENYEKITI**: Majibu ya swali hilo, Mhehsimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mikataba iliyotakiwa kuisha Disemba mwaka jana. Hata hivyo, kama tunavyofahamu, tulipata changamoto ya kuongezeka kwa gharama za vifaa kipindi ambacho kulikuwa na magonjwa ya *UVIKO*. Pamoja na hayo tumepata faida nyingine ya kupata ongezeko la kilometa mbili kwa kila kijiji ambacho kilitakiwa kupelekewa umeme. Kwa hiyo vijiji vilivyo vingi upelekaji wa umeme utakamilika kufikia mwezi Disemba mwaka huu 2023. Kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi kwenye baadhi ya maeneo kwa Mheshimiwa Ngassa, mwezi Aprili mwaka huu kuna maeneo ambayo tayari yatakuwa yamefikiwa na umeme kwa kadri alivyoiliza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, nimekuona.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Naomba kuiuliza Serikali;

Je, ni lini vijiji 63 vilivyopo katika Jimbo la Newala Vijijini ambavyo havijawahi kuona umeme kabisa vitapatiwa umeme ili nao wawe wanufaika wa nishati hii muhimu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mhehsimiwa Mwenyekiti, wakandarasi katika Mkoa wa Mtwara na Lindi wako kazini wananendelea. Tumehimizana na wakandarasi walio katika maeneo hayo na kufatiliana nao kwa wakati ili kuhakikisha kazi yao inakamilika. Kama nilivyosema, ile kazi ya nyongeza na ya awali itakamilika mwezi Disemba mwaka huu 2023.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florence Samizi nimekuona.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Ukosefu wa *copper wire* na mita ni moja ya sababu inayochelewesha uunganishwaji wa umeme katika Jimbo la Muhambwe, ikiwemo kata ya Busagara, Kitahara, Kumsenga na Mlungu;

Je, ni lini Serikali italeta vifaa hivi, ili kata hizi ziweze kunufaika na kuunganishiwa umeme?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Florence Samizi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa uzalishaji wa vifaa ulitokea katika maeneo mengi baadaya kupata matatizo ya *UVIKO,* na hivyo milango ilivyofunguliwa *order* zilikuwa nyingi na wahitaji walikuwa wengi, Kwa hiyo na sisi tunahakikisha tunatoa *order* za kutosha na kwa kadri zinavyozaliswha tunazipata. Nimuhakikishie tu Mheshimiwa Samizi kwamba, katika eneo lake na maeneo mengine vifaa vitapatikana na huduma kwa wananchi itaendelea kuunganishwa kwa sababu pesa tunayo na tunaendelea kufatilia kwa ajili ya upatikanaji wake.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofata. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, aulize swali lake.

Na. 118

**Hitaji ya Umeme wa REA Kata ya Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Kijiji cha Kanonge Kata ya Nsimbo kitapelekewa umeme wa REA?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kanoge kilichopo Kata ya Nsimbo kina jumla ya vitongoji vitano vya Kanoge A, Kanoge B, Tupindo, Kavikonge na Tulieni. Kijiji cha Kanoge tayari kimefikiwa na huduma ya umeme katika vitongoji vya Kanoge B na Tulieni. Vitongoji vitatu vilivyosalia vitafikishiwa umeme kupitia Mradi wa kusambaza umeme wa Kitongoji kwa Kitongoji *(Hamlet Electrifiction Project)* unaotajariwa kutekelezwa nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Hiki Kijiji cha Kanoge hata kwenye ramani ya *REA* hakipo, pamoja na

vitongoji vyake. Sasa ninaomba uhakika kwa sababu nimetokea huko hata kwenye ramani ya *REA*, ina maana kijiji hiki ni kijiji cha siku nyingi, kilirukwa sasa naomba *commitment* ya Wizara. Ni lini kitawekwa kwenye ramani pamoja na vitongoji vyake na wataingia katika mchakato wa kuwekewa umeme?

Mheshimiwa mwenyekiti, la pili, katika Kijiji cha Usense Kata ya Ulwira pamoja na Kijiji cha Nyamasi, Kata ya Ugala mpaka leo miti inaoza hasa naomba *commitment* ya Wizara;

Je, ni lini vijiji hivyo vitapata umeme, kwa sababu hakuna dalili kabisa ya kupatiwa umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Lupembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kabla ya mwaka huu kuisha, vijiji hivyo alivyovitaja ambavyo vinaonekana havijafikiwa na huduma ya umeme, vitakuwa vimefikiwa kwa sababu kwenye mkataba wetu tumekubaliana kabla ya Desemba mwaka huu vijiji hivyo viwe vimepata umeme na zile changamoto tulizokuwa nazo tayari tumezitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la kwanza naomba nikitoka hapa nitawasiliana nae kwa sababu sisi taarifa tulizo nazo kutoka *site* ni hizi. Kwa hiyo tutakaa pamoja ili tuweze kuziweka pamoja. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba baada ya mradi wa *REA*-3 awamu ya pili kupita hatutarajii kuwepo na kijiji chochote ambacho hakina umeme; na hayo ndio maelekezo ya Mheshimiwa Rais

Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo tutahakikisha rekodi zetu zinakaa sawa ili kila kijiji kiweze kuwa kimepata umeme kwa kadri ya mkataba na maelekezo yaliyopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati nimekuona.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kijiji kidogo cha Msukanzi katika kata ya Illula kimerukwa kuwekewa umeme lakini kata inayofuata kuna umeme. Sasa ni lini Serikali itaona umuhimu kwamba kuruka hivi vijiji si kitu kizuri, ili vijiji vyote viwe vinapata umeme kuliko kuacha kimoja hafu vingine vinapata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Iringa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuhakikishie yeye pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba katika awamu hii ya tatu mzunguko wa pili ambayo ni ya mwisho hakuna kijiji kitakachoachwa. Tulipita humu Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge kuwaomba watuambie vijiji ambavyo vinadhani vimeachwa na tukavichukua tukaviweka kwenye orodha. Kwa hiyo kama kuna Mheshimiwa Mbunge yoyote anayedhani kuna kijiji ambacho kimerukwa kwa taarifa alizokuwa nazo basi tuwasiliane tukichukue kwa sababu sisi kwa taarifa tulivichukua vyote. Hata hivyo nitaenda pia kuwasiliana na Mheshimiwa Ritta Kabati, ili tukione hicho kijiji ambacho kimebaki tukichukue kama anavyosema.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Byabato kwa majibu hayo ya Wizara ya Nishati. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 108

**Mfuko wa mabadiliko ya tabianchi**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuanzisha mfuko wa mabadiliko ya tabianchi kusaidia kupambana na athari za mabadiliko ya Tabianchi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge na mtumishi wa wananchi wa Jimbo la Donge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa uwepo wa vyanzo vya fedha vya uhakika ili kuimarisha jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kufuatia kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, Serikali kwa sasa inafanya mapitio ya Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 ikiwemo taratibu za kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira. Mfuko huu ukianzishwa, pamoja na mambo mengine utazingatia ufadhili wa shughuli za mabadiliko ya tabianchi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba moja; kwa kuwa tayari kuna jitihada ambazo zilishafanyika toka mwaka 2014 za kuanzisha mfumo wa fedha wa mabdiliko ya tabianchi *(Tanzania Climate Financing Mechanism),* pamoja na tafiti nyingi pia zilifanyika, ili kuanzisha mfuko wa mabadiliko ya tabia ya nchi.

Je, kwa nini Serikali haioni haja ya kutumia taarifa na tafiti mbalimbali ambazo zilifanyika huko kabla ili kuweza kuharakisha utaratibu huu wa kuanzisha mfuko wa mabadiliko ya tabianchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili; kama ninavyokumbuka kwamba dunia inalichukulia suala la mabadiliko ya tabianchi ni janga kubwa kuliko athari nyingine za kimazingira;

Je kwa nini Serikali haioni haja ya kutengeneza mfuko wa mabadiliko ya tabia ya nchi unaojitegemea ili kuweza kuchochea ufadhili na kuweza kuhamasisha wafadhili na wahisani kuweza kuchangia mfuko wa mabadiliko ya tabianchi sambamba na zile jitihada za Serikali kuweza kuji-*commit* fedha zaidi katika huu mfuko? Ahsnate sana.

**MWENYEKITI:** Mhehimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Jimbo la Donge, maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo alilolishauri Mheshimiwa Mbunge, tayari ni jambo ambalo tumeshaanza kulifanyia kazi. Hivi ninavyokwambia tumeshaanza mchakato wa mapitio ya Sheria hii ya Mazingira ambayo imo katika Sura ya 191. Tumeanza mchakato huu lengo na madhumuni ili kuona, kwanza namna gani mfuko huu utaundwa, lakini vipi unaweza ukapokea fedha, namna utakavyozitoa hizo fecha, ni fursa na faida gani na ni athari zipi ambazo zinanweza zikapatiwa msaada ama zikasaidiwa kupitia mfuko huu, baada ya mfuko huu kwa sasa unaanza kutoa hizo. Kwa hiyo kikubwa nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato umeanza na muda wowote unaweza ukakamilika na hiyo hali ikaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba lengo na adhma ya Serikali katika kuunda mfuko huu kwanza ni kuhakikisha kwamba mfuko huu unajitegemea, lakini la pili ni kuhakikisha kwamba mfuko huu unapata fedha ya kutosha, tatu ni kuhakikisha kwamba mfuko huu unapata misaada kutoka kwa wafadhili mbalimbali, ili lengo na madhumuni mfuko huu uweze kusaidia wananchi katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Hivyo nimwambie tu Mhehsimiwa Mbunge kuwa adhma ya Serikali inaendanana na mawazo yake.

Mheshimiwa Mwenyekti, nakushukuru.

Mwenyekiti: Nimemuona Mheshimiwa Asha Abdullah na Mheshimiwa Simai Sadiki atafuata.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafsi. Kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yana madhara makubwa na huweza kusababisha majanga.

Je Serikali inaimarishaje kuwapa taaluma kisasa zaidi ya uokozi na uhifadhi watu wengi zaidi badala ya kutegemea JWTZ na Zima Moto pekee?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, najibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za mabadiliko ya tabianchi siku zote zinasababishwa na zinachangiwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinandamu ambazo binadamu wanafanya katika maisha yao ya kila siku. Zikiwemo shughuli za ukataji wa miti, shughuli za uharibifu wa vyanzo vya maji, shughuli za uchomaji wa misitu, shughuli za ufanyaji wa shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya hifadhi na shughuli nyingine. Kwa hiyo hatua moja ambayo tumeichukua kwanza ni kuwaelemisha wananchi, kuwaeleza athari ambazo zinapatikana baada ya wao kufanya hizo shughuli za kiubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili amabalo tunalifanya ni kusimamia sheria. Kwa sababu mbali na kuwaelimisha lakini kwa vile sheria zipo ni kuzisimamia sheria. Tatu ni kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote wanaochafua ili lengo na madhumnuni tusiwape mzigo wengine wakina Zima Moto na watu wanaoshirikiana maafa na watu wengine.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai Sadiki.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa masuala ya badiliko ya tabianchi si masuala ya ki-Muungano lakini masuala ya mikataba ya kimataifa na masuala ya mikataba ya kikanda ni masuala ambayo yanahusika moja kwa moja na masuala ya kimuungano je mtaishirikisha vipi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika matayarisho ya mfuko huo wa mazingira?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimia Mwenyekiti, kwanza pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa *Comrade* Chillo, Naibu Waziri wangu naomba kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu Simai, kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala la mazingira si suala la Muungano. Hata hivyo, katika kipindi chote, kwa sababu mazingira hayajali mipaka, tumehakikisha kutekeleza miradi mbalimbali upande wa Tanzania Bara na upande wa Visiwani. Ndiyo maana leo hii tuna mradi mkubwa wa ujenzi wa ukuta kule Wete Pemba, hali kadharika Kaskazini A kuna mradi unaendelea. Hata hivyo katika mradi wetu, na juzi mmeona tulikuwa na tukio kubwa sana la kupokea Mwana Mfalme katika nchi yetu katika mradi wa *carbon credit,* na kwenye jambo hili tumeshirikiana kwa kizuri zaidi. Kwa hiyo huku tunakokwenda sasa ushirikiano wetu unakuwa mkubwa zaidi; na hata katika vikao hivi vya awali ambavyo tumeendelea kuvifanya vyote tunashiriki kwa umoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza Zanzibar kule, kwa lengo la kuhakikisha kwamba mazingira tunayashughulikia wote kwa upana wake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimia Waziri, Selemani Jafo. Nilikuona Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na jitihada nzuri za Serikali ambazo wiki iliyopita tuliona imetoa kanuni na miongozo ya namna gani Taifa litanufaika na namna ya kuuza ile hewa ya ukaa, kwa maana ya *Carbon emission*.

Je, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira iko tayari kutoa mafunzo kwenye Halmashauri ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kupanda miti kama ilivyo Halmashauri ya Mafinga, Mufindi, Kilolo na Halmashauri katika Mkoa wa Njombe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chungahela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika wakati tumeona kwamba jambo hili la biashara hii ya hewa ukaa ni jambo ambalo pamoja na kwamba lina umaarufu lakini bado lina ugeni kwa baadhi ya maeneo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kikubwa ambacho tumekifanya kwanza tumeandaa kanuni. Tayari kanuni zipo na katika kanuni zile tayari imeelezwa namna ambavyo tutapita kila kijiji na kila eneo. Hivi tunavyokwambia tayari tumeshashirikiana na Wizara nyingine za kisekta wakiwemo watu wa Halmashauri na Wizara nyingine ili lengo na madhumuni kupitia maeneo yote ya Tanzania hasa kwa upande huo; ili lengo na madhumuni kuwaeleza wananchi fursa na faida zinazopatikana katika biashara ile ikiwa ina mnasaba wa kutunza na kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika maeneo

aliyoyataja yote tutapita, tutatoa elimu, tutawaelimisha wananchi ili waweze kujua fursa na faida zinazopatikana katika biashara hii ya *carbon credit*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamza Khamis kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, litaulizwa na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini.

Na. 109

**Kuwapatia wananchi maeneo kutoka kwenye Hifadhi na Mapori yasiyo na wanyama**

**MHE. VINCENT P. MBOGO K.n.y. MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwapatia Wananchi maeneo ya kulima kutoka kwenye mapori na Hifadhi ambazo hazina wanyama kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ni mojawapo ya wilaya zitakazonufaika na uamuzi wa Baraza la Mawaziri

wa kumega maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za wananchi ikiwemo kilimo, ufugaji na makazi. Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi unatakiwa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya hekta 10,828 zimependekezwa kumegwa kutoka Msitu wa Hifadhi ya Lowasi unaopakana na Pori la Akiba la Lwafi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na makazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Nina swali moja;

Kwa kuwa robo tatu ya Pori Tengefu la Lwafi la Wilayani Nkasi halina wanyama na wananchi wameshaingia wanafanya shughuli zao za kiuchumi; na mipaka hiyo tangu 1948 kipindi cha ukoloni iliwekwa, lakini baadaye ikaja ikabadilishwa ikasogezwa kwa wananchi.

Je, Mhesimiwa Waziri haoni kuwa ni kukwamisha juhudi za wananchi wa Wilaya ya Nkasi wanaojitafutia riziki zao?

Je, ni lini tutakuja kupitia upya ili mipaka irekebishwe, wananchi wameongezeka ili wapate maeneo ya kulima? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vicent Mbogo, Mbunge wa Nkasi, akiwakilishwa na Mbunge wa Nkasi Kaskazini Aida Khenani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wilaya ya Nkasi haina uhaba wa maeneo, isipokuwa kuna changamoto ya mtawanyiko. Wananchi wanaishi pale ambapo wanahitaji kukaa, kitu ambacho tunaipa mzigo Serikali kupeleka huduma kwa wananchi tukiendelea kuwaruhusu waendelee kutokomea kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoelekeza Serikali ni kwamba wananchi wapangwe kwa kuangalia matumizi bora ya ardhi ili kuwepo na miundombinu inayowezesha huduma bora za wananchi ziweze kuwafikia wananchi. Hili swali analolisema kwamba robo tatu ya Lwafi haina wanyama. Ili eneo lihifadhiwe vizuri na ili liwe na madhari nzuri ni pale tu ambapo litaachana na shughuli za kibinadamu. Ndiyo maana yale maeneo ambayo tunayatunza vizuri wanyama huwa wanarudi taratibu na uhifadhi unakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niwaambie tu wananchi wa Nkasi kwamba maeneo ambayo tunayahifadhi mengine tunayachukua yakiwa hayastahili kuwa hifadhi; lakini yanapotunzwa kwa muda mrefu uoto wa asili unarudi, madhari inarudi na wananyama wanaanza kurudi. Kwa maana nyingine wanyama wanatoweka baada ya shughuli za kibinadamu kuingilia maeneo ya hifadhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko nimekuona, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sababu kwa sasa kuna migogoro mingi inayoendelea nchini ambayo inapelekea mpaka mauaji kwenye maeneo ya hifadhi na wananchi;

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kupitia upya sheria za uhifadhi ili ziweze kuendana na nyakati za sasa

na kupunguza migongano kati ya wananchi na wahifadhi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizi Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Pombe Magufuli aliunda Kamati ya Mawaziri nane ambao walipita nchi nzima. Na utekelezaji wake ni kama ambavyo umeona, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetekeleza kwa kwenda kijiji kwa kijiji, kata kwa kata, wilaya kwa wilaya, kutoa ufafanuzi. Yale maeneo ambayo yameonekana wananchi wanaweza kuachiwa; tumeachia jumla ya vijiji 975 vimerudi kwa wananchi. Kuna yale maeneo ambayo ni ushoroba wa wanyama, ni mahitaji mahsusi kwa ajili ya uhifadhi endelevu yamerudishwa kwa Serikali; na ndiyo maana maeneo ambayo tumeyaachia wananchi walishangilia na tulivyokuwa tunapita wananchi wamefurahi kwamba Serikali imewasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya machache ni kwa ajili ya uhifadhi mahsusi ili kutunza vyanzo vya maji lakini kuhifadhi mazingira pamoja na uhifadhi endelevu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Mwita Witara nimekuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ninaipongeza Wizara, walituma timu kwa ajili ya kutatua mgogoro kwenye Hifadhi ya Kitulo na Mpanga Kipengele. Swali langu; ni lini wananchi hawa wa maeneo ya

Ipelele, Ikovo na Mfumbi ambao wanapakana na Hifadhi ya Kitulo pamoja na Pori la Mpanga Kipengele mtawapatia barua, kwa sababu mlionesha nia ya kuwaongeza maeneo, ili waanze kufanya shuguli zao za kichumi kwa kuwa muda mrefu sasa wameendelea kusubiri barua lakini hawajapata maamuzi ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo hili kwamba, Serikali iliunda Kamati ambayo ilienda kufanya tathmini uwandani, na Kamati hii imeshapita maeneo takribani nchi nzima, ikiwemo eneo la Mheshimiwa Sanga. Kwa hiyo, sasa hivi kinachofanyika ni utekelezaji wa uchambuzi uliofanyika uwandani. Wakati wowote naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Kitulo kwamba kuanzia sasa utekelezaji wake utafanyika na tutawajulisha wananchi maeneo husika, kwamba sasa tathmini imeenda hivi. Tutapita pia kijiji kwa kijiji, hifadhi kwa hifadhi, tunashirikiana kuweka vigingi ili kuondoa hii taharuki ya wananchi kutofahamu mipaka halisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Joseph Musukuma nimekuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Hifadhi ya Serengeti na Kata za Nyanungu, Goroma na Kuhihancha, ni mgogoro wa muda mrefu na mipaka iliwekwa mwaka 68 bila kushirikisha wananchi. Naomba nijue Wizara ya Maliasili; ni lini sasa itaenda katika kata hizo ikae na wananchi pamoja bila kutumia mzinga na

bunduki wasikilize wajadiliane kumaliza mgogoro katika eneno hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu mafupi ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna changamoto kubwa katika Jimbo la Mheshimiwa Waitara; na hivi karibuni tu askari wetu ameuwawa kwa kupigwa mshale. Hili kwa kweli sisi kama Serikali tunasikitika sana wananchi wanapojichukulia mamlaka ya kudhuru wahifadhi ambao wanalinda rasilimali zetu sisi kwa faida yao wenyewe. Hili naomba niliseme hadharani kwamba wale askari wako kwa ajili ya kulinda rasilimali za Taifa na si vinginevyo. Kwa hiyo tunaomba tuheshimu mipaka, tuheshimu hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomuua askari hauwezi kuibadilisha ile ramani. Askari atakufa lakini ramani itaendelea kuwepo; ni mpaka pale Serikali itakaporudi kuutatua huu mgogoro. Kwa hiyo tunaomba wananchi wasijichukulie sheria mkononi, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili, nataka nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaenda wenyewe kwenda kutatua ana kwa ana na wananchi na kuwatahadharisha kwamba kuendelea kuua askari wataishia jela, kwa sababu lazima sheria ichukue mkondo wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ningependa kumuuliza swali la nyongeza

Mheshimiwa Naibu Waziri. Naipongeza Serikali kwa kumaliza Mgogoro wa Ngorongoro vizuri kabisa kwa kuwahamisha wale wananchi waliokuwa Kata ya Ngorongoro kwenda Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Nyatwali iliyopo Bunda ni sawa sawa na kata iliyoko Ngorongoro. Ile kata ina hamishwa yote ikiwa na miundombinu ya shule, hospitali na vitu vyote, na ni kata ya enzi na enzi. Hata hivyo, kuna *double standard* ya Serikali. Inaonekana kule watalipwa milioni mbili ilhali kule watu walihamishwa kistaarabu mpaka na ng'ombe wakabebwa kwenye gari.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza Mgogoro wa Nyatwali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musukuma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Nyatwali na vijiji jirani vinavyozunguka kata hiyo, Serikali ilitoa mapendekezo ya kulichukua eneo hilo kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza katika eneo hilo. Wananchi hawa wako kihalali na hii sentensi Serikali kila siku tumekua tukiiongelea; wako kihalali sio wavamizi na vijiji vilivyoko pale vimesajiliwa kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo, Serikali inapoona kuna umuhimu wa eneo lile kulichukua kwa maslahi ya Taifa, hapa nikisema maslahi ya Taifa, tuna *resources* nyingi ambazo tunazitumia kwa maslahi ya Taifa. Kwa hiyo, hata hili eneo tunaliangalia kwa upana zaidi na si kwa wananchi wachache. Kwa hiyo, tunachofanya,

tumefanya uthamini na wananchi waliomba mapendekezo kwamba badala ya heka kulipwa milioni mbili basi wanaomba milioni tatu. Ahadi tuliyoitoa ni kwamba tathmini ifanyike watathmini waingie uwandani waone halafu Serikali itaona nini kifanyike na tutarejesha kwa wananchi mrejesho ambao utakuwa ni muafaka kati ya wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa tahadhari tu, hawa wanaohamishwa ni kwa mujibu wa sheria za nchi. Ngorongoro imekuwa *treated* tofauti na maeneo mengine. Mara nyingi Waheshimiwa Wabunge wanadai pale ambapo wananchi wanahamishwa wanataka walinganishe na Ngorongoro. Suala la Ngorongoro lipo tofauti kabisa na maeneo mengine, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mary Massanja, Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na utalii kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu sasa aulize swali lake.

Na. 110

**Hitaji la taa za barabarani Wilayani Magu**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuweka taa za barabarani katika Miji ya Magu, Kisesa, Nyanguge, Lugeye na Ilungu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Mwanza umepanga kuweka taa katika Miji ya Magu, Kisesa, Nyanguge, Lugeye na Illungu. Uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi unaendelea na unatarajiwa kukamilika tarehe 15 mwezi Februari mwaka huu wa 2023 na kazi inatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu wa 2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Songe kwa niaba ya Mheshimiwa Boniventura Destery.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niishukuru sana Serikali kwa mpango iliyoweka, tuiombe sasa tu zabuni iwahi na mkandarasi apatikane ili wanachi wanufaike na taa hizi za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza mahali hapa. Ni nini sasa Mkakati wa Serikali ya uwekaji wa taa za barabarani kwenye miji iliyoendelea ikiwemo Magu, Busega pale Masanza pamoja na Nasa *Ginnery* lakini pamoja na Itilima Mkoani Simiyu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe tu maelezo kwa ajili ya swali hili. Kwamba kwa sasa Serikali imetoa mamlaka kwa Mameneja wa Mikoa wote wa *TANROADS* kupitia

mikutano ya mifuko ya barabara pamoja na *RCC* kuanisha miji yote mikubwa ambayo imekua na inahitaji taa ili waweze kuziombea hela kwa ajili ya kuweka barabara kwenye miji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa kwa barabara zote ambazo zinajengwa kwa sasa imekuwa ni sehemu ambapo tunapoanza kujenga barabara miji yote inawekewa taa. Kwa hiyo inakuwa ni sehemu ya gharama ya zile barabara. Kwa hiyo ni pamoja na hiyo miji aliyoisema Mheshimiwa Simon Songe, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anton Mwantona na Mheshimiwa David Mathayo nimewaona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini pia namshukuru Rais wa Jamhuri wa Tanzania alipofanya ziara katika Jimbo langu la Rungwe aliahidi kuweka taa katika Mji Kiwila, Mji mdogo wa Tukuyu pamoja na Ushirika.

Je, ni lini sasa taa hizo zitawekwa katika miji hiyo ambayo nimeitaja?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi tunavyoongea miji ya Kiwila, Tukuyu na Ushirika itawekewa taa; na sasa hivi Mkandarasi ameshapatikana, wako kwenye hatua za *mobilization*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Mathayo nilikutaja, Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunapokuwa na taa za barabarani kwanza kuna kuwa na usalama wa wasafiri lakini vile vile wananchi wanafanya shughuli zao za uchumi mpaka usiku kwa sababu kuna usalama.

Je, ni lini Miji ya Hedaru, Makanya, Mji mdogo wa Same, Njoro Kisiwani pamoja na Mwembe watawekewa taa za barabarani?

**MWENYEKITI:** Tutulizane Waheshimiwa, naomba tutulizane, tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Mathayo David, Mbunge wa Same, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, miji aliyoitaja, Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro ameshawasilisha maombi na tunategemea fedha itaenda mwaka huu ili miji hiyo iweze kuwekewa taa kwa ajili ya usalama lakini pia na kupendeza miji aliyoitaja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tarehe 22 Mwezi wa Nane 2022 Serikali ya kuanza kujenga Barabara ya Morogoro – Njombe *boarder* kwa kiwango cha kilometa 100 kutoka Ifakara kwenda Chita.

Je, Wananchi wa Mlimba wangependa kujua taa inaweza kuwa *component* kwenye tenda hasa kwenye maeneo ya miji kama Mchombe na Mgeta na Mlimba Mjini? Ahsa nte.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa sasa barabara zote ambazo tunazi – *design* na kuzijenga, miji yote ambayo inapitiwa na hiyo barabara inawekewa taa. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba, kwamba miji yote ambayo itapitiwa na hiyo barabara kilometa 100 taa itakuwa ni sehemu ya hiyo kandarasi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Godfrey Msongwe, kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 111

**Wakulima wa zao la Mwani**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wakulima wa zao la Mwani ili kuongeza tija?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023 Serikali imetenga fedha za *program* maalum ya Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* kupitia dirisha la *Extended Credit Facility (ECF)* kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wa mwani pembejeo kwa mkopo wa masharti nafuu na usio na riba kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa awamu ya kwanza, Wizara itatoa pembejeo za mwani zenye thamani ya shilingi 447,251,244 kwa wakulima 343 waliokwenye vikundi katika wilaya saba za Muheza, Pangani, Mtama, Mkuranga, Kilwa, Lindi Mjini na Mtwara Vijijini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutenga hizi fedha milioni 400 kwa ajili ya wakulima wa mwani, lakini fedha hizi bado ni chache, hazitoshi. Wanawake wa pembezoni mwa ukanda huu wa bahari wamehamasika sana kulima mwani;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanakwenda kuwaongezea fedha ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili, pamoja na akina mama kuhamasika kulima mwani bado kuna changamoto kubwa ya soko;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunganisha wakulima wa mwani pamoja na masoko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kweli, na ndiyo maana katika jibu la msingi nimesema hii ni ya awamu ya kwanza; lakini awamu ya pili ambayo tayari maandalizi yake yamekwisha kukamilika ni jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.5 zitaongezwa. Na kwa hili tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kwenye *program* hii iongezwe fedha ambayo itakawenda kuongezeka kwa vikundi kadhaa vya kina mama watakao nufaika na mkopo huu usio na riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni changamoto ya soko. Upande wa soko unakwenda sambamba na upande wa uzalishaji. Kwa hatua tunayoiendea ya kuongeza uzalishaji imevutia wanunuzi wakubwa wengi. Hivi ninavyozungumza, ushindani juu ya ununuzi wa zao la mwani umeanza. Kampuni zimekwishafikisha bei ya mwani aina ya *spinosum* shilingi 900

na kwa upande wa aina ya *cottonii* ni shilingi 200. Kwa hiyo tunakwenda vizuri. Kwa upande wa Serikali tumejipanga kujenga maghala lakini pia vile vile kutengeneza mashine kwa ajili ya ukaushaji wa mwani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakuona Mheshimiwa Juma Usonge, Mheshimiwa Asya Mwadini atafuata.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana namimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tumekuwa tukishauri sana hususan sisi Wabunge ambao tunatokea mwambao wa Pwani kuhusiana na bei ndogo ya mwani.

Je, Serikali haioni haja sasa kufungamanisha mfumo huu wa ununuzi wa mwani na mfumo wa stakabadhi ghalani ili kupunguza utitiri wa wanunuzi ambao wamejipangia bei ndogo na kumuumiza mkulima wa mwani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi nimeeleza, mkakati wetu ni pamoja na kujenga maghala. Hili la kujenga maghala ni kuelekea katika kile alichokishauri Mheshimiwa Mbunge, ya kwamba tunaweza pale mbele kwenda katika mfumo wa kuliingiza zao la mwani katika stakabadhi ghalani. Tukijenga maghala na tukaongeza uzalishaji tutafanikiwa kufika katika hatua ile aliyoishauri Mheshimiwa Juma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, nimekuona.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Bagamoyo Kata ya Zinga, Kijiji cha Mlingotini, kuna wakulima mahiri kabisa wa mwani.

Je, ni lini Serikali itawapatia vifaa husussan boti ili waweze kufika katika maeneo ya uzalishaji kwa urahisi zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muharami Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna chama kikubwa na cha mfano cha ukulima na uchakataji wa mazao yatokanayo na mwani, kinaitwa Chama cha Ushirika cha Msichoke kilichopo Mlingotini – Bagamoyo kimeomba jumla ya fedha shilingi milioni 40. Chama hiki kitapata fedha hizi hapa karibuni kwa lengo la kununua boti itakayowawezesha kina mama wale kuingia baharini kwenda kuchukua mazao yale na vile vile kamba na taitai na zana zingine. Hongera sana Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bagamoyo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani nilikuona.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wizara ya Mifugo imekuwa ikitoa ahadi kwa wananchi wa Ushetu kwa ajili ya kuwajengea majosho. Hata Mheshimiwa Mpina wakati akiwa Waziri alishafika Kaya za Nyankende, Ulewe na Ubagwe akaahidi lakini utekelezaji wake mpaka sasa hivi hakuna. Nataka nipate kauli ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, *commitment* ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imefanikiwa kupeleka jumla ya fedha shilingi milioni 540 kwa ajili ya ujenzi wa majosho katika halmashauri mbalimbali nchini, na bado kiasi cha shilingi takribani milioni 100 zipelekwe pia. Ninaamini Wilaya ya Ushetu ni miongoni mwa Wilaya ambazo ni wanufaika. Naomba mara baada ya hatua hii ya Bunge nikutane na Mheshimiwa Mbunge Cherehani aweze kunipatia orodha ya vile vijiji vyake ili niweze ku-*cross check* kwa ajili ya ufuatiliaji wa ujenzi wa majosho haya ya wananchi wa Ushetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Asya Mwadini nilikutaja.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mwani unatambulika duniani kwamba ni zao kubwa ambalo linawasaidia akina mama kulima lakini linaweza kutupa bidhaa kama vipodozi, vyakula na vitu vingine.

Je, Serikali haioni sasa kuanzisha kiwanda ama viwanda nchini vya kuchakata mwani ili tuweze kuzalisha bidhaa hizi ndani ya taifa letu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asya Mwadini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwani hutumika kwa ajili ya kutengeneza kimiminika kizito ambacho

hutengenezea vipodozi, na pia vile vile hutumika kama sehemu ya kutengenezea vyakula hususan kama *ice cream* na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tunao mpango wa kukutana na wazalishaji wa ndani ya nchi wanaotumia malighafi hii kwa lengo la kuwahamasisha kuingia katika utaratibu ambao utapelekea wakulima wetu waweze kuchakata na kuwauzia wao wanaotumia ndani ya nchi kama vile kampuni za utengenezaji wa vipodozi na kampuni za utengenezaji wa vyakula. Ndiyo maana katika mkakati wetu tumeweka mashine za ukaushaji na hatimaye kutengeneza mpaka katika kufikia hatua ya kuwa kimiminika kizito kitakachokwenda kutengeneza *colgates* na vipodozi kama vile *lotions* lakini vile vile kwa ajili ya kutengenezea *ice creams.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando sasa aulize swali lake.

Na. 112

**Mpango wa kuongeza magari ya kisasa ya Zimamoto**

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza magari ya kisasa ya zimamoto?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imekamilisha hatua zote za mkopo wa *Euro* milioni 4.9 kutoka Nchini Austria kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya kuzima moto. Kati ya magari yanayonunuliwa mawili ni ya ngazi *(Turntable ladder)* kwa ajili ya kuzima moto katika majengo marefu. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokozi linatarajia kupata magari matatu ya kuzimia moto ambayo yalipatikana kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 kutoka Shirika la *Nyumbu Tanzania Automotive Technology Center (TATC)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salim Mussa Omar.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nipende tu kuishukuru na kuipogeza Serikali kwa majibu yake mazuri. Hata hivyo, kwa idadi ya magari haya ambayo yameoneshwa hapa katika mpango wao wa kuyaleta, bado kwa tathmini ni machache mno. Ningependa tu kuiomba Serikali tuendelee kutenga fedha kwa wingi ili kuweza kuweka mazingira ya usalama wa wananchi wa Tanzania na mazingira salama ndani ya taifa letu la Tanzania. Suala la zimamoto limekuwa ni changamoto kubwa ya siku nyingi na ni lazima iweze kuchukuliwa *serious,* ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ni ushauri huo Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilimwona Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru saba kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa mikoa ambayo inategemea sana uchumi wa misitu; mikoa ya nyanda za juu Kusini na hasa Mkoa wa Njombe, wananchi wamepata umasikini mkubwa sana kutokana na moto ambao unatokea mwaka baada ya mwaka. Serikali ina mpango gani wa kuwa na mkakati wa

kusaidia kwa kuleta vifaa vya kisasa kwenye maeneo hayo ambayo yanashambuliwa sana na moto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayoyasema hutokea kwenye mikoa na wilaya nyingi zenye misitu. Kwa kutambua hilo ndiyo maana Mkoa wa Njombe hadi sasa wanayo magari mawili, moja liko Njombe Mjini na lingine liko Makambako. Ni dhamira ya Serikali kadiri uwezo wetu utakavyoongezeka wa kununua magari ya kuzimia moto, Mkoa wa Njombe pia utazingatiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 113

**Kudhibiti kuhama kwa Mto Ruvu-Kibaha**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti kuhama kwa Mto Ruvu-Kibaha ili kuzuia uharibifu wa mashamba na miundombinu ya Reli ya *SGR*?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael

Costantino Mwakamo Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Ruvu eneo la Kibaha hadi Bagamoyo umekuwa na kawaida ya kuhamahama kwa vipindi tofauti tofauti kutokana na kuwa katika uwanda wa chini karibu na Bahari ya Hindi. Hali hii hupunguza kasi na kufanya udongo kutuwama ndani ya mto na kusababisha mto kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na kazi ya kunyoosha mto pamoja na kuimarisha kingo zilizoathiriwa kwa kuweka *gabions* na njia mbalimbali, ikiwemo upandaji wa miti pembezoni mwa mto na kwenye vyanzo vya maji, kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuhifadhi vyanzo vya maji, kuiwezesha jamii kutekeleza shughuli mbalimbali za kujipatia kipato ili kuondoka ndani ya vyanzo vya maji. Kuweka alama na mipaka na mabango ya makatazo ya kuzuia kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi ya vyanzo vya maji ili kurudisha uoto wa asili na kupunguza athari za mmomonyoko. Jitihada hizi zitaepusha mashamba katika eneo hilo kuathiriwa na maji ya mto Ruvu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa majibu mazuri, lakini niongezee nyongeza moja kwamba hadi leo hii lile eneo ambalo tulilizungumza na liliuliziwa swali, Serikali imetekeleza vizuri na limeziba lile eneo, kwa hiyo tunawapongeza sana. Swali moja dogo la nyongeza; kwa kuwa wakulima wa bonde hilo walikuwa wanazuiwa kuendeleza shughuli zao za kilimo katika maeneo hayo kutokana na Mto Ruvu kupungua kasi yake ya maji na sasa eneo lile limeshazibwa.

Je, Serikali inampango gani sasa wa kuwasaidia wakulima wale waendelee na shughuli zao za umwagiliaji mdogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kushukuru kwa kupongeza jitihada kubwa ambayo taasisi ya *DAWASA* imeweza kufanya na sasa maji hayatapakai tena. Vile vile Serikali ina mipango mbalimbali kuhakikisha suala la maji kuchepuka kutoka kwenye mto tunakwenda kulidhibiti. Hili tutalifanya kwa kutumia Bonde la Maji ya Wami-Ruvu na tayari wameshapata mhandisi mshauri ambaye anafanya usanifu kwa ajili ya kujenga bomba kuu moja ambalo wananchi watapaswa kujiunga katika kikundi kimoja ili waweze kuhudumiwa kwa sehemu moja halafu wao sasa ndio watachepusha kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuipatia Wizara fedha. Tayari tumeshaingiza mitambo ya kuchimba mabwawa na tunatarajia kama Wizara tuweze kuchimba mabwawa madogo madogo ambayo nyakati za mvua tutaweza kuvuna maji, tutayahifadhi pembezoni mwa mto huko ili wananchi waweze kuja kuyatumia kwa ajili ya umwagiliaji na wasiweze kudhuru mto katika shughuli za kuleta chanzo cha maji kwa shughuli za kibinadamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis Londo nimekuona.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vijiji vya Changarawe katika Kata ya Masanze na Vijiji vya Malangali, Muungano, Mamoyo, Kibaoni na Maluwi katika Kata za Tindiga na Mabwerebwere mito yake imepoteza

mwelekeo, inahatarisha maisha ya watu. Sasa nilikuwa naomba kuuliza Serikali;

Je, ni madhara kiasi gani kwa wananchi wetu yatokee ili Serikali ichukue hatua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Londo (Mb) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba, ni kiasi gani cha madhara ili Wizara iweze kuchukua hatua. Wizara hatusubiri madhara lakini tayari tunachukua hatua kwa kutimiza majukumu yetu kuhakikisha maji hayawi laana, maji ni neema. Maeneo ambayo maji yanachepuka na kusababisha maeneo ya wananchi kuvamiwa tayari tumeyapa kipaumbele. Kwa maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, hasa Mto Miombo ambao unasababisha madhara kwenye kata alizozitaja ya Masaza, Masava na nyingine tayari mkandarasi yupo *site* anafanya utafiti. Lengo ni kuona maeneo yote ambayo yanaathirika na maji yanapochepuka kwenye mto hasa nyakati za masika tunakwenda kuyadhibiti, yanaenda kutumika vizuri kwa shughuli za kibinadamu. Shughuli ambazo zinafanyika na wananchi hawa za mboga mboga, kilimo kidogo kidogo basi yote yatajengewa miundombinu rafiki ili kulinda mto kwa sababu kulinda vyanzo vya maji ni jukumu letu sote.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji, *Engineer* Maryprisca Mahundi kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 114

**Elimu ya ugonjwa wa Fistula**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu juu ya ugonjwa wa fistula?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupambana na ugonjwa wa fistula Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa njia zifuatazo: -

a. Kuzuia mimba za utotoni kupitia elimu ya uzazi kwa vijana.

b. Kuwaelemisha akinamama kuhudhuria kliniki mapema ili wapate huduma muhimu na kupata ushauri wa mpango wa kujifungua.

c. Kutoa elimu kwa wajawazito kujifungulia katika vituo vya afya ili kuwahi kupatiwa msaada kama kutatokea tatizo la uchungu pingamizi au jingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Tanzania, ugonjwa huu wa fistula ni ugonjwa ambao unasumbua sana.

Je, ni hospitali ngapi au zipi zenye wataalamu wa kutibu ugonjwa wa fistula zilizoko nchini ukiondoa Hospitali ya *CCBRT?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Ukiangalia sana ukizingatia haki za binadamu huu ugonjwa huwezi kumsafirisha mgonjwa kukiwa katika magari ya kawaida.

Je, Serikali imejipangaje kutoa usafiri maalum kwa ajili ya watu hao na namna ya kujikimu ili kutoka sehemu moja na kwenda nyingine ukizingatia waliowengi hali zao ni duni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa kufuatilia haya mambo ambayo kwa kweli yanawasumbua akina mama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza ni hospitali ngapi; hospitali zetu zote za mikoa, kanda na taifa zinatoa huduma hiyo. Kumekuwepo kila wakati sasa hivi madaktari kutoka Hospitali ya Muhimbili na hospitali zetu za kanda wakienda kwenye hospitali za mikoa yetu ili kuendelea kuongeza nguvu na ujuzi kwa hospitali zetu za mikoa ili huduma hii iweze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge; moja tuna mkakati kwamba magari yanapita kuhamasisha mtaani. Pia akipatikana mgonjwa yeyote huwa *ambulance* inamfuata na kupelekewa sehemu husika. Hata hivyo, ninajua kwamba kwenye eneo hilo bado hatujajiimarisha vizuri. Hivyo,

tunachukua wazo lako ili tuweze kulifanyia karibu kwa kushirikiana na hospitali zetu za wilaya ili akina mama wale wakionekana waweze kupelekwa bila kupitia mabasi ya kawaida, waende kwa kutumia gari za Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan nimekuona.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tunajua ugonjwa huu unawasumbua akina mama wengi sana wakati wa kujifungua.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuongeza huduma za tija kwenye Hospitali za Mikoa ya Kusini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBI WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inaongeza, na unapozungumzia kusini ndio maana kuna Hospitali ya Kanda ya Mtwara Kusini kule, ambayo kwa kweli inajengewa uwezo mkubwa kama hospitali zingine za kanda. Moja kutoa huduma lakini pia kujenga uwezo kwa hospitali za upande huu kwa chini ili waweze kutoa huduma hiyo. Pia kwa muda wa miaka hii miwili vimejengwa vituo 862; na kati ya hivyo 421 vimewekewa sehemu za kupasua akina mama ili kuwanusuru na hili jambo. Tutaendelea kufanya hivyo ili kuweza kuwanusuru akina mama. Kwa hiyo kuna mkakati wa nchi nzima si suala la Kusini peke yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo nilikuona.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ilivyo ugonjwa wa fistula pia maambukizi ya virusi vya UKIMWI bado ni janga kwenye nchi yetu, lakini

inaonekana kama Serikali imelegalega katika kutoa elimu. Mimi nataka kujua;

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuendelea kutoa elimu ya kujikinga na virusi vya UKIMWI kwa wananchi wetu wa Tanzania?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBI WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani anachosema, Serikali haijalegalega lakini ni *strategy* tu zimebadilika kwa ku-*approach* kulingana na hatua ambazo tumefikia. Kwa sababu ukiangalia hali ya maambukizi sasa hivi imeshuka sana na hali ya maambukizi ni makubwa kwa makundi maaulum na nguvu zinaelekezwa kwenye makundi maalum kuhakikisha hali hiyo inadhibitiwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Daktari Christine Gabriel Ishengoma Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 115

**Upanuzi wa Hospitali ya Rufaa Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafanya upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya majengo ya huduma za dharura, huduma za wagonjwa mahututi, huduma za mionzi ambapo majengo haya yamekamilika na yanatumika. Pia ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.8, umefanyika. Pamoja na maboresho hayo, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 350 kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la upasuaji wa mifupa ambapo jengo hili litakamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya usanifu wa majengo yanayokusudiwa kujengwa ikiwa ni sehemu ya mpango wa upanuzi wa hospitali hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo. Swali la kwanza; licha ya mpango mzuri na unaoendelea wa upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro lakini kuna mpango wa kujenga Hospitali ya kisasa ya Rufaa ya Mkoa wa Hospitali ya Morogoro.

Je, ni lini ujenzi huu utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Kituo cha Mafiga Manispaa ya Morogoro wanawake wengi wajawazito wanapenda sana kujifungulia kwenye kituo hicho lakini tatizo mojawapo linalojitokeza kituo hiko hakina jengo la upasuaji.

Je, kuna mpango gani wa kuweka jengo la upasuaji katika Kituo hicho cha Mafiga? Ahsante sana,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge nikupongeze. Unakumbuka ulikuja na ukaniambia na tulikwenda hospitali ya mkoa na uliona miundombinu na uwekezaji mkubwa ambao umefanyika kwenye hospitali yenu ya mkoa. Najua lengo lenu, pamoja na upanuzi unaozungumziwa kwenye eneo hili la hospitali mnahitaji kujenga hospitali nyingine eneo lingine. Mimi nikuombe, kama nilivyosema hapa, majadiliano yanayoendelea kati ya Wizara na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro tukiyamaliza basi tutakaa pamoja ili tuweze kwenda *forward* tukiwa pamoja. Kwa sababu sasa hivi nikikupa majibu inawezekana huo mchakato wa kimkoa wakawa na mawazo mengine tofauti na hayo ambayo wewe unayo. Kwa hiyo tutashirikiana kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili unazungumzia kwamba pale kwa akina mama hakuna jengo la upasuaji. Mheshimiwa Mbunge naomba nikimaliza hili swali tukae mimi na wewe tukae na *TAMISEMI* tuweke mkakati wa pamoja tuhakikishe hicho unachokisema kinaenda kutokea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo nimekuona.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali anayoiongoza kwa kutupatia fedha za kumalizia jengo la mtoto katika Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro, Hospitali ya Mawenzi. Tangu alipoitembelea

Octoba 2021 fedha zimekuwa zikija na fedha za UVIKO zimekuja, na sasa jengo lile linamalizika.  Sasa swali langu ni;

Je, ni lini Serikali itaanza mpango wa kuitengeneza *master plan* ya hospitali ile upya ili kuondoa yale majengo ya zamani na kuweka majengo mapya ya ghorofa yanayoendana na hospitali za kisasa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBI WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie Mbunge Rais wetu Daktari Samia Suluhu Hassan alipotembelea pale Hospitali ya Mawenzi yeye aliomba mambo kadhaa na mambo hayo Rais wetu ameshatoa hela. Aliomba bilioni sita ya kumalizia jengo la mama na mtoto na tayari bilioni sita zimekwenda. Pia aliomba *CT-Scan,* tayari imekwenda, aliomba bilioni 1.3 kwa ajili ya *emergency department* imeshajengwa na bilioni 1.3 imekwenda, na jana zimekwenda bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza kazi ambayo unasema kwamba kubomoa yale majengo ya zamani na kunyanyua mengine ambayo yatafanya ile hospitali iwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja tu ambalo tunaenda kutekeleza kabla ya Juni mwaka huu ambalo ulimwomba Mheshimiwa Rais; la ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha gesi tiba, hilo litaenda kutekelezwa kabla ya Juni na kazi itaenda pale vizuri sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kazi uliyomwomba Rais inaendelea kufanyika na ahadi amezitekeleza takriban zote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang’ata nimekuona.

**MHE. BUPE N. MWAKANG’ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa

Hospitali ya Rufaa Mkoani Rukwa kwa sababu tayari uwanja ulishapatikana na ufundi sanifu ulishafanyiwa. Je, ni lini Serikali sasa itaanza ujenzi wa hospitali hiyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBI WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa anachosema na usanifu ni kweli umefanyika kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema. Kwanza nimpongeze kwamba anafatilia masuala mazima ya afya ya hopsitali yao ya mkoa. Kwa mwaka huu zimetengwa bilioni 5.5 kwa ajili ya hospitali anayosema na usanifu anaouzungumzia unaenda kufanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya Daktari Godwin Mollel. Tuaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge wa Mkinga aulize swali lake.

Na. 116

**Mpango wa kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Maji ya Umwagiliaji ya Mwakijembe**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mwakijembe pamoja na bwawa la kukinga maji?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Mavunde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu ya umwagiliaji inakadiriwa kuwa na jumla ya hekta 450. Hekta 200 katika Kijiji cha Mwakijembe na hekta 250 katika Kijiji cha Mbuta ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji wa mazao makuu yakiwa ni mahindi, maharage na mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu zilizopo katika Bonde la Mto Umba ikiwemo skimu ya Mwakijembe kwa lengo la kupata gharama halisi za ujenzi. Baada ya kukamilisha zoezi la upembuzi yakinifu na usanifu wa kina skimu hii itaingia katika mpango wa ujenzi wa mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Skimu ya Mwakijembe wananchi wamekuwa wanasubiri kwa takriban miaka 14 sasa. Na kwa kuwa Bunge hili lilipitisha fedha mwaka huu kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu.

Je, Waziri yuko tayari kwenda kusimamia jambo hili ili upembuzi huo na usanifu ukamilike ndani ya mwaka huu tuliotengea fedha na mwaka ujao wa fedha kazi hii ya ujenzi iweze kuanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili skimu hii ilitumia zaidi ya bilioni moja na milioni mia mbili, fedha ambazo ni kama zilipotea kwa sababu skimu haijaweza kufanya kazi.

Je, Wizara iko tayari kwenda kuangalia kwa kina *design* itakayofanyika ili *design* hiyo ihusishe ujenzi wa bwawa la kuhifadhia maji na ujenzi wa mifereji ili skimu iweze kutumika kwa uhakika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge Mkinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri Mheshimiwa Mbunge amekuwa mfatiliaj mzuri wa jambo hili; na ni kweli skimu hii imekaa muda mrefu. Kulikuwa na changamoto nyingi na hasa kutokana na kwamba katika miaka mingi iliyopita tume yetu haikuwa na uwezo mzuri sana ya kuweza kuisimamia miradi hii mikubwa. Hata hivyo tumefanya mabadiliko makubwa ambapo hivi sasa tumeshamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuhakikisha ya kwamba wanaipa kipaumbele skimu hii. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha tunafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili changamoto zilizokuwa zinajitokeza katika miradi iliyopita zisiweze kujirudia, na ikiwemo hoja ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema, ya ujenzi wa mabwawa ili kuhakikisha upatikanaji wa maji wa mwaka mzima na wakulima wa eneo hilo waweze kufanya kilimo kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tutasimamia kwa ukaribu kabisa kazi hizi

zifanyike mapema ili basi tutenge fedha kwa ajili ya ujenzi na wananchi waweze kunufaika na mradi huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Anthony Mavunde kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mohamed Said Issa Mbunge wa Konde aulize swali lake.

Na. 119

**Vigezo vya msamaha wa Kodi ya *VAT* kwa viwanda nchini**

**MHE.OMAR ALI OMAR K.n.y. MHE. MOHAMMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, ni vigezo gani Serikali inavitumia kusamehe kodi ya VAT kwa viwanda mbalimbali nchini ili kuleta usawa kwa wote?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Said Issa, Mbunge wa Konde kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani umewekwa kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148. Sheria imeelezea kwa kina vigezo vinavyotumika kutoa misamaha ya Kodi ya *VAT*. Vigezo vinavyotumika kusamehe *VAT* kwa sekta ya viwanda ni kama ifuatavyo: -

i. Uagizaji wa malighafi zinazotumika kutengenezea vyandarua;

ii. Uagizaji au usambazaji wa bidhaa au huduma kwa Serikali zitakazotumika kwenye miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali, mikopo na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

iii. Uagizaji au usambazaji wa bidhaa au huduma kwa ajili ya unafuu wa majanga ya asili; na

iv. Uagizaji au usambazaji wa bidhaa au huduma kwa kampuni yenye makubaliano na Serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Ali Omar kwa niaba ya Mheshimiwa Mohamed Said Issa swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni viwanda vingapi vya wazawa ambavyo vimepata msamaha huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, vimewasaidiaje viwanda hivyo? ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri; rudia tena Mheshimiwa Omar.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza;

Je, ni viwanda vingapi vya wazawa ambavyo vimefaidika na msamaha huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali imevisaidiaje viwanda hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri swali la kwanza ni la takwimu kama unazo utatoa kama huna utaleta baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli swali la kwanza ni suala la takwimu naomba hili tulichukue tutampelekea kwa maandishi. Swali la pili, ni hakika kabisa viwanda vyote vya wazawa nchini vinapata misamaha kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa majibu hayo tunaendelea na Wizara ya Madini Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo aulize swali lake.

Na. 120

**Madini yanayopatikana katika Mkoa wa Rukwa**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, kwa mujibu wa tafiti ni madini aina gani yanapatikana katika Mkoa wa Rukwa na katika maeneo yani?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Jimbo la Kalambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa iliyobarikiwa kuwa na madini ya aina mbalimbali. Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST)* mkoa huu una madini yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhahabu katika kata za Kabwe, Namanyere, Msenga na Ninde. Shaba katika Kata za Kirando, Namanyere, Msenga, Kala na Ninde. Risasi katika Kata za Namanyere na Ninde, Makaa ya Mawe katika Kata za Chala, Kipande, Muze na Ntendo. Madini ya viwandani kuna chokaa Kata ya Ntendo, na Kyanite Kata ya Msenga. Chumvi Kata za Kirando, na Kipeta. Ulanga Kata za Mkwamba, Mwazye, Kaoze na Senga. Vito katika Kata za Chala, Kipande, Senga na Malangali. Rare Earth Elements Kata za Mkwamba na Msenga. Chemichemi za majimoto zenye kuambatana na gesi ya helium katika Kata za Kirando na Msenga, na Chuma katika Kata ya Katazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini mengine ni madini ujenzi ambayo ni kokoto na mchanga ambayo yanapatikana katika Wilaya zote za Mkoa wa Rukwa ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na ninaomba niishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri ambayo yamesheheni taarifa za kutosha. Naomba niulize maswali madogo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba pamoja na hayo madini ambayo yametajwa kwa idadi kubwa shughuli ya uchumi kwa maana ya uchimbaji haijaanza kufanyika, na hii inawezekana ni kwa sababu hamasa na elimu haijatolewa kwa ajili ya wananchi kuweza kuchimba.

Je, Serikali iko tayari kutoa hamasa na elimu ili wananchi waanze kuchimba madini hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika taarifa ambayo imetajwa na Serikali imetajwa kwa ujumla kwa mfano Kata ya Katazi.

Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti wa kina kujua *exactly deposit* hiyo inapatikana wapi? ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la kwanza; ni kweli uchimbaji bado haujapata kasi katika wilaya yake, lakini nimhakikishie kwamba, kama ni kutokana na uelewa mdogo Tume ya Madini wamejipanga kuzunguka nchi nzima kuhamasisha wachimbaji wadogo katika maeneo yenye madini ili waweze kujipanga waunde vikundi na tuweze kuwasaidia kwa ukaribu wafaidike na madini waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili ni kweli taarifa hizi tulizozitoa hapa ni taarifa za utafiti wa awali unaofanywa na taasisi yetu ya *GST,* lakini utafiti wa kina ufanywe kwa kutumia vifaa vya kisasa vya uchongaji. Na

kutambua umuhimu wa kuwasaidia wachimbaji wadogo Wizara ya Madini imeagiza kupitia Taasisi yake ya *STAMICO* mitambo mitano ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wafahamu kiwango cha madini kinachopatikana katika maeneo yao ili wanapokwenda kuanza kuzalisha wachimbe madini wakiwa na uhakika kwamba watapata tija kutokana na juhudi zao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Madini kwa majibu hayo tunamalizia na Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 121

**Tatizo la mirathi kwa wajane**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza: -

Je, Serikali inawasaidiaje wajane ili kuondoa mila na desturi potofu zinazomkandamiza Mwanamke kwenye suala la mirathi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo Mbunge wa viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa wajane na katika kulinda haki zao kwa kutunga Sheria mbalimbali na Kanuni za kulinda haki za Wanawake wajane katika uuala zima la mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mila na desturi potofu ni eneo ambalo Serikali imeanzisha mchakato wa mapitio ya sheria za kimila ili kuondoa aina yoyote ya ukandamizaji kwa wajane katika suala la mirathi. Serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu Sheria ya Mirathi hususani umuhimu wa kuandika wosia ili kuondoa changamoto zinazotokana na mila na desturi potofu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa maswali madogo mawili ya nyongeza.

Je, Serikali inampango gani kuajiri wanasheria ambao wanaweza kusaidia kuleta elimu ya mirathi katika ngazi ya kata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana na inatia huzuni wanawake wajane baadhi yao wamejikunja hawajui hatima yao kwasababu wanadhurumiwa haki zao za mirathi, hivyohivyo wanakuwa wanateseka kwa namna hata ya kusomesha Watoto wao;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaleta sheria ambayo itasaidia kuleta mpango mkakati kwa ajili ya kunusuru ndoa na mirathi ili kuepusha changamoto za mirathi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuajiri wanasheria katika ngazi ya kata, kimsingi kule tuna Mahakama ambapo shughuli zote za kimahakama zinafanywa katika maeneo yale, na wale mahakimu ni watalamu ambao wamehakikiwa. Tunakwenda kubadili Sheria ile ya Wazee wa Baraza na badaye kuruhusu wanasheria binafsi vilevile kwenda kusimama kwenye mahakama hizo ili kuwasaidia wananchi wengi ambao wangehitaji msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo suala la ule mkandamizaji napenda nitumie nafasi hii kuanza kuwafahamisha wananchi wote; kumekuwa na mkanganyiko tu wa akili za wananchi wachache wenye tamaa, unapopewa nafasi ya kuwa msimamizi wa mirathi huko ndiko kunako anzia tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamizi wa mirathi si mrithi. Msimamizi wa mirathi kazi uliyopewa ni kukusanya mali za marehemu na kusimamia warithi kupata kwa kuzingatia haki zao na mrithi namba moja kwenye haki za mirathi ni mke wa marehemu, watoto wa marehemu ndilo kundi la pili na kundi la mwisho ni wazazi wa marehemu, kama wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kinachotokea sasahivi ni kwamba mtu akipewa tu nafasi ya kusimamia mirathi, anaanza kujirithisha yeye mwenyewe. Huyu ni mwizi na anastahili kushtakiwa kama mwizi wa kuaminiwa. Hili ndiyo jambo ambalo kimsingi linakera sana kwenye jamii zetu. Akina mama wengi wananyanyasika katika mazingira kwamba shemeji aliye aminiwa na ile familia kusimamia na kukusanya mali za marehemu yeye mwenyewe ndiye anabaki katika mazingira ya kurithi na kuila ile mali ya wale walengwa ambao kimsingi wanakuwa ni familia ile ya marehemu iliyoachwa baada ya kifo cha wazazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni jambo tu la uelewa, hakuna mtu mwingine yeyote mwenye haki ya kurithi mali iliyoachwa na marehemu nje ya hao niliowataja. Kuna mila nyingine ni potofu sana; kwa mfano kuna mila ambazo zinamfanya mtu anaitwa mrithi awe na sauti asilimia mia kwenye mali zile. Ile si urithi wa kisheria. Urithi wa kisheria unaotambuliwa ni mke, watoto na mzazi wa marehemu; na katika mgao mzazi wa marehemu anapata kiasi kidogo sana kuliko watoto na mke wa marehemu kwasababu mke wa marehemu anakuwa bado anaendelea kuilea ile familia ambayo imeachwa na yule marehemu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Mizengo Pinda ahsante sana. Hilo ndilo swali letu la mwisho kwa siku ya leo.

Sasa hivi tunaingia wakati wa matangazo, na hapa tuna matangazo ya leo; kuna wageni waliyopo Bungeni asubuhi hii. Kuna wageni kwanza waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Wageni wa Mheshimiwa Spika ni Mwakilishi Mkazi wa Taasisi ya Aga Khan Nchini Tanzania Mheshimiwa Amin Kurji, yuko pale, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Ndugu Ambulance Amos, Mwanamuziki wa Bongo Fleva kutoka *Jajoji Music Label,* karibu sana mwanamuziki wetu. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni 31 wa Mheshimiwa George Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Mkesha wa Kuliombea Dua Taifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati Kitaifa Askofu Dkt. Godfrey Malassy. Wanamaombi wetu karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Taasisi ya *The Launchpad Tanzania* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wengine wageni watatu wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Wako pale karibuni sana wanafamilia wetu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Maryprisca ni *Jibu Music Africa* kutoka Jijini Dar es Salaam, hao hapo karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 29 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana Madiwani wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni Maafisa Watendaji wa Kata kutoka Halmashauri ya Msalala Mkoa wa Shinyanga, karibuni wageni wetu kutoka huko Msalala. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni Makatibu wa CCM Kata ya Moshi Mjini kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana wageni wetu kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam na Zanzibar. Wanafamia wa Mheshimiwa Malembeka karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wawili pia wa Mheshimiwa Mwanakhamisi Said ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar Mjini. Watoto, yule pale namuona mmoja, yuko pale mmoja

mtoto wa Mheshimiwa Mwanahamisi Said, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 50 wa Mheshimiwa Mrisho Gambo ambao ni Viongozi wa Jumuiya yetu ya Wazazi Wilaya ya Arusha, karibuni sana viongozi wetu wa wazazi kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Michael Mwakamo ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Wako pale karibuni sana ndugu wa Mheshimiwa Mwakamo. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Venant Protas ambaye ni Ndugu Chichi Hilda Banda kutoka Dar es Salaam ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano *Tanzania Commercial Bank*. Yule pale karibu sana mgeni wetu. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambaye ni mama yake mzazi Ndugu Faustina Bikasa, karibu mama yetu mzazi katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni wapiga kura wake kutoka Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Wapiga kura wa Mheshimiwa Muharami karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna wageni wanane wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dodoma. Wageni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambaye ni mtoto wake kutoka Kasulu, Mkoa wa Kigoma Ndugu Elisha Mbatari, yule pale, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wametembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 50 na walimu watano kutoka *Independent School* ya Jijini Dar es Salaam. Wale pale karibuni sana wanafunzi kutoka shule hiyo ya *Independent School. (Makofi)*

Vilevile pia tuna wanafunzi 75 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma kozi ya Uhusiano wa Kimataifa wakiongozwa na Ndugu Kelvin Jackson, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma.

Katibu tuendelee!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022 na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na hoja zetu za Kamati leo tuna Kamati ya Katiba na Sheria naomba nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama karibu.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyo wasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Shughuli za Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni kinaipa Kamati hii jukumu la kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Wizara zifuatazo: -

Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya pili ya taarifa yetu inahusu shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa masuala yaliyobainika. Sehemu ya kwanza inahusu uchambuzi wa miswada ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilijadili Miswada ya Sheria Nne kama ifuatavyo: -

i. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 7 ya mwaka 2021.

ii. Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mafaa wa mwaka 2022.

iii. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 2 wa mwaka 2022.

iv. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya masuala ya jumla yaliyojitokeza katika uchambuzi wa miswada hiyo ya sheria ni pamoja na lugha ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza ili lugha ya Kiswahili iwe lugha rasmi ya uandishi wa sheria. Ili kukidhi masharti hayo baadhi ya miswada ya sheria iliyowasilishwa Bungeni katika kipindi kinachotolewa taarifa hii iliwasilishwa na kusomwa katika hatua zake zote ikiwa imeandikwa kwa lugha hiyo ya Kiswahili. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri huo wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba uandishi wa sheria katika lugha ya Kiswahili pekee unachangamoto mbalimbali moja kati ya changamoto hizo ni uchache wa misamiati na Istilahi za kisheria katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuleta ugumu katika tafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya rejea katika nchi nyingine za Jumuiya ya Madola ili kupata uzoefu wa namna nchi hizo zinavyotumia lugha ya Kingereza na lugha ya asili ya nchi hizo katika uandishi wa miswaada. Katika nchi ya India mathalani Bunge la Juu la India limeweka utaratibu kwa maamuzi ya Bunge kwamba muswada wowote unapowasilishwa Bungeni ni lazima uwe katika makala ya lugha ya kingereza nan akala katika lugha ya kihindi. Mfano huu unaweza kulisaidia Bunge letu na Serikali kwa ujumla kutafakari kwa pamoja ili endapo kutakuwa na ulazima basi marekebisho ya sheria yafanyike ili kuakisi msimamo kuhusu lugha rasmi ya uandishi wa sheria katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inahusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizo za ukaguzi zilifanyika katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha kati ya tarehe 14 mpaka 19 Machi, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa isipokuwa kwa miradi michache ambayo Kamati ilitolea ushauri na mapendekezo mahususi katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka fedha 2021/2022 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023. Mara baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati ilipokea na kujadili utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na masuala mengine Kamati ilibaini kwamba katika utekelezaji wa Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu hadi kufikia Februari, 2022 jumla ya shilingi bilioni moja zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni asilimia 100 ya fedha iliyotengwa. Taarifa za utekelezaji wa mradi zinaonesha kuwa maombi ya vijana yaliyopokewa na kukidhi vigezo hadi Februari, 2022 yalikuwa ni shilingi milioni 205 sawa na asilimia 20.52. Kwa kiasi hicho asilimia 79.5 ya fedha iliyopokelewa imeendelea kubaki bila kupata walengwa waliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu uchambuzi wa taarifa za utekeleza wa majukumu ya Wizara na taasisi zake na sehemu ya kwanza katika hizo inahusu utekelezaji wa Idara ya Mpigachapa Mkuu, Utendaji wa Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali *(Government Printer)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu utendaji wa Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Kamati imebaini kwamba kwa muda mrefu

idara hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zina athiri utendaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa mitambo, uhaba wa watumishi pamoja na kuchelewa na kutofika kabisa kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kamati ilitioa ushauri mahususi kuhusu umuhimu wa Idara hii kuwezeshwa ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba Kamati inaridhishwa na namna ambavyo Serikali imetekeleza maoni na ushauri uliyotolewa na Bunge. Moja kati ya *tour* za msingi zilizochukuliwa na Serikali ni kutoa fedha ili kujenga Kiwanda cha Serikali cha Uchapishaji Jijini Dodoma. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu ili taarifu Kamati kwamba Serikali ina mpango wa kubadilisha Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali kuwa Wakala wa Serikali wa Upiga Chapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Serikali wa kubadilisha Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali na kuwa wakala ni hatua nzuri ambayo kwa maoni ya Kamati utawezesha taasisi hiyo muhimu kuwa na uwezo wa kibajeti na kirasilimali watu ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya pili inahusu mjadala kuhukusu masuala ya kazi na ajira. Kamati inatambua kwamba ajira ni suala mtambuka. Kwa muktadha huu Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu imepewa jukumu mahususi la kuratibu utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya kukuza ajira na kutoa huduma za ajira ili kuongeza nafasi za ajira kwa Watanzania ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kukosekana kwa mifumo yenye usawa na uhalisia katika suala la

mchakato wa baadhi ya ajira Serikalini. Mathalani, suala la kufanya usaili wa maelfu ya waombaji wa ajira kwa nafasi chache za ajira si tu unaleta usumbufu usiyo na lazima kwa Vijana wanao tafuta kazi lakini pia unaweza ukafanya zoezi la kupata watu sahihi kwa kazi husika likawa gumu.

Mheshimwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Kamati ililijadili kwa kina ni umuhimu wa kuwepo na utaratibu wa mgawanyo wa nafasi za ajira Serikalini kwa kuzingatia maeneo ya kijografia mikoa wanakotoka kulingana na wingi wa watu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu muongozo wa utekelezaji, ujumuishwaji na uhimarishaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ili taarifiwa kwamba lengo kuu la mwongozo huu ni kutoa maelekezo kwa wadau kuhusu utekelezaji, ujumuishwaji na uimarishwaji wa usawa, haki, fursa na huduma kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuandaa mwongozo huu kwa sababu utachochea hatua na mikakati madhubuti ya kujumuisha na kuimarisha miundombinu na huduma mbalimbali kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi *(PSSSF);* pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa mfuko huu, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa kuhusu utaratibu wa mafao ya kustaafu kabla au ifikapo tarehe ya kustaafu kwa watumishi wa umma. Moja kati ya changamoto hizo ni uratibu wa taarifa za wastaafu kutokamilika kwa wakati na hivyo kusababisha usumbufu wakati wa kufuatilia mafao yao. Kwa sehemu kubwa changamoto hii inachangiwa na waajiri ambao hawatekelezi wajibu wao kikamilifu wa kuwasilisha

taarifa za watumishi wao kwa wakati, na kuchelewesha au kutowasilisha michango ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania *(Law School of Tanzania);* katika taarifa iliyowasilishwa Kamati imebaini kwamba kiwango cha ufaulu cha wanafunzi wanaopita katika taasisi hiyo ni mdogo tofauti na matarajio ya wengi. Kwa wastani kwa mfano, muhtasari wa matokeo ya mtihani kuanzia kundi la kwanza hadi la 17, kiwango cha juu kabisa cha ufaulu kilikuwa ni asilimia 31.1 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa na mjadala mkubwa katika siku za hivi karibuni. Serikali imeunda vikosi kazi mbalimbali na ripoti zao kuonesha kwamba kuna changamoto mbalimbali na moja ya changamoto hizo ni utofauti wa ufundishaji na uelewa wa sheria katika vyuo vyetu kwa ngazi ya shahada ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita inahusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai. Kwa upande wa uendeshaji wa mashauri ya jinai, taarifa iliyowasilishwa na Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kufikia Disemba 2022, inabainisha mafanikio mbalimbali kuhusu suala la uendeshaji wa mashauri ya jinai katika Mahakama. Pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwemo kuchelewa kwa utekelezaji wa hukumu mbalimbali za Mahakama hususan katika mashauri ambayo yanahusisha utaifishaji wa mali za watuhumiwa pale ambapo Serikali imeshindwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya taarifa yetu inahusu maoni na mapendekezo. Moja ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; ufanisi na utendaji wa Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali:-

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa utendaji wa Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali unakabiliwa na changamoto mbalimbali zinaoathiri ufanisi ikiwemo uhaba wa watumishi, uchakavu wa vitendea kazi,

Na kwa kuwa, Idara hiyo ina umuhimu katika kuchapa na kuchapisha nyaraka mbalimbali za Serikali ambazo kwa muda mrefu, baadhi ya nyaraka hizo zimekuwa zikichapwa au kuchapishwa kwa kampuni binafsi ambako kunaathiri ubora, ulinganifu na usiri,

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kuja na mkakati wa kuiwezesha Ofisi hiyo ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kimiundombinu, kiteknolojia na kimtaji, ili itekeleze majukumu yake kwa ufanizi na kwa viwango vya ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inahusu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. Kuhusu Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu: -

Kwa kuwa, Serikali imefanya juhudi za kuhakikisha kwamba inaandaa Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwahi na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.

Na kwa kuwa, Mwongozo huo ni muhimu katika mipango ya nchi katika mustakabali wa maendeleo ya watu wake.

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) Kuweka mikakati madhubuti na endelevu ya kuhakikisha kwamba, elimu inatolewa kwa taasisi zote za Serikali na umma kwa jumla kuhusu Mwongozo huo,

(ii) Inafanya tafiti na inazingatia upatikanaji taarifa na takwimu muhimu kuhusu watu wenye ulemavu,

(iii) Kila taasisi ya Serikali inahakikisha kwamba, inatekeleza kikamilifu vipengele vya mwongozo huu kulingana na mahitaji yaliyopo,

(iv) Kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika maamuzi mbalimbali yenye kuboresha utekelezaji wa mwongozo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya (b), Mfumo wa Maendeleo wa Vijana:-

Kwa kuwa, hadi kufikia Februari 2022, ni kiasi cha fedha cha shilingi milioni 202 tu sawa na asilimia 25 kati ya shilingi bilioni moja iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 ndicho kilikuwa kimetolewa kwa vijana walioomba na kukidhi vigezo.

Na kwa kuwa, kiasi kikubwa cha fedha iliyobaki ambacho hakijawanufaisha vijana kinaashiria kwamba, vijana wasiokuwa na vigezo ni wengi kuliko walionufaika na mfuko huo.

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) Kutoa elimu ya kutosha kwa vijana nchini ili waweze kunufaika na mfuko huo,

(ii) Kutathmini vigezo vilivyowekwa ili vijana wengi zaidi wanufaike na mradi,

(iii) Kuongeza thamani ya mfuko kwa kuuongezea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (c) ni masuala ya kazi na ajira: -

Kwa kuwa, Kamati inatambua kwamba ukosefu wa ajira hasa kwa vijana ni changamoto ambayo ina athari za kijamii na za kiuchumi.

Na kwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ina wajibu wa kuratibu utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya kukuza ajira na kutoa huduma za ajira ili kuongeza nafasi za ajira kwa watanzania ndani na nje ya nchi.

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) Kuongeza jitihada za kusimamia Sera na Sheria mbalimbali ambazo zinaweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara,

(ii) Kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili viweze kuajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi nchini na vijana wengine kujiajiri wenyewe,

(iii) Kuwe na mpango wa kuhamasisha vijana nchini kujifunza stadi za kazi za kimkakati na baadaye kuwaunganisha vijana hao na fursa za kazi zenye staha nje ya nchi kulingana na ushindani wa soko la ajira la kimataifa katika sekta za mbalimbali kwa kushirikiana na balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu Mfuko wa Hifadhi wa Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba kuna changamoto kwa baadhi ya wastaafu wa utumishi wa umma kupata stahiki zao kwa ukamilifu na kwa wakati, kitu ambacho kinasababisha usumbufu na kadhia kwa wastaafu hao.

Na kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba, changamoto hiyo inaweza kusababishwa na baadhi ya Waajiri ambao wamechelewa kuwasilisha taarifa muhimu za wastaafu hao kwa ukamilifu na kwa wakati.

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) *PSSSF* ifuatilie michango na kuhakikisha kwamba, inalipwa kikamilifu,

(ii) Ichukue hatua kali za kisheria na kinidhamu kwa mwajiri ambaye hajawasilisha michango kwa wakati na kwa ukamilifu,

(iii) Itoe elimu ya mara kwa mara kwa wanachama kuhusu umhimu wa kufuatilia kupata taarifa binafsi za michango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu Wizara ya Katiba na Sheria. Sehemu ya Nne (a) ni lugha ya uandishi wa Sheria: -

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba, Serikali imeanza utaratibu wa kuwasilisha Bungeni Miswada kwa lugha ya Kiswahili pekee,

Na kwa kuwa, matumizi ya Lugha ya Kiswahili pekee katika uandishi wa Sheria yanaweza kuleta changamoto ya tafsiri na utekelezaji wa sheria husika,

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali ione uwezekano wa kufanya marekebisho tena ili sasa miswada ya sheria iwasilishwe Bungeni kwa lugha zote mbili, yaani Kingereza na Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya (c) ni uendeshaji wa mashauri ya jinai: -

Kwa kuwa, nchi yetu ya Tanzania inaheshimu misingi ya utawala wa sheria ambayo ni nguzo muhimu ya kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

Na kwa kuwa, suala la uendeshaji wa mashauri ya jinai, unahusisha haki za mtuhumiwa kwa upande mmoja na wajibu wa mwendesha mashtaka kwa upande mwingine.

Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha kwamba, inatekeleza maamuzi yote ya Mahakama ili kulinda haki za raia, ikiwemo kurejesha mali zilizotaifishwa iwapo mtuhumiwa ameshinda kesi na pale ambapo hatua zote za rufaa zimekamilika,

(ii) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika katika upelelezi, ukamataji na utaifishaji wa mali za watuhumiwa, kulinda haki za watuhumiwa hao na mali zao bila kuathiri thamani ya mali zao endapo watuhumiwa hao watashinda kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (c) inahusu mafunzo ya sheria kwa vitendo na ufaulu wa wanafunzi.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko kuhusu kiwango cha ufaulu katika Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo.

Na kwa kuwa, malalamiko hayo yamesabisha kuwepo kwa madai kuhusu uwezo mdogo wa wanafunzi wanaodahiliwa kwa upande mmoja, lakini pia ugumu wa mfumo wa mafunzo ambao unasababisha wanafunzi kufeli kwa upande mwingine;

Hivyo basi, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kufikiria na ikibidi kuamua kuanzisha mitihani ya kuingia *(entry examinations),* ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaojiunga na taasisi hiyo wana ujuzi wa nadharia unaotosheleza kufanya mafunzo kwa vitendo kwa ufanisi,

(ii) Mamlaka husika kufanya utafiti wa kutosha kuhusu mitaala na uwezo wa vyuo katika kufundisha taaluma ya sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa ushirikiano mkubwa aliotupa Kamti yetu ya Katiba na Sheria wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yetu. Kamati inamuahidi kumpa ushirikiano na inamuaombea kila la kheri katika utekelezaji bora wa majukumu yake. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Kwa heshima

kubwa naomba majina yao yaingine katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, ninawashukuru viongozi wote wa Serikali kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake. Kwa heshima kabisa, naomba kuwatambua kama ifuatavyo: -

i. Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),

ii. Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu),

iii. Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo(Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano),

iv. Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria,

v. Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

vi. Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu),

vii. Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),

viii. Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira),

ix. Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niwashukuru watendaji wote wa Mhimili wa Utendaji na Mhimili wa Mahakama kwa ushirikiano walioipatia Kamati. Kwa niaba yao wote naomba niwatambue viongozi wao kama ifuatavyo: -

i. Dkt. John Anthony Jingu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

ii. Prof. Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

iii. Ndg. Mary Ngelela Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

iv. Ndg. Mary Gabriel Makondo, Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria.

v. Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndgugu Nenelwa Mwihambi, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naliomba sasa Bunge lako liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**8 FEBRUARI, 2023**

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARU, 2022 HADI JANUARI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Taarifa hii inahusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambapo pamoja na masuala mengine, inaelezea kwa muhtasari kuhusu muundo na majukumu ya Kamati, pamoja na kuainisha mbinu zilizotumika kutekekeleza majukumu hayo.
b) Sehemu ya Pili inabainisha majukumu/shughuli zilizotekelezwa na kutoa ufafanuzi wa uchambuzi kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika.
c) Sehemu ya Tatu ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na
d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

### 1.2 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Katiba na Sheria ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo imeundwa chini ya Kifungu cha 5 (b) cha Nyongeza ya Nane

ya Kanuni za Kudumu za Bunge.[1] Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni, Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zifuatazo: -

a) Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)
b) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)
c) Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); na
d) Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa Kamati nyingine za kisekta, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria imekabidhiwa majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### 1.3 Njia na Mbinu Zilizotumika Kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Katiba na Sheria hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Majukumu hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya

[1] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

Muungano na vyombo vyake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ikisomwa pamoja na Ibara ya 63 (3).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 136 (3) na (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kutumia mbinu na njia zifuatazo: -

a) Kufanya vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za wizara na taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wa majukumu, mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo;

b) Kuchambua na kujadili miswada ya sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu miswada hiyo;

c) Kufanya ziara za mafunzo katika taasisi na maeneo mbalimbali ya kisekta kwa lengo la kuona na kujifunza namna ambavyo taasisi hizo zinatekeleza majukumu yake;

d) Kutembela na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kujiridhisha kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji na ufanisi wa miradi hiyo; na

e) Kupokea semina na mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujenga uelewa wa masuala mahsusi yanayotekelezwa na Wizara na taasisi zake, pamoja na wadau wengine.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MASUALA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inalipa Bunge madaraka ya kutunga sheria. Aidha, Ibara ya 97 inaweka utaratibu kwamba, Bunge litatumia madaraka hayo kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria kabla ya kibali cha Rais ili kuwa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo na kwa kuzingatia Kanuni ya 97, katika kipindi cha mwaka mmoja kati ya Februari 2022 na Januari 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilijadili Miswada ya Sheria minne (4). Miswada hiyo ni: -

a) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.7 wa Mwaka 2021** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Act, 2021]* ambao ulifanya marekebisho katika sheria zifuatazo:-

   i) Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Sura ya 209 *[The College of Wildlife Management Act, (CAP. 209)]*

   ii) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura ya 218 *[The Copyright and Neighbouring Rights Act, (CAP 218)]*

   iii) *Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200 [The Economic and Organised Crimes Control Act, (CAP. 200)]*

iv) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka *[(The National Prosecutions Service Act, (CAP. 430)]*

v) Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49 *[(The National Sports Council of Tanzania Act, (CAP. 49)]*

vi) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 *[(The Penal Code, (CAP. 16)]*

vii) Sheria ya Upatikanaji wa Huduma ya Mawasiliano kwa Wote, Sura ya 422 *[(The Universal Communications Services Access Act, (CAP. 422)]*.

viii) Sheria ya Veterinari, Sura ya 319 *[(The Veterinary Act, (CAP. 319)]*.

b) **Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022** ambao pamoja na masuala mengine, ulikuwa unaanzisha Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Maafa kwa lengo la kujiandaa kukabili majanga, kuchukua hatua za kupunguza madhara ya majanga, pamoja na kurejesha jamii katika hali ya awali au bora zaidi baada ya maafa. Aidha, Muswada huu ulikuwa na lengo la kuifuta Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura ya 242 iliyokuwa inatumika tangu Mwaka 2015 kutokana na kubainika kuwepo na changamoto za utekelezaji wa Sheria hiyo.

c) **Muswada wa Sheria ya ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2022** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2022]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 *(The Anti–Trafficking in Person Act, Cap. 432)*

ii) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 *(The Drug Control and Enforcement Act, Cap 95)*

iii) Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 *(The Public Leadership Code of Ethics Act, Cap 398)*; na

d) **Muswada wa Sheria ya ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2022** *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2022]* ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

i) Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333 *(The Antiquities Act, Cap. 333)*

ii) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 *(The Banking and Financial Institutions Act, Cap. 342)*

iii) Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 *(The Capital Markets and Securities Act, Cap. 79)*

iv) Sheria ya Madini, Sura ya 123 *(The Mining Act, Cap. 123)*

v) Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281 *(The National Museum of Tanzania Act, Cap. 281)*

vi) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 *(The Public Finance Act, Cap. 348)* ; na

vii) Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 *(The Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226)*

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya kina kuhusu uchambuzi wa maudhui ya Miswada hiyo ya sheria yanapatikana katika taarifa husika zilizowasilishwa Bungeni. Hata hivyo, kuna masuala ya jumla ambayo ni muhimu Kamati ikayatolea ufafanuzi kama ilivyobainika katika uchambuzi. Masuala hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo: -

a) **Lugha ya Uandishi wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuwasilisha Miswada ya Sheria Bungeni kwa Lugha ya Kiswahili. Katika kuzingatia ushauri huo, Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ili lugha ya Kiswahili iwe lugha rasmi ya uandishi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Miswada ya Sheria iliyowasilishwa Bungeni katika kipindi kinachotolewa Taarifa hii, iliwasilishwa na kusomwa katika Hatua zake zote ikiwa imeandikwa kwa Lugha ya hiyo. Kamati inapongeza Serikali kwa utekelezaji wa ushauri wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi uliofanywa hivi karibuni, Kamati imebaini kwamba uandishi wa sheria katika Lugha ya Kiswahili peke yake una changamoto mbalimbali. Moja kati ya changamoto hizo ni uchache wa misamiati na istilahi za kisheria katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuleta ugumu katika tafsiri. Aidha, Sheria zilizoandikwa kwa Kiswahili peke yake zinaweza kuleta changamoto kwa Mahakama katika kufikia maamuzi hasa kwa kuzingatia kwamba Mfumo wa Sheria wa nchi yetu unafuata misingi ya Jumuiya ya Madola.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuathiri nia njema ya Serikali katika kutekeleza maoni ya Bunge kuhusu lugha ya uandishi wa sheria kuwa Kiswahili, Kamati imetafakari uwezekano wa kufanyika marekebisho tena ili sasa Miswada ya Sheria iwasilishwe Bungeni kwa lugha zote mbili, yaani Kiingereza na Kiswahili. Lengo la mapendekezo haya, ni kuwapa Wabunge wigo mpana wa kuelewa kwa kina masharti na mapendekezo ya Miswada husika.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imefanya rejea katika nchi nyingine za Jumuiya ya Madola ili kupata uzoefu wa namna nchi hizo zinavyotumia lugha ya Kiingereza na lugha za asili ya nchi hizo katika Uandishi wa Miswada. Katika nchi ya India mathalani, Bunge la Juu la India (Rajya Sabha) limeweka utaratibu kwa Maamuzi ya Bunge *(Ruling)* kwamba, Muswada wowote unapowasilishwa Bungeni ni lazima uwe katika nakala ya Lugha ya Kiingereza na nakala katika Lugha ya Kihindi.[2] Msimamo huu unaweza kulisaidia Bunge letu na Serikali kwa ujumla kutafakari kwa pamoja ili endapo kutakuwa na ulazima, basi marekebisho ya Sheria yafanyike ili kuakisi msimamo kuhusu lugha rasmi ya uandishi wa sheria za nchi yetu.

b) **Ushiriki wa Wadau katika Mchakato wa Kutunga Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge imekuwa ikishirikisha wadau mbalimbali katika hatua ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria. Hata hivyo, kumekuwepo na madai kutoka kwa baadhi ya wadau kwamba, ushirikishwaji wao katika mchakato wa kuandaa mapendekezo ya Muswada kabla ya kuwasilishwa Bungeni umekuwa hauridhishi.

---

[2] Kitabu kilichoandikwa na Sekretarieti ya Bunge la Juu la India (Rajya Sabha) kuhusu Uendeshaji wa Bunge (Rajya Sabha at Work), Sehemu ya 21 inazungumzia kuhusu Mchakato wa Kutunga Sheria (Legislation).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kuthamini mchango wa wadau mbalimbali, nje na ndani ya Serikali katika uchambuzi wa Miswada unaofanywa na Kamati za Bunge. Hata hivyo, kwa maoni ya Kamati, kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali, kabla ya kuwasilisha muswada wowote Bungeni Kusomwa Mara ya Kwanza, mapendekezo ya Muswada huo yakajumuisha maoni ya wadau wengi kadri iwekezekanavyo. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaboresha maudhui ya Muswada, na pia Bunge litatumia muda mfupi kuchambua na kujadili Muswada husika bila kufanya marekebisho makubwa iwapo hakutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo.

## 2.2 Uchambuzi wa Mikataba ya Kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Mikataba ya Kimataifa ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ya kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa kwa mujibu Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Katika kipindi kinachotolewa Taarifa hii, Kamati ya Katiba na Sheria kwa niaba ya Bunge na kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ilichambua na kutoa maoni yake kuhusu **Itifaki ya Kuongeza Mamlaka ya Mahakama ya Haki ya Afrika Masharik**i *(The Protocol to Operationalise the Extended Jurisdiction of the East African Court of Justice)* ili Bunge liweze kujadili na kuridhia Itifaki hiyo kwa Azimio la Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, pamoja na kwamba Itifaki hiyo ilikubaliwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu Februari, 2015, nchi yetu ilikuwa bado haijaridhia Itifaki hiyo. Kuchelewa kuridhia itifaki hiyo kuliathiri lengo la Jumuiya kuiwezesha Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (*The East African Court of Justice)*

kushughulikia masuala ya migogoro ya kibiashara, uwekezaji na sarafu ya pamoja, pale inapotokea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuridhia Itifaki hiyo, Bunge limetekeleza wajibu wake ambao una faida zifuatazo: -

a) Kuwezesha Nchi Wanachama kuwa na mamlaka moja yenye tafsiri moja kisheria katika Itifaki pale inapotokea utata katika tafsiri ya vipengele vya Itifaki katika migogoro ya kibiashara, uwekezaji na sarafu ya pamoja; na

b) Kuimairisha mahusiano ya kibiashara na uwekezaji kwa Nchi Wanachama ambazo zimeridhia Itifaki hii.

c) Kuwawezesha wafanyabiashara kufungua kesi za kibiashara

2.3 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika ili Kamati iwe katika nafasi nzuri zaidi ya kuzishauri Wizara inazozisimamia katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, ziara hizo za ukaguzi zilifanyika katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha kati ya tarehe 14 – 19 Machi, 2022 ambapo miradi ifuatayo ilitembelewa: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kuhifadhia Kumbukumbu za Mahakama, Tanga (Mradi Na. 6327)

b) Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Wavulana katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA), Lushoto (Mradi Na. 6311)

c) Mradi wa Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Same (Mradi Na. 6312)

d) Mradi wa Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mwanga (Mradi Na. 6312)

e) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi (Mradi Na. 6314)

f) Mradi wa Ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Kutoa Haki (IJC) Arusha (Mradi Na. 6389)

g) Mradi wa Ujenzi wa Vitalu Nyumba *(Greenhouses*) Arusha katika Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini (Mradi Na. 6581)

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika katika ziara za ukaguzi wa miradi hiyo, yanapatikana katika Taarifa za Kamati zenye maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa kila Wizara husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa isipokuwa kwa miradi michache ambayo Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo mahsusi katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masuala ambayo yalibainika katika baadhi ya taasisi ni kutokuwa na utamaduni wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati mdogo wa mara kwa mara *(regular maintenance)* wa miradi ya ujenzi. Kwa sababu hiyo, miradi hiyo ambayo inatumia fedha nyingi za umma, huanza kupoteza ubora wake na kuchakaa katika muda mfupi.

2.4 **Uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge katika Mchakato wa Bajeti *(the budget cycle)* kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kikamilifu masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge kwa kufanya ulinganisho baina ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Aidha, Kamati iliangalia mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kupima ufanisi wa utekekelezaji wa bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge hili kupata picha ya masuala yaliyobainika katika uchambuzi wa Bajeti ya Serikali

2022/2023, ufuatao ni muhtasari wenye kuonyesha mwenendo wa Bajeti ya Wizara/Taasisi zinazosimamiwa na Kamati: -

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

a) Katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake, Kamati ilibaini yafuatayo: -

i) Kwa ujumla wake, hali ya upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa ya kuridhisha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hadi wakati taarifa ya Kamati inawasilishwa Bungeni, Ofisi hiyo na Taasisi zake zilipokea wastani wa **asilimia 84.15** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliongezeka kwa **asilimia 14.66** ukilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022. Moja kati ya sababu ya ongezeko hilo ilikuwa ni utekelezaji wa maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi.

iii) Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bajeti ya Ofisi hiyo ilipungua kwa **asilimia 4.2** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati ilibaini kwamba upungufu huo ulitokana baadhi ya miradi kutotengewa fedha kwa kuwa ilikuwa katika hatua za mwisho, na baadhi ya miradi mingine ilitengewa fedha pungufu.

iv) Katika utekelezaji wa **Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana** ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), hadi kufikia Februari 2022, jumla ya

**Sh. 1,000,000,000** zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni asilimia mia moja (100%) ya fedha iliyotengwa. Taarifa za utekelezaji wa mradi zinaonyesha kuwa, maombi ya vijana yaliyopokewa na kukidhi vigezo hadi Februari 2022 yalikuwa ni **Sh. 205,000,000** sawa na **asilimia 20.5**. Kwa kiasi hicho, **asilimia 79.5** ya fedha iliyopokewa imeendelea kubaki bila kupata walengwa waliokusudiwa. Kamati ilitoa maoni mahsusi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa elimu ya kutosha kuhusu mfuko wa maendeleo ya vijana na pia kutathmini vigezo vilivyowekwa ili vijana wengi zaidi wanufaike na mradi huo.

v) Kamati ilibaini kwamba ni **asilimia 42.23** tu ya fedha za nje na **asilimia 59.38** ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Ofisi ya Waziri Mkuu ndizo zilipatikana. Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatoa Fedha za Maendeleo kwa wakati na kuweka mikakati ya kubajeti *(budgeting)* kwa kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi ya maendeleo ili kupunguza utegemezi wa fedha za nje.

**<u>OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)</u>**

b) Katika bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Kamati ilibaini yafuatayo: -

i) Katika Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 bajeti iliongezeka kwa **asilimia 29.35** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko hili ni matokeo ya ushauri uliotolewa na Kamati ili kuwezesha Ofisi hiyo na taasisi zake ziwe na fedha ya kutosha kutekeleza majukumu yake.

ii) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilibaini kwamba fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni pungufu kwa **asilimia 27.32** ukilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Vilevile Kamati ilibaini kwamba kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kilitokana na Fedha za Ndani kwa asilimia mia moja (100%) kama ambavyo ilikuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Pamoja na kwamba kiasi cha bajeti ya maendeleo kilipungua, Kamati iliipongeza Ofisi hiyo kwa kuendelea kutenga fedha za utekelezaji wa miradi yake kwa kutumia Fedha za Ndani. Hatua hii ni sehemu muhimu ya kuchochea juhudi kwa Serikali nzima kukusanya mapato ya ndani ili kujitosheleza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

c) Kwa upande wa Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

d)

i) Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliongezeka kwa wastani wa **asilimia 41.91** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko hili liliakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake.

ii) Hata hivyo, kwa upande wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ongezeko la makisio ya makusanyo hayo lilikuwa **asilimia 3.55** ukilinganisha na Makadirio

ya Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati ilikuwa na maoni kwamba, wastani wa ongezeko hili ni mdogo hasa kwa kuzingatia kwamba kufikia Februari, 2022 baadhi ya taasisi zilikusanya maduhuli zaidi ya makisio yaliyowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu Uchambuzi wa Bajeti za kila Wizara husika, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa kwa nyakati tofauti katika Mkutano wa Saba wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2022.

2.5 **Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake**

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Msingi wa shughuli hii umejengwa katika utekelezaji wa Madaraka ya Bunge kama chombo kikuu kwa niaba ya wananchi cha kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muhtasari naomba nitoe maelezo kuhusu taarifa na masuala mbalimbali yaliyojadiliwa na Kamati kama ifuatavyo: -

2.5.1 **Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Wizara zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika Vikao vya Kamati za Bunge vilivyofanyika kuanzia tarehe 16 – 27 Januari, 2023, Kamati ilipokea Taarifa za Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Maazimio hayo yalitokana na Taarifa ya Mwaka ya

Kamati ya Februari, 2021 hadi Januari, 2022 iliyowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sehemu kubwa, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maazimio ya Bunge uliofanywa na Wizara na taasisi hizo. Kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo zaidi katika utekelezaji wake, Kamati imetoa ushauri mahsusi kwa kila Wizara na taasisi zake ili yakafanyiwe kazi zaidi.

**OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU)**

2.5.2 **Maendeleo ya Ujenzi wa Mji wa Serikali na Mpango wa Serikali Kuhamia Makao Makuu ya Nchi, Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kuhusu namna Ofisi hiyo inavyoratibu Mpango wa Serikali Kuhamia Makao Makuu ya Nchi, Dodoma. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilielezwa maendeleo ya ujenzi wa Mji wa Serikali na baadaye kutembelea eneo la mradi huo ili kujionea hali halisi ya ujenzi wa baadhi ya majengo, na miundombinu muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa iliyowasilishwa, Kamati imebaini kwamba usanifu pamoja na ujenzi wa ofisi na miundombinu katika Mji wa Serikali umezingatia masuala muhimu ikiwemo jiolojia ya eneo la Mtumba, dhana ya kuwa na Mji wa Kijani *(Green City*) na matumizi ya nishati mbadala *(Renewable Energy Sustainability)*. Aidha, ujenzi wa Mji wa Serikali unahusisha ujenzi wa miundombinu mingine ya kudumu inayojengwa juu na chini ya ardhi ikiwemo barabara, maji safi, maji taka, umeme, gesi, mawasiliano, TEHAMA, usalama, zimamoto na uokoaji pamoja na programu za Upandaji miti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huu

mkubwa na muhimu, na pia inazipongeza Taasisi zote ambazo tayari wameshaanza kuhamia katika majengo yaliyopo.

**Mheshimiwa Spika**¸ kwa upande mwingine, Kamati imebaini kwamba Serikali ina mpango wa kufanya upanuzi wa eneo la mji huo ambapo hadi wakati Taarifa yake inawasilishwa mbele ya Kamati, Serikali ilikuwa inakamilisha taratibu za kutwaa eneo la Hekta 2,030.88 lililopo kati ya Mji wa Serikali na Ikulu ya Chamwino. Kamati ilitaarifiwa kwamba, upatikanaji wa eneo hili ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma (2019-2039). Eneo hilo litatumika kwa ajili ya uendelezaji wa Mji wa Serikali ikiwemo ujenzi wa nyumba za makazi ya Viongozi, Ofisi za Taasisi na huduma mbalimbali za kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, katika mjadala baina ya Wajumbe wa Kamati kuhusu suala la upanuzi wa Mradi wa Mji wa Serikali, ipo hoja iliibuka kuhusu namna ambavyo Serikali inapanga kutwaa eneo hilo katika hatua ambayo tayari Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi. Kwa uchambuzi uliofanyika, hatua ya kutwaa eneo hilo ilipaswa kufanyika mapema kabla ya Mpango Kabambe kuwekwa. Kwa muktadha huo, ni vyema Serikali ikajizatiti katika kuweko mipango thabiti na endelevu ili kuepuka gharama. Kupanga ni kuchagua.

### 2.5.3 Utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali *(Government Printer)*

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali. Kamati imebaini kwamba, kwa muda mrefu Idara hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utendaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa mitambo, uhaba wa watumishi, pamoja na kuchelewa au kutofika kabisa kwa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilitoa ushauri mahsusi kuhusu umuhimu wa Idara hii kuwezeshwa ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, Kamati imeridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Bunge. Moja kati ya hatua za msingi zilizochukuliwa na Serikali, kutoa fedha ili kujenga Kiwanda cha Serikali cha Uchapishaji jijini Dodoma. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu iliitaarifu Kamati kwamba Serikali ina mpango wa kubadilisha Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali kuwa Wakala wa Serikali wa Upigaji Chapa.

**Mheshimiwa Spika**, mpango wa Serikali kubadilisha Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali kuwa Wakala, ni hatua nzuri ambayo kwa maoni ya Kamati, utawezesha Taasisi hiyo muhimu kuwa na uwezo kibajeti na kirasilimali watu ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hata hivyo, ni muhimu kwa Serikali kufanya utafiti wa kutosha na kushirikisha wadau wote muhimu ili kubaini umuhimu wa kuanzishwa kwa Wakala huo na kuainisha umahsusi wa majukumu yake.

2.5.4 **Utekelezaji wa Majukumu na Vipaumbele vya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC)**

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) liliundwa kwa mujibu wa wa Waraka wa Rais Na. 1 wa Mwaka 2001 ili kutekeleza majukumu mbalimbali kwa lengo la kuratibu ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Moja kati ya majukumu ya Baraza hilo ni kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera za kibiashara, kiuchumi na kijamii. Katika Taarifa iliyowasilishwa, Kamati ilijifunza masuala mbalimbali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Baraza hilo pamoja na mafanikio na changamoto za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji wenye mafanikio wa Baraza hili, Kamati ilibaini kwamba kuna kasi ndogo ya utekelezaji wa maazimio ya Vikao na Mikutano ya Baraza hili. Aidha, kumekuwepo na ufanisi usioridhisha wa Mikutano ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa (RBCs) na ile ya Mabaraza ya Biashara ya Wilaya (DBCs). Changamoto hii inadhoofisha majadiliano na maazimio kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi hizo. Changamoto hii pia inachangiwa na idadi ndogo ya Watumishi wenye utaalamu na uzoefu kwa ajili ya kuendesha majadiliano ambao pia wanaweza kufanya uchambuzi wa mazingira ya biashara ili kushauri ipasavyo.

2.5.5 **Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyowasilishwa ilikusudia kuwapa Wajumbe uelewa wa kina kuhusu namna Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inavyotekeleza majukumu yake msisitizo ukiwa katika mafanikio na changamoto. Majukumu ya Tume yamefafanuliwa bayana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 lakini pia katika Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 pamoja na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ina wajibu wa kuratibu na kusimamia uendeshaji wa chaguzi kwa kuzingatia sheria kwa manufaa ya wananchi, vyama vya siasa na wagombea ili kuimarisha demokrasia nchini. Kamati imebaini kwamba, kwa sehemu kubwa, Tume ya Taifa ya uchaguzi inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, pamoja na kuwepo kwa changamoto kadhaa. Changamoto kubwa ni uchache wa watumishi ukilinganisha na mahitaji halisi ya Tume hiyo.

**OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)**

2.5.6 **Mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulianzishwa na Serikali mnamo mwaka 1993 chini ya Sheria ya *Fedha (The Exchequer and Audit Ordinance, cap 439)* namba 21 ya mwaka 1961. Kamati ilitaarifiwa kwamba, moja ya malengo ya Mfuko huo ni kuwawezesha vijana nchini (Tanzania Bara) wenye umri kati ya Miaka 15 hadi 35 kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha au kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali. Aidha, Mfuko una malengo ya kuwasaidia vijana kujenga tabia ya kuweka akiba, kukopa kwa busara na kurejesha kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali imeandaa Mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Toleo la Mwaka 2022 kwa lengo la kutatua changamoto za kiutekelezaji zilizokuwepo katika Mwongozo wa awali wa Mwaka 2013, lakini pia kutekeleza maelekezo ya viongozi na maoni ya wadau husika.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya maeneo ambayo yameboreshwa katika Mwongozo mpya, ni kuruhusu kijana mmoja mmoja kukopa badala ya vikundi peke yake. Aidha, Mwongozo mpya unaongeza wigo wa wachangiaji wa Mfuko kutoka bajeti ya Serikali kuu na kuruhusu wadau wengine kuchangia. Vilevile Mwongozo unaweka mfumo madhubuti kwa ajili ya tathmini na ufuatiliaji wa Mfuko na kuweka mfumo wa uwajibikaji kwa vijana pamoja na wasimamizi wa Mfuko katika ngazi zote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kusikiliza maoni ya Wabunge kuhusu namna bora za kuweka mifumo ya kitaasisi ambayo itachangia juhudi za

kuwasaidia vijana wa nchi hii kujikwamua kiuchumi kwa mustakabali mpana wa maendeleo ya nchi yetu.

### 2.5.7 Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali iliandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 ili kuendana na mabadiliko mbalimbali yaliyojitokeza ambayo hayakuzingatiwa ipasavyo katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 1996. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2007 ina lengo kuu la kuwajengea uwezo vijana, kuwawezesha na kuwaongoza vijana na wadau wengine katika utekelezaji wa masuala ya maendeleo ya vijana.

**Mheshimiwa Spika**, malengo mahususi ya Sera hii ni pamoja na kuwawezesha vijana kupata ujuzi na uzoefu wa ajira; kuwawezesha vijana kukubali majukumu ili kuweza kuwa na mwenendo na maadili mema; kujenga mazingira yanayofaa kwa ajili ya kushiriki katika kutoa maamuzi; na kuongeza kasi ya kuanzisha na kutumia huduma za jamii ambazo ni rafiki kwa vijana.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana imetekelezwa kwa takribani kipindi cha miaka 16 hadi sasa ambapo katika kipindi hicho cha utekelezaji kumekuwepo na mafanikio mbalimbali yaliyopatikana. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto mbalimbali. Moja kati ya changamoto hizo ni Sera hiyo kutokuwa na Mkakati wa Utekelezaji suala ambalo limesababisha kutokuwepo kwa ufanisi katika uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo imesababisha wadau wengi wakiwemo vijana kutoifahamu Sera husika na kutotambua majukumu yao ya utekelezaji wa Programu na Afua za Maendeleo ya Vijana zinazopaswa kutekelezwa na Taasisi

hizo. Aidha, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ililenga kuzuia mmomonyoko wa maadili unaotokana na utandawazi lakini haikueleza bayana kuhusu fursa za matumizi ya TEHAMA kwa vijana ikiwemo uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi kwa vijana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali iko katika mchakato wa mapitio ya Sera hiyo kwa lengo la kuiboresha ili iendane na mazingira ya sasa.

2.5.8 **Mjadala Kuhusu Masuala ya Kazi na Ajira**

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao mbalimbali vilivyofanyika baina ya Kamati na Serikali, suala la kazi pamoja na ajira hususan kwa vijana, limekuwa likitawala majadiliano. Msingi wa majadiliano hayo, unatokana na nia thabiti ya Wajumbe kuona kwamba, masuala ya kazi na ajira yanapewa kipaumbele inavyostahili ili Serikali iwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, Watanzania na hasa vijana wananufaika na mikakati ya kuongeza fursa za ajira na kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba ajira ni suala mtambuka. Kwa muktadha huo, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) imepewa jukumu mahsusi la kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya kukuza ajira na kutoa huduma za ajira ili kuongeza nafasi za ajira kwa watanzania ndani na nje ya nchi. Kamati inapongeza juhudi mbalimbali zinazofanywa na Ofisi hii ikiwemo:-

a) Kutoa mafunzo kwa vijana ya kushindania fursa za ajira, ushauri nasaha, na kuwaunganisha na fursa za ajira pamoja na mafunzo tarajali

b) Kuandaliwa kwa Ripoti ya Uchambuzi wa Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (Nguvukazi) na kutoa Viashiria muhimu vya Soko la Ajira; na

c) Kuandaliwa kwa mfumo wa kielektroniki wa taarifa za soko la ajira kwa ajili ya kukusanya na kutoa taarifa za soko la ajira nchini ikiwa ni pamoja na kusajili wahitimu na watafuta kazi nchini.

Hatahivyo, pamoja na jitihada hizo za Serikali, Kamati imebaini kwamba, suala la ajira, hususan kwa vijana ni changamoto kubwa kwa Taifa na hasa kwa kuzingatia kwamba, kundi la vijana ni zaidi ya asilimia 57 ya watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi *(Integrated Labour Force Survey)* wa Mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kukosekana kwa mifumo yenye usawa na uhalisia katika suala la mchakato wa baadhi ya ajira serikalini. Mathalani, suala la kufanya usaili wa maelfu ya waombaji wa ajira kwa nafasi chache tu za ajira, sio tu unaleta usumbufu usio wa lazima kwa vijana wanaotafuta kazi, lakini pia unaweza ukafanya zoezi la kupata watu sahihi kwa kazi husika likawa gumu.

**Mheshimiwa Spika**, jambo lingine ambalo Kamati ilijadili kwa kina, ni umuhimu wa kuwepo na utaratibu wa mgawanyo wa nafasi za ajira Serikalini kwa kuzingatia maeneo ya kijiografia (mikoa wanayotoka) kulingana na wingi wa watu wa maeneo hayo *(population density)*. Msingi wa hoja hii unatokana na ukweli kwamba, nchi yetu imejengwa katika misingi ya kuthamini umoja wa kitaifa, bila kujali tofauti za makabila, dini, wala mikoa tunayotoka. Mathalani, Wajumbe walitafakari kwamba, iwapo taasisi inahitaji kuajiri wafanyakazi 40, basi kwa kadri itakavyowezekana, na bila kuathiri taratibu za kiutumishi, walau kila mkoa uwakilishwe na Mtanzania mmoja.

2.5.9 **Utendaji wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inatekeleza jukumu la utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya usuluhishi

na uamuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Kanuni zake. Utekelezaji wa jukumu hilo unalenga kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu sehemu za kazi na hivyo kuleta tija na mazingira rafiki ya uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa iliyowasilishwa kwa Kamati, Tume ilieleza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika kusuluhisha migogoro ya kikazi iliyosajiliwa kwenye Tume. Mafanikio hayo ni pamoja na kutatua asilimia 79 ya migogoro ya kikazi iliyosajiliwa katika hatua ya usuluhishi, na kuamua asilimia 74.7 ya migogoro ya kikazi iliyosajiliwa katika hatua ya uamuzi kufikia Februari, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Tume hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kuendesha mashauri kwa ufanisi zaidi kutokana na kukosekana kwa mfumo wa kielektroniki wa uendeshaji mashauri na utunzaji kumbukumbu katika baadhi ya ofisi zake. Hadi wakati taarifa inawasilishwa katika Kamati, Tume ilikuwa imefanikiwa kusimika na kutumia mfumo wa kielektroniki wa uendeshaji mashauri na utunzaji kumbukumbu katika ofisi 10 za Tume kati ya 32.

### 2.5.10 **Usalama na Afya Mahali Pa Kazi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti, Kamati ilipokea taarifa kutoka kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA) kwa lengo la kupata uelewa wa jumla kuhusu majukumu ya Wakala huo, pamoja na masuala mahsusi ya utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** OSHA ilianzishwa mnamo tarehe 31 Agosti, 2001 chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 ili kiwe chombo mahsusi cha Serikali kitakachosimamia Usalama na Afya mahali pa kazi Tanzania Bara. OSHA inawajibika kuhakikisha kunakuwepo na sera na

mikakati endelevu ambayo itawezesha wafanyakazi kufanya kazi katika mazingira salama kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuzuia ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na mazingira ya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imeridhishwa na Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya OSHA na hasa suala zima la kusimamia matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya ya Mwaka 2003.

**Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine Kamati ilitaarifiwa kwamba, Katika Mkutano wa 110 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) uliofanyika Geneva, Uswisi kuanzia tarehe 27 Mei, 2022 hadi tarehe 11 Juni 2022, Nchi Wanachama waliazimia kwa pamoja kujumuisha masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika Miongozo ya ILO kuwa suala la msingi wa haki katika maeneo ya kazi. Aidha, tarehe 11 November 2022 kikao cha kamati ya kazi na ajira cha Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC) kilichofanyika Johanesburg, Afrika Kusini kiliridhia kuunga mkono kauli hiyo na kushauri nchi wanachama kuridhia Mikataba husika ya ILO. Kwa muktadha huo, masuala ya Usalama na Afya mahala pa kazi yanapaswa kuwa ni Haki ya msingi mahali pa kazi na sio wajibu wa kisheria pekee.

> "*Safe and healthy working environment is among the fundamental principles and rights at work*".

**Mheshimiwa Spika**, kwa hatua hii, Tanzania kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa katika kusimamia masuala ya haki za msingi za watu, inapaswa kuongeza juhudi za kuhakisha kwamba haki hizo za wafanyakazi nchini zinalindwa kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inapongeza hatua ambazo OSHA inachukua katika kuelimisha waaajiri kuhusu masuala ya usalama mahali pa kazi. Kipekee kabisa, Kamati

inapongeza hatua ya Wakala huo kutoa mafunzo maalum ya usalama na afya mahali pa kazi kwa watu wasioona, kwa kutumia kitabu maalum chenye maandishi ya nukta nundu.

2.5.11 **Utekelezaji wa Majukumu ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263. Mfuko huu ulianzishwa na Serikali ili kutimiza matakwa ya Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003. Mfuko huu pia ulianzishwa ili kuondokana na mapungufu yaliyokuwepo katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya 1949 ambayo ilifutwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, mfuko huu una majukumu mbalimbali ambayo yanajumuisha suala la kuhamasisha uzuiaji wa majanga, kutoa huduma mbalimbali na kulipa fidia. Fidia zinazotolewa na mfuko huu zinajumuisha huduma ya matibabu, malipo ya ulemavu wa muda mrefu na kudumu, pamoja na malipo kwa wategemezi endapo mfanyakazi atafariki.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya mafanikio yaliyobainika katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko ni pamoja na maboresho ya matumizi ya mfumo wa TEHAMA ambao unachangia zaidi ya asilimia 80 ya huduma za Mfuko kupatikana kwa njia ya mtandao. Aidha Mfuko umefanikiwa kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa kuingia makubaliano na hospitali na watoa huduma mbalimbali nchini.

2.5.12 **Utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto Wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, Mwongozo wa Taifa wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto Wenye Ulemavu ulizinduliwa rasmi mnamo tarehe 03 Desemba, 2021.

Walengwa wa Mwongozo huo ni pamoja na Wazazi, walezi na Watoto, Maafisa Ustawi wa Jamii, Watoa huduma za Afya, Viongozi na Watendaji wa Serikali za Mitaa na Vijiji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Mwongozo huo umeandaliwa ili kuwawezesha walengwa kufanya Utambuzi wa Mapema wa Watoto Wenye Ulemavu kwa kusudio la kuzuia, kupunguza na kuondoa ulemavu kwa kutekeleza malengo mbalimbali. Moja kati ya malengo hayo ni kuwezesha wazazi/walezi na watoa huduma kuwatambua Watoto wenye Ulemavu na walio hatarini kupata ulemavu kabla na baada ya kujifungua na kuwaunganisha na afua stahiki. Vilevile mwongozo unakusudia kuwaunganisha Watoto wenye Ulemavu na huduma za marekebisho na utengamao; pamoja na kusaidia kuondoa mila na desturi potofu katika jamii zinazo athiri ustawi wa Watoto wenye Ulemavu.

2.5.13 **Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa iliyowasilishwa, Kamati ilibaini kwamba utekelezaji wa masuala ya Watu Wenye Ulemavu umekuwa ukikabiliwa na changamoto ikiwemo ujumuishwaji hafifu na huduma zisizokidhi hali halisi ya mahitaji yao.Kwa msingi huo Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilikamilisha Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini wa mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, lengo kuu la Mwongozo huo ni kutoa maelekezo kwa Wadau kuhusu Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Usawa, Haki, Fursa na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu. Aidha, malengo mengine mahsusi ni pamoja na:-

a) Kutoa mwelekeo utakaowaongoza wadau mbalimbali katika kuandaa afua zinazolenga kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu;

b) Kuainisha hatua mahususi zinazopaswa kuchukuliwa katika kuhakikisha huduma bora zinapatikana na kutolewa kwa Watu wenye Ulemavu; na

c) Kuwezesha uwepo wa mipango shirikishi na jumuishi ya huduma kwenye maeneo yote ya umma na binafsi, ili kuleta tija na ufanisi katika upatikanaji na huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuandaa Mwongozo huu kwa sababu utachochea hatua na mikakati madhubuti ya kujumuisha, na kuimarisha miundombinu na huduma mbalimbali kwa watu wenye ulemavu. Hatua hii pia ni kielelezo cha kuwa na jamii ya kistaarabu ambayo inajali watu wake kwani kipimo cha ustaarabu wa jamii yoyote kinapimwa kwa namna jamii hiyo inavyojali na kuwahudumia watu wenye ulemavu.

> *"How a society treats its disabled is the true measure of civilization."*[3]

2.5.14 **Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(The National Social Security Fund Act)* Sura ya 50 yaliyofanyika Mwaka 2018, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umepewa jukumu la kutoa huduma ya hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi wa sekta binafsi na wale wa sekta isiyo rasmi nchini. Kwa kutambua umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa makundi hayo, Kamati ilishauri NSSF kuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba, kundi kubwa la watu waliojiajiri wenyewe na

[3] Chen Guangcheng, mwanaharakati maarufu wa haki za binadamu kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

kufanya shughuli za uzalishaji mali kwenye sekta isiyo rasmi wanakuwa wanachama wa Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya hatua ambazo Mfuko huu zimefanya, ni kutambua na kuandikisha wanafunzi wa vyuo vikuu ili kuwajengea utamaduni wa kujiwekea akiba na kuwa wanachama wa Hifadhi ya Jamii mapema iwezekanavyo. Kamati inatambua na kupongeza jitihada zilizofanywa na NSSF kuwahusisha pia Wabunge ili kuhamasisha wanachuo kujiunga na Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika**, wazo hili la kuhamasisha vijana wa vyuo vya elimu ya juu nchini kujiunga na Mpango wa Uchangiaji wa Hiari wa NSSF lilitokana na ukweli kwamba idadi ya wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na idadi hiyo haiendani na uwezo wa soko kuwaajiri vijana hawa katika ajira rasmi na ajira za moja kwa moja. Ni dhahiri kwamba kutokana na changamoto hii, fursa kubwa ipo katika kujiajiri mara baada ya kuhitimu masomo yao. Hivyo, utamaduni wa kujiwekea akiba kutokana na fedha kidogo za kujikimu wanazopata wakiwa vyuoni ni wa muhimu kwa wanafunzi hawa, ili ziweze kuwasaidia kuanza maisha ya kujitegemea mara baada ya kuhitimu masomo yao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada hizo za NSSF katika kuhamasisha wanachuo kujiunga na Mfuko, bado kuna umuhimu wa Mfuko huo kuhamasisha zaidi makundi mengine kama vile wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanyabiashara ndogo ndogo na wajasiramali wa aina mbalimbali. Ni ukweli usiopingika kwamba, sekta binafsi na sekta isiyo rasmi zinaajiri kundi kubwa zaidi la jamii, na hivyo basi, hamasa kwa kundi hilo kujiunga na hifadhi ya jamii ni muhimu kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla. Changamoto ambayo Kamati inaona katika eneo hili, ni uwezo wa Mfuko kuwafikia jamii kubwa zaidi ya Watanzania katika muda mfupi inavyowezekana.

2.5.15 **Mfuko Hifadhi ya Jamiii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Hifadhi ya Jamiii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamiii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371 *(The Public Service Social Security Fund Act, Cap 371)*. Lengo la kuanzisha Mfuko huu lilikuwa ni la kuunganisha Mifuko ya Pensheni ya PSPF, LAPF, GEPF na PPF na kuunda mfuko mmoja wa PSSSF mahsusi kwa ajili ya Watumishi wa Umma pamoja na taasisi na makampuni ambayo Serikali au taasisi zake zinamiliki zaidi ya asilimia 30% ya hisa.

**Mheshimiwa Spika**, katika mijadala ndani ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mfuko huu, Kamati imeridhishwa na mafanikio ya utekelezaji wake. Moja kati ya mafanikio hayo, ni Serikali kukubaliana na wadau wa sekta ya hifadhi ya jamii, imeweka kikokotoo kipya ambacho kimepanda kwa wastani kutoka 25% iliyolalalamikiwa mwaka 2018 hadi kufikia 33% ambao unaweka usawa na uwiano kwa wanufaika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa Mfuko huu, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa kuhusu utaratibu wa mafao ya kustaafu kabla au ifikapo tarehe ya kustaafu kwa watumishi wa umma. Moja kati ya changamoto hizo, uratibu wa taarifa za wastaafu kutokamilika kwa wakati na hivyo kusababisha usumbufu wakati wa kufuatilia mafao. Kwa sehemu kubwa changamoto hii inachangiwa na waajiri ambao hawatekelezi wajibu wao kikamilifu wa kuwasilisha taarifa za watumishi wao kwa wakati, na kuchelewesha au kutowasilisha michango ipasavyo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)**

2.5.16 **Uratibu wa Masuala ya Muungano**

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti Kamati imefanya vikao na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ili kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kamati inaendelea kupongeza jitihada za Ofisi hii za kuratibu masuala ambayo yanaimarisha Muungano wetu. Katika utekelezaji wake, moja kati ya masuala ya muhimu ambayo Kamati imepata fursa ya kuyachambua ni yale yanayohusu Hoja za Muungano. Kamati imefurahishwa na jitihada zilizofikiwa na Serikali zetu mbili, ambapo tayari hoja nyingi zimepatiwa ufumbuzi kwa kiwango kinachoridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, suala lingine ambalo limekuwa likisisitizwa na Kamati ni suala la uwepo wa Ofisi katika pande zote mbili, kwamba ni vyema Taasisi za Muungano zote zikawa na Ofisi pande katika pande mbili za Muungano. Hadi wakati taarifa hii inaandaliwa, Kamati imebaini kwamba, kati ya Taasisi 33 za Muungano, ni Taasisi 2 tu ambazo hazina Majengo ya Ofisi katika eneo la Zanzibar. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, kwa taasisi ambazo ni za Muungano, kutokuwa na ofisi katika pande zote za Muungano, kunaathiri utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, walengwa wa huduma za taasisi hizo, wanaweza kukosa huduma za msingi kwa ukaribu zaidi.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

2.5.17 **Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST): Hali ya Chuo, Matarajio na Changamoto**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST) kwa

lengo la kufahamu kwa kina namna ambavyo chuo hicho kinatekeleza majukumu yake na changamoto wanazokabiliana nazo. Aidha, Kamati ilipewa taarifa za kina zaidi kuhusu mwenendo wa udahili wa wanafunzi, hali ya ufaulu na masuala mengineyo muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (Law School of Tanzania) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, (Sura ya 425 ya mwaka 2007). Kuanzishwa kwa Taasisi hii ni matokeo ya mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na wataalam mbalimbali ambao ni pamoja na Ripoti ya Tume ya Msekwa ya Mwaka 1974 pamoja na Ripoti Tume ya Bomani ya Mwaka 1996. Kwa pamoja, walipendekeza kwamba iundwe Taasisi inayojitegemea ambayo itatoa, kuendesha, kusimamia programu za mafunzo ya kisheria kwa vitendo kwa wanafunzi waliohitimu shahada ya kwanza ya sheria (LL. B).

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kwamba, hali ya udahili wa Taasisi hiyo tangu kundi la kwanza ($1^{st}$ Cohort) mwaka 2008 imeongezeka kutoka wanafunzi 288 hadi kufikia wanafunzi 792 katika kundi la 32 ($32^{nd}$ Cohort) kwa mwaka 2021. Kamati inapongeza hatua hii kwa sababu inaongeza wigo wa kuwa na wanasheria wengi zaidi ambao wanapata mafunzo kwa vitendo kutoka katika Taasisi hiyo sambamba na uhitaji wa taaluma hii katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo ya udahili, Kamati imebaini kwamba kiwango cha ufaulu cha wanafunzi wanaopita katika taasisi hiyo ni mdogo tofauti na matarajio ya wengi. Kwa wastani kwa mfano, muhtasari wa matokeo ya mtihani kuanzia Kundi la 1 hadi la 17, kiwango cha juu kabisa cha ufaulu *(highest pass rate)* kilikuwa ni asilimia 31.1 tu katika Kundi la 9.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko ya aina mbili. Kwa upande mmoja, Kamati ilitaarifiwa kwamba baadhi ya wanafunzi wameonesha kutoridhishwa kwao na hali ya ufaulu mdogo wakidai kwamba Taasisi hiyo ina mfumo mgumu wa ufundishaji na mitihani na kusababisha wengi wao kufeli huku tayari wamepoteza muda wao na fedha. Kwa upande mwingine, waalimu na wakufunzi wanaofundisha katika Taasisi hiyo wamekuwa wakitoa madai kwamba kiwango cha wanafunzi na matarajio ya maarifa kutoka kwa wanafunzi hao ni cha chini na kinaakisi uwezo mdogo wa taaluma ya sheria waliyo nayo.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili limekuwa na mjadala mkubwa katika siku za hivi karibuni, ambapo Serikali imeunda vikosi kazi mbalimbali na ripoti zao kuonesha kwamba kuna changamoto mbalimbali na moja ya changamoto hizo ni utofauti wa ufundishaji na uelewa wa sheria katika vyuo vyetu kwa ngazi ya shahada ya kwanza.

2.5.18 **Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala (ADR) Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa hii kwa lengo la kujua hatua mbalimbali ambazo Serikali inachukua katika kuongeza jitihada za kutatua migogoro kwa njia mbadala ikiwa ni sehemu ya kumaliza migogoro nje ya mahakama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala una faida mbalimbali ikiwemo kuharakisha zoezi la utoaji haki, kupunguza gharama na kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba bado jamii kubwa haina uelewa kuhusu mfumo huu na njia nyingine zinazoweza kutumika katika kufikia maamuzi na faida zake.

### 2.5.19 Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Kurekebisha Sheria: Mafanikio na Changamoto

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Kurekebisha Sheria imeanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, sura ya 171 ambapo imepewa majukumu mbalimbali. Majukumu makuu ya Tume hiyo ni kufanya mapitio ya sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupendekeza maboresho yake, kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria, na kutoa elimu ya sheria kwa umma kuhusu maendeleo ya sheria mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa iliyowasilishwa kwake, Kamati ilijulishwa kuhusu namna ambavyo tume hiyo inatekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria, na nyenzo zinazotumika kutekeleza majukumu hayo. Moja kati ya nyenzo hizo, ni kushirikisha wananchi kutoa maoni yao. Kamati inapongeza hatua hii kwa kuwa inaongeza uwazi na uwajibikaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya Tume hii. Moja kati ya changamoto hizo, ni kuongezeka kwa mahitaji ya kufanya mapitio na tathmini ya sheria kusikolingana na rasilimali zilizopo. Kamati ilihoji iwapo Tume hiyo ina mpango wowote wa kukabiliana na changamoto hizo, ambapo Tume iliweka bayana mipango yake ya kuendelea kuomba kuongezewa ukomo wa bajeti *(ceiling)* ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

### 2.5.20 Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilianzishwa Mwaka 2018 kwa Hati Idhini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi hii, ambayo ipo kwa mujibu wa Katiba na Sheria nyingine zilizotungwa na Bunge, ina majukumu makuu ya uendeshaji wa mashtaka katika Mahakama za kiraia nchini, pamoja na kuratibu shughuli za upelelezi/uchunguzi

ikiwemo upelelezi/uchunguzi unaofanywa na taasisi kama vile Mamlaka za Uhifadhi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama kama vile Polisi, Uhamiaji na TAKUKURU.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Kamati imebaini kwamba Ofisi hiyo imefanikiwa kuajiri watumishi wa kada mbalimbali. Kamati inapongeza hatua hiyo ya Serikali kwa kuwa inatekeleza ushauri wa Bunge kuhusu hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua mbalimbali ambazo inazichukua ikiwemo kufanya ukaguzi katika magereza ambapo lengo la ukaguzi huu ilikuwa ni kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki kutatua changamoto hizo. Aidha, Kamati inatambua juhudi za Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ya kuendelea kutekeleza Progamu ya kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka kwa kusogeza huduma za mashtaka karibu na wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Ofisi hiyo bado ina changamoto ambazo utatuzi wa haraka unahitajika. Moja kati ya changamoto kubwa ni uhaba wa majengo ya ofisi mikoani, na pia kutoka ofisi, ufinyu wa bajeti ya uendeshaji, na kutokuwa na Mfumo Maalum wa Kieletroniki kwa ajili ya Uratibu wa Uendeshaji wa Mashtaka *(Case Management Information System-CMIS)* hasa kwa kuzingatia kwamba tayari Mahakama wanatumia mifumo ya kieletroniki katika usajili na usikilizaji wa kesi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa uendeshaji wa mashauri ya jinai, Taarifa iliyowasilishwa na Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kufikia Desemba 2022, inabainisha mafanikio mbalimbali kuhusu suala la Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Pamoja na mafanikio hayo, Kamati

imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Moja kati ya changamoto zilizopo ni kuchelewa kwa utekelezaji wa hukumu mbalimbali za Mahakama hususan katika mashauri ambayo yanahusisha utaifishaji wa mali za watuhumiwa pale ambapo Serikali imeshindwa kesi.

2.5.21 **Mjadala Kuhusu Lugha ya Mahakama**

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti Kamati ilipokea na kujadili masuala mbalimbali kuhusu utendaji wa Mahakama. Moja kati ya hoja zilizojadiliwa kwa kina na lugha ina yotumika katika mwenendo na maamuzi mbalimbali ya Mahakama. Changamoto kubwa iliyopo ni matumizi ya lugha ya Kiingereza hususan katika hukumu na nyaraka za mwenendo wa mahakama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba Mhimili wa Mahakama unakusudia kusanifu programu maalum *(software)* ambayo itatumika kutafsiri mwenendo wa mashauri na hukumu mahakamani kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili. Kamati inapongeza hatua hiyo ya Mahakama kwa sababu itarahisisha uelewa kwa wananchi kuhusu maamuzi na mwenenendo wa mashauri mahakamani.

2.5.22 **Uratibu wa Majukumu ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu, Ufilisi na Udhamini**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii iliwasilishwa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa lengo la kuwapatia Wajumbe uelewa kuhusu mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa uratibu wa majukumu ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria za nchi, RITA imepewa majukumu mbalimbali ikiwemo kufanya usajili na utoaji wa vyeti kwa matukio ya vizazi, vifo na sababu zake yanayotokea Tanzania Bara; kuandikisha na kutoa shahada

za ndoa kwa wafungisha ndoa na leseni za kufungisha ndoa; na pia kusajili na kusimamia bodi za wadhamini.

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa iliyowasilishwa, Serikali ilibainisha mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya RITA. Mafaniko hayo ni pamoja na:-

a) kuongezeka kwa idadi ya watoto waliosajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa;

b) kubuni Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri wa Miaka 5-17 walio Shuleni;

c) matumizi ya mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (e-RITA) unaoruhusu kutuma maombi ya huduma za usajili wa kizazi na kifo popote na kupata cheti wilayani

d) RITA kwa Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) kubuni mfumo wa kielektroniki utakaorahisisha usajili na upatikanaji wa marejesho ya ndoa zote zinazofungwa nchini pamoja na upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali za wasajili wa ndoa hizo: na

e) kuanzisha mfumo wa kieletroniki wa utoaji huduma za bodi za wadhamini. Mfumo huu unarahisisha usajili na upatikanaji wa taarifa mbalimbali za bodi za wadhamini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza RITA kwa ubunifu mbalimbali ambao kwa ujumla wake unasaidia juhudi za Serikali za kuendelea kusogeza huduma kwa wananchi kwa njia ya mtandao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa ambazo zinaathiri utekelezaji wa majukumu ya RITA. Miongoni mwa

changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa watumishi, ukubwa wa gharama za uendeshaji ukilinganisha na ada zitokanazo na huduma wanazotoa, pamoja na ukubwa wa gharama za kuhifadhi mifumo na kubadilishana taarifa baina yake na taasisi nyingine za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoukabili mfumo wa ufilisi nchini. Changamoto hizo ni pamoja na wingi wa sheria na mamlaka nyingi tofauti ambazo zinasimamia ufilisi, na kutokuwepo kwa chombo mahsusi cha kusimamia wataalam wa ufilisi. Changamoto hizi zimesababisha mfumo wa kisheria wa ufilisi kutoeleweka ipasavyo na kuwepo kwa mkanganyiko katika usimamizi wa masuala ya ufilisi.

2.5.23 **Utendaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali *(Solicitor General)* ilianzishwa kisheria mwaka 2018 kwa lengo kuimarisha uwezo wa Serikali katika kuratibu, kusimamia, kushauri na kuendesha mashauri yote ya madai. Mashauri hayo yanajumuisha mashauri yanayohusu Katiba, Haki za Binadamu, Katiba, Uchaguzi na Mashauri ya Usuluhishi yanayofungulia na Serikali/Taasisi zake au dhidi ya Serikali/Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kupongeza mchango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano *(Government Negotiation Teams)* na kufanikisha kumaliza mashauri/migogoro mbalimbali kwa njia ya majadiliano, usuluhishi na maridhiano nje ya Mahakama. Kwa hatua hii, Ofisi imesaidia Serikali kuepuka gharama kubwa za kutumia Mawakili wa kujitegemea wa ndani na nje ya nchi na kuokoa fedha nyingi ambazo zingelipwa kwa wadai endapo wangeshinda kesi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Ofisi hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa watumishi hasa mawakili wenye stadi maalum, ufinyu wa bajeti, na uhaba wa vitendea kazi.

2.6 **Semina, Mafunzo na Ushiriki wa Matukio Mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawashukuru sana wadau wote ambao walijitokeza katika kutoa semina za mafunzo na kuwajengewa uwezo Wajumbe wa Kamati. Semina na warsha hizo zimekuwa na manufaa katika kuongeza uelewa wa Wajumbe katika sekta mbalimbali zinazosimamiwa na Kamati. Mafunzo ambayo Kamati imeyapata yamekuwa na faida sana katika kuiwezesha Kamati kutoa ushauri wenye tija. Ni imani ya Kamati kuwa ushirikiano huo utaendelea katika kuijengea Kamati uwezo kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Aidha Kamati inazishukuru Wizara na Taasisi zake ambazo mara kwa mara wamekuwa wakialika Wajumbe wa Kamati hii katika matukio mbalimbali. Kamati inatoa rai na kuendelea kushauri kwamba kwamba, ushirikiano huu endelee.

**SEHEMU YA TATU**

3.0 **MAONI NA MAPENDEKEZO**

3.1 **Maoni ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Mafanikio, Changamoto na yaliyobainika katika kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ina maoni yafuatayo: -

a) Suala la upungufu wa rasilimali watu limekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa baadhi ya Taasisi na hivyo kuathiri utendaji kazi wa Taasisi hizo, Wizara na Serikali kwa ujumla. Pamoja na kwamba Kamati inatambua juhudi za Serikali kuongeza idadi ya watumishi ili kutatua changamoto hii, kuna umuhimu pia kwa Serikali

kuwa na mahitaji ya msingi hasa vifaa, vitendea kazi na miundombionu ya mazingira ya kazi vinaboreshwa pia.

b) Kamati inapongeza Wizara na taasisi zake kwa kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kwa baadhi ya Wizara na taasisi za Serikali hazina utamaduni wa kutenga fedha za kufanya ukarabati mdogo mdogo wa mara kwa mara kwa miradi hiyo. Kamati ina maoni kwamba, kwa kutotenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa aina hiyo, miradi hiyo inaweza kuanza kupoteza ubora wake. Hivyo basi, ni vema Wizara na taasisi zake zikajenga utamaduni wa kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa namna hiyo.

3.2**Mapendekezo**

3.2.1 **OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU)**

a) **Upanuzi wa Eneo la Mji wa Serikali**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba Serikali ina mpango wa kufanya upanuzi wa eneo la Mji Serikali ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma, ikiwa ni sehemu ya Mradi wa Ujenzi wa Mji huo

**NA KWA KUWA** Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu zoezi la kusimamia ujenzi unaoendelea pamoja na kuratibu zoezi la utwaaji ardhi kwa eneo linalokusudiwa kuongezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri ya Jiji la Dodoma,

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) Kuhakikisha fedha zote zilizopangwa kutekeleza Mradi huu zinatolewa kwa wakati

ii) Serikali ihakikishe inapotekeleza zoezi la utwaaaji ardhi inazingatia taratibu zote za kisheria ikiwemo kushirikisha Wananchi.

b) **Uendeshaji wa Shughuli za Baraza la Taifa la Biashara Katika Ngazi za Mikoa na Wilaya**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba kuna changamoto ya kasi isiyoridhisha ya utekelezaji wa maazimio ya vikao na mikutano ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) katika ngazi ya Mikoa (RBCs) na ile ya Mabaraza ya Biashara ya Wilaya (DBCs) ambayo inadhoofisha majadiliano na maazimio kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi hizo

**NA KWA KUWA** changamoto hiyo kwa kiasi kikubwa inachangiwa na kuwepo kwa idadi ndogo ya Watumishi wenye utaalamu na uzoefu kwa ajili ya kuendesha majadiliano ambao pia wanaweza kufanya uchambuzi wa mazingira ya biashara ili kushauri ipasavyo

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kuwa na mkakati wa haraka na endelevu wa kuongeza watumishi kulingana na mahitaji ya Baraza hili katika ngazi za mikoa na wilaya.

ii) kuhakikisha kuna ushiriki wa kutosha wa wadau muhimu katika Mikutano ya TNBC katika ngazi hizo

c) **Ufanisi wa Utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali unakabiliwa na changamoto mbalimbali zinaoathiri ufanisi ikiwemo uhaba wa watumishi, uchakavu wa vitendea kazi

**NA KWA KUWA** Idara hiyo ina umuhimu katika kuchapa na kuchapisha nyaraka mbalimbali za Serikali ambazo kwa muda mrefu, baadhi ya nyaraka hizo zimekuwa zikichapwa au kuchapishwa kwa kampuni binafsi ambako kunaathiri ubora, ulinganifu na usiri

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya utafiti na kuja na mapendekezo ambayo yatasababisha Idara hiyo kuongezewa uwezo, uhuru na miundombinu yote muhimu ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi na viwango bora.

3.2.2 **OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)**

a) **Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu**

**KWA KUWA** Kamati inatambua juhudi ambazo Serikali imezifanya za kuhakikisha kwamba inaandaa Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwahi na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu,

**NA KWA KUWA** Mwongozo huo ni muhimu katika mipango ya nchi katika mustakabali ya maendeleo ya watu wake,

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) inaweka mikakati madhubuti na endelevu ya kuhakikisha kwamba elimu inatolewa kwa taasisi zote za Serikali na umma kwa jumla kuhusu Mwongozo huo
ii) inafanya Tafiti, upatikanaji taarifa na Takwimu muhimu kuhusu Watu Wenye Ulemavu
iii) kila taasisi ya Serikali inahakikisha kwamba inatekeleza kikamilifu vipengele vya Mwongozo huu kulingana na mahitaji yaliyopo

iv) kuimarisha Ushiriki na Ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu katika maamuzi mbalimbali yenye kuboresha utekelezaji wa Mwongozo huo.

b) **Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Vijana**

**KWA KUWA** lengo la Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ni kuwajengea uwezo vijana, kuwawezesha na kuwaongoza vijana na wadau wengine katika utekelezaji wa masuala ya maendeleo ya vijana.

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kutokuwepo kwa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo suala ambalo limesababisha kutokuwepo kwa ufanisi katika uratibu, na ufuatiliaji wa utekelezaji wake unaokwamisha maendeleo ya vijana

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kuharakisha mchakato wa mapitio ya Sera hiyo, na hatimaye ikamilike mapema iwezekanavyo kwa lengo la kuiboresha au kuiandika upya ili iendane na mazingira ya sasa.

c) **Mfuko wa Maendeleo wa Vijana**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba,hadi kufikia Februari 2022, kiasi cha fedha Sh. 205,000,000 zilikuwa zimetolewa kwa vijana walioomba mna kukidhi vigezo kati ya Sh. 1,000,000,000iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 sawa na **asilimia 20.5** tu;

**NA KWA KUWA** kiasi kikubwa cha fedha iliyobaki ambacho hakijawanufaisha vijana kinaashiria kwamba vijana wasiokuwa na vigezo ni wengi kuliko walionufaika na Mfuko huo;

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kutoa elimu ya kutosha kwa vijana nchini ili waweze kunufaika na Mfuko huo

ii) kutathmini vigezo vilivyowekwa ili vijana wengi zaidi wanufaike na mradi

iii) kuongeza thamani ya Mfuko kwa kuuongezea fedha

d) **Masuala ya Kazi na Ajira**

**KWA KUWA** Kamati inatambua kwamba ukosefu wa ajira hasa kwa vijana ni changamoto ambayo ina athari kijamii na kiuchumi

**NA KWA KUWA** Ofisi ya Waziri Mkuu ina wajibu wa kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya kukuza ajira na kutoa huduma za ajira ili kuongeza nafasi za ajira kwa watanzania ndani na nje ya nchi

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kuongeza jitihada za kusimamia Sera na Sheria mbalimbali ambazo zinaweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara

ii) kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili viweze kuajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi nchini na vijana wengine kujiajiri wenyewe

iii) kubuni utaratibu madhubuti na wenye uwazi ambao utaratibu zoezi zima la ajira Serikalini kwa namna ambayo, nafasi zitakozajazwa zitaakisi umoja wa kitaifa bila kuathiri vigezo

iv) kuwa na mpango wa kuhamasisha vijana nchini kujifunza stadi za kazi za kimkakati na baadae

kuwaunganisha vijana hao na fursa za kazi zenye staha nje ya nchi kulingana na ushindani wa soko la ajira la kimataifa katika sekta za mbalimbali kwa kushirikiana na balozi zetu

e) **Matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki katika Usuluhishi na Uamuzi**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2023 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ilikuwa imesimika na kutumia mfumo wa kielektroniki katika Ofisi 10 tu kati ya Ofisi 32 nchini;

**NA KWA KUWA** kutotumika kwa mfumo wa kielektroniki katika Ofisi ambazo hazina mfumo huo kunaathiri ufanisi wa utetekelezaji wa majumu ya Tume hiyo katika uendeshaji wa mashauri na kutunza kumbukummbu;

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kuongeza fedha katika Bajeti ya Serikali ili Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) iweze kusimika mfumo wa kielektroniki wa uendeshaji mashauri na utunzaji kumbukumbu katika ofisi zake zote.

f) **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba kuna changamoto kwa baadhi ya wastaafu wa utumishi wa umma kupata stahiki zao kwa ukamilifu na kwa wakati, kitu ambacho kinasababisha usumbufu na kadhia kwa wastaafu hao

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba, changamoto hiyo inaweza kusababishwa na baadhi ya Waajiri ambao aidha wamechelewa kuwasilisha taarifa muhimu za wastaafu hao kwa ukamilifu na kwa wakati,

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) PSSSF ifuatilie michango na kuhakikisha inalipwa kikamilifu

ii) PSSSF ichukue hatua kali za kisheria na kinidhamu kwa mwajiri wajiri ambaye hajawasilisha michango kwa wakati na kwa ukamilifu

iii) PSSSF kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wanachama kuhusu umhimu wa kufuatilia na kupata taarifa zao binafsi na michango yao.

g) **Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Sekta Isiyo Rasmi**

**KWA KUWA** binafsi na sekta isiyo rasmi zina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi ambapo inajumuisha kundi kubwa zaidi la watu wakiwemo wajasiriamali, wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara mbalimbali

**NA KWA KUWA** kuna umuhimu wa kundi hilo kuwa na hifadhi ya jamii kwa lengo la kuwapatia stahiki mbalimbali ikiwemo huduma za msingi, mafao tofauti pamoja na pensheni

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kuongeza jitihada za kuhamasisha watu wengi zaidi kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

ii) kubuni mifumo na njia rahisi zaidi zitakazowezesha jamii kubwa ya Watanzania kujiunga, kutumia huduma, na kupata stahiki zitokanazo na kuwa wanachama wa NSSF

3.2.3 **OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

a) **Hoja za Muungano**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba Serikali zetu mbili tayari zimekubaliana kuhusu masuala ya msingi ili kuzipatia ufumbuzi Hoja za Muungano;

**NA KWA KUWA** ufumbuzi uliopatikana unahitaji kutekelezwa na pande zote mbili za Muungano

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) Kuharakisha utekelezaji wa makubaliano hayo kwa lengo la kutatua hoja zote za Muungano; na

ii) Elimu itolewe zaidi kwa umma kuhusu hatua ambazo zimechukuliwa kutatua Hoja za Muungano.

b) **Taasisi za Muungano**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba, kuna Taasisi za Muungano ambazo hazina Ofisi katika upande wa Zanzibar.

**NA KWA KUWA** kwa kutokuwepo kwa Ofisi hizo, kunaweza kusababisha wananchi kukosa huduma zinazotolewa na taasisi hizo kwa ukaribu zaidi;

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Muungano zinakuwa na Ofisi pande zote za Muungano mapema iwezekanvyo.

3.2.4 **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

c) **Lugha ya Uandishi wa Sheria**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba Serikali imeanza utaratibu wa kuwasilisha Bungeni Miswada kwa lugha ya Kiswahili pekee,

**NA KWA KUWA** matumizi ya Lugha ya Kiswahili peke yake katika uandishi wa Sheria yanaweza kuleta changamoto ya tafsiri na utekelezaji wa sheria husika,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ifanye utafiti wa kutosha kuhusu namna bora ya matumizi ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika uandishi wa sheria; na

ii) Taarifa ya Utafiti huo iwasilishwe Bungeni kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu matumizi ya lugha ya uandishi wa sheria.

d) **Lugha ya Mahakama**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba kuna changamoto ya uelewa wa maamuzi na mwenendo wa mashauri mahakamani inayotokana na matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa kuwa wananchi walio wengi hawaielewi

**NA KWA KUWA** changamoto hiyo inapelekea kucheleweshwa kupatikana kwa haki kwa wananchi

**KWA HIYO** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kusanifu programu ya kutafsiri mwenendo wa mashauri na hukumu za Mahakama kutoka katika Lugha ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya Kiswahili ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka.

e) **Ushiriki wa Wadau katika Kuandaa Miswada ya Sheria**

**KWA KUWA** suala la ushiriki wa wadau husika katika mchakato wa utungwaji wa sheria nchini ni takwa muhimu la kisheria,

**NA KWA KUWA** ushiriki wa wadau hao katika mchakato huo unasaidia kuleta uelewa kwa wananchi na kupunguza marekebisho makubwa ambayo hutokea wakati wa uchambuzi wa muswada katika ngazi ya Kamati.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali ihakikishe na kuthibitisha kuhusu ushiriki wa wadau husika katika maandalizi ya awali ya miswada ya Sheria.

f) **Uendeshaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS)**

**KWA KUWA** Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni taasisi muhimu katika mlinganyo wa HakiJinai nchini ambapo utekekelezaji wenye ufanisi wa majukumu yake ni muhimu katika kuharakisha kesi za jinai, kufanikisha zoezi la kutenganisha shughuli za mashataka na upelelezi,

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba Ofisi hiyo bado ina uhaba wa miundombinu muhimu kwa Watumishi wake ambayo inadhoofisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kuandaa mpango wa haraka na endelevu wa kuhakikisha kwamba Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inapatiwa miundombinu yote muhimu ikiwemo mifumo wezeshi ya kielektroniki, majengo ya ofisi na vitendea kazi.

g) **Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai**

**KWA KUWA** nchi ya Tanzania inaheshimu misingi ya Utawala na Sheria ambayo ni nguzo muhimu ya kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa,

**NA KWA KUWA** suala la uendeshaji wa mashauri ya jinai, unahusisha haki za mtuhumiwa kwa upande mmoja, na wajibu wa mwendesha mashtaka kwa upande mwingine,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kuhakikisha kwamba, inatekeleza maamuzi yote ya Mahakama ili kulinda haki za raia, ikiwemo kurejesha mali zilizotaifishwa iwapo mtuhumiwa ameshinda kesi na pale ambapo hatua zote za rufaa zimekamilika;

ii) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika katika upelelezi, ukamataji, na utaifishaji wa mali za watuhumiwa, kulinda haki za watuhumiwa hao na mali zao bila kuathiri thamani ya mali zao endapo watuhumiwa hao watashinda kesi.

h) **Umuhimu wa Kutilia Mkazo Suala la Utatuzi wa Migogoro Nje ya Mahakama**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba suala la Utatuzi wa Migogoro Nje Mahakama ni hatua muhimu katika kuboresha utoaji haki nchini,

**NA KWA KUWA** utaratibu huo unasaidia kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani, kupunguza gharama za mashauri, kuchochea kukua kwa uchumi, na pia kutumia muda mfupi bila kufungwa na masharti ya kisheria na taratibu za kiufundi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kutoa elimu ya kutosha kwa wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu, na faida za utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama

ii) kuimarisha mifumo ya kisheria na kiutendaji ambayo itachochea utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama kwa ufanisi zaidi

i) **Umuhimu wa Kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali *(Solicitor General)***

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jukumu mahsusi la kuwa mstari wa mbele kuiwakilisha Serikali katika mashauri mbalimbali ya madai yanayoihusisha Serikali ndani na nje ya Nchi, ambapo kwa kufanya hivyo kunasaidia kuongeza ufanisi na kuokoa fedha za umma

**NA KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba, utekelezaji wa jukumu hilo mahsusi una changamoto zinazochangiwa na upungufu wa watumishi hasa mawakili wenye stadi maalum, ufinyu wa bajeti, na uhaba wa vitendea kazi

**KWA HIYO BASI** Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

i) kuongeza ukomo wa bajeti *(ceiling)* ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo

ii) kutathimini uwezekekano wa kuajiri mawakili wa kujitegemea ambao wana stadi maalum katika maeneo maalum yenye maslahi kwa serikali ili kuongeza uwezo wa Ofisi hii kusimamia mashauri kwa weledi na ufanisi zaidi

j) **Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo na Ufaulu wa Wanafunzi**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko kuhusu kiwango cha ufaulu katika Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo *(Law School of Tanzania)*,

**NA KWA KUWA** malalamiko hayo yamesabisha kuwepo kwa madai kuhusu uwezo mdogo wa wanafunzi wanaodahiliwa kwa upande mmoja, lakini pia ugumu wa mfumo wa

mafunzo ambao unasababisha wanafunzi kufeli kwa upande mwingine,

**HIVYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kufikiria na ikibidi kuamua kuanzisha mitihani ya kuingia *(entry examinations)* ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaojiunga na Taasisi hiyo wana ujuzi wa nadharia unaotosheleza kufanya mafunzo kwa vitendo kwa ufanisi;

ii) Mamlaka husika kufanya utafiti wa kutosha kuhusu mitaala na uwezo wa vyuo katika kufundisha taaluma ya sheria nchini.

k) **Marekebisho ya Sheria**

**KWA KUWA** Kamati imebaini ongezeko kubwa la sheria zinazohitaji marekebisho/ mabadiliko ya sheria katika sekta hii, ili ziendane na mazingira ya sasa

**NA KWA KUWA** Mabadiliko hayo hayafanyiki kwa wakati kutokana na changamoto zinazoikabili Tume ya Kurekebisha Sheria
**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kutenga fedha za kutosha kwa Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

ii) Tume ya Kurekebisha Sheria ibuni njia mbadala za zitakazohusisha matumizi ya teknolojia ya mtandao, kuhusisha washauri elekezi *(consultants)* na taasisi za utafiti wa kisheria ili kufanya marekebisho ya sheria yanayoenda na mabadiliko na mazingira yaliyopo sasa.

l) **Kuridhia Mikataba ya Kimataifa**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba, kuna baadhi ya mikataba ya kimataifa ambayo Serikali iliingia lakini lakini ikachelewa kuridhiwa

**NA KWA KUWA** kuchelewa kuridhia mikataba hiyo kunacheleweshа utekelezaji wake ambako kunaweza pia kuathiri mahusiano baina ya wa nchi yetu na nchi nyingine

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na taasisi husika za kisekta, kuhakikisha kwamba inafanya utafiti kuhusu mikataba yote ya kimataifa ambayo nchi yetu inahusika lakini bado haijaridhiwa, ili kutoa ushauri stahiki kuhusu umuhimu wa kuridhia au kutoridhia mikataba hiyo.

ii) Kwa ile mikataba ya kimataifa ambayo haijaridhiwa na ina maslahi kwa nchi yetu, Serikali ihakikishe mikataba hiyo inaridhiwa mapema iwezekanavyo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kukupongeza kwa kuteuliwa kuwa Spika wa Nane wa Bunge la Jamahuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati inakuahidi kuendelea kukupa ushirikiano na tunakuombea kila kila la kheri katika utekelezaji bora wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii kwa muda wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.
4. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb.
8. Mhe. Noah Lemburis Ole Saputu Mollel, Mb.
9. Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb.
10. Mhe. Omar Ali Omar, Mb.
11. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
12. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
13. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb.
14. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
15. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb.
16. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb.
17. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
18. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
19. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.
20. Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb.
21. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
22. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
23. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb.
24. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa, niwashukuru viongozi wote wa Mhimili wa Utendaji *(The Executive)* kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake. Kwa heshima kabisa, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
2. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)**
3. Mhe. Dkt. Selemani Said Jafo, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)**
4. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb. – **Waziri wa Katiba na Sheria**
5. Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mb. – **Mwanasheria Mkuu wa Serikali**
6. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – **Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
7. Mhe. Paschal Patrobas Katambi, Mb. – **Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)**
8. Mhe. Khamis Hamza Khamis, Mb. - **Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)**
9. Mhe. Geophrey Mizengo Pinda, Mb. – **Naibu Waziri wa Katiba na Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, vile vile niwashukuru Watendaji wote wa Mhimili wa Utendaji *(The Executive)* na Mhimili wa Mahakama *(The Judiciary)* kwa ushirikiano walioipatia Kamati. Kwa niaba yao wote naomba niwatambue viongozi wao kama ifuatavyo:-

1. Dkt. John Anthony Jingu – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
2. Prof. Jamal Adam Katundu – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)**
3. Ndg. Mary Ngelela Maganga – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)**
4. Ndg. Mary Gabriel Makondo – **Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria**
5. Prof. Elisante Ole Gabriel – **Mtendaji Mkuu wa Mahakama**

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge **Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*** kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Elihaika Mtui na Ndg. Yona Kirumbi wakisaidiwa na Ndg. Theresia Jacob kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

4.2 **Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako sasa liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria**
08 FEBRUARI, 2023

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Dkt. Joseph Kizito Mhagama. Na hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Kabla sijamuita Mwenyekiti, kuna mgeni; naomba tumtambue mgeni wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kagera ambaye huyu mgeni wake ni kaka yake ambaye anatoka Jijini Dar es Salaam anaitwa Ndugu Elias Patrick Elias, karibu sana kaka yetu kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati karibu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Awali ya yote naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inaelezea kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia mwezi Februari, 2022 hadi mwezi Januari, 2023 kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi kinachotolewa taarifa zilihusu udhibiti wa madaraka ya Bunge ya kutunga Sheria yanayokasimiwa kwa mamlaka za utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo wa Taarifa. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla, sehemu ya pili inahusu shughuli zilizotekelezwa, sehemu ya tatu ni maoni na mapendekezo kutokana na shughuli zilizotekelezwa na sehemu ya nne ni hHitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii pia ina viambatisho viwili ambavyo ni cha kwanza, Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba. Kiambatisho cha pili, Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati umebainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni za Bunge na Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Katiba imebainisha lengo kuu la Serikali kuwa ni ustawi wa wananchi na mamlaka ya kutunga sheria za nchi kuwa ni ya Bunge na kwamba, Bunge linaweza kukasimu madaraka yake kwa mtu au mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, ni matarajio kuwa Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria zitaakisi namna Bunge linavyotekeleza madaraka hayo. Matarajio hayo yanahusiana na maneno ya Profesa Kenneth Bailey, aliyewahi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali ya Australia mwa 1930 ambaye alisema, nanukuu; *"It is for the Executive in making regulations to declare what parliament itself would have laid down had its mind been directed to the precise circumstances.'* Mwisho wa kunukuu.

Kwa tafsiri ya Kiswahili, tunaweza kusema yafuatayo; *"Katika utunzi wa kanuni zake, Serikali inatakiwa kutamka kile ambacho Bunge lenyewe lingeweza kutamka kama lingeelekeza nguvu zake katika utunzi wa kanuni hizo kwa kuzingatia mazingira yanayohusika"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Tanzania kama yalivyo Mabunge mengine duniani linapaswa kuendelea na utaratibu wa kufuatilia, na kwa kufanya hivyo litaweza kujiridhisha iwapo madaraka yaliyokasimiwa yametumika kwa namna ambavyo Bunge lingeweza kuyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanataka Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni kuonesha njia au mbinu zilizotumiwa na Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Kamati ilitumia njia kuu sita kama inavyoainishwa katika Taarifa ya Kamati. Njia hizo zimeiwezesha Kamati kupata matokeo ya uchambuzi kwa namna inayotoa matumaini. Niwashukuru

Mawaziri waliohusika na Sheria Ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati, ufafanuzi wa shughuli zilizotekelezwa umeelezwa kwa kina katika sehemu ya pili ya taarifa hii. Shughuli hizo ni uchambuzi wa sheria ndogo na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa sheria ndogo na maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Kwa kuwa kila shughuli ni chanzo cha mapendekezo ya hoja ya Kamati, naomba kufafanua shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shughuli ya kwanza iliyotekelezwa na Kamati ilihusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa. Matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge yalikwisha wasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane, mnamo tarehe 21 Septemba, 2022. Matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa yanawasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli mahususi zilizotekelezwa katika uchambuzi wa sheria ndogo zilizingatia umuhimu wa kubaini iwapo kuna dosari au hakuna dosari katika kutumia madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka zingine. Aidha, utaratibu wa kupata maelezo ya mamlaka zinazohusika ulizingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya bunge kuhusu sheria ndogo; katika kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo 24 ambazo ziliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne. Matokeo ya ufuatiliaji wa

maazimio kuhusu sheria ndogo hizo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 21 Septemba, 2022 wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge. Kwa upande wa maazimio kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba, matokeo yake yanaelezewa katika Taarifa hii. Lengo ni kulionesha Bunge hatua inayofikiwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge yanafaa kuripotiwa. Matokeo hayo yanaonesha kwamba, hatua za utekelezaji zilizoripotiwa zinagawanyika katika makundi makuu matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua hatua hizo za utekelezaji ili kuliwezesha Bunge kufuatilia ipasavyo na hatimaye kutoa maazimio yanayostahili. Katika kufanya hivyo, naomba kubainisha Wizara saba zinazohusika na sheria ndogo zilizopata maazimio ya Bunge. Wizara hizo ni: -

i. Ofisi ya Rais *TAMISEMI* ilikuwa na sheria ndogo nne;
ii. Wizara ya Fedha ilikuwa na sheria ndogo nne;
iii. Wizara ya Afya ilikuwa sheria ndogo mbili;
iv. Wizara ya Nishati ilikuwa sheria ndogo tatu;
v. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikuwa na sheria ndogo moja;
vi. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilikuwa na sheria ndogo nne; na mwisho
vii. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyokuwa na sheria ndogo tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taswira halisi ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inabainishwa katika Kiambatisho Na. 1 (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa

Tano, Mkutano wa Sita, na Mkutano wa Saba). Jedwali hilo ambalo ni sehemu ya Taarifa hii linafafanua hatua sita zilizofikiwa na Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nzuri na ya kupongezwa ni ile ya kukamilisha marekebisho na kutangazwa katika Gazeti la Serikali, kwa sababu hatua hiyo inajielekeza kwenye kuondoa hitilafu zilizobainishwa. Kundi hili linahusu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kundi jingine linajumuisha hatua za Utekelezaji uliochelewa ambazo nayo inarekebisha hitilafu zilizobainika lakini kwa kuchelewa. Hatua hizo si mbaya ingawa ingelifaa kukamilisha mapema ili kupunguza muda wa athari hasi za dosari zilizobainishwa. Wizara zilizofikia hatua hizo ni: -

Wizara ya Afya iliyofikia hatua ya rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo iliyohakikiwa na kusubiri namba ya tangazo la Serikali;

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliyofikia hatua ya rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliyofikia hatua ya rasimu ya marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

Wizara za Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambazo bado zinaendelea kukamilisha mchakato wa rasimu ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika baadhi ya sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la mwisho linahusu Wizara ambazo hazijatekeleza Maazimio ya Bunge katika baadhi ya

sheria ndogo. Wizara hizo ni Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Mipango; na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Kutokutekelezwa kwa maazimio kunaendeleza changamoto ambazo Bunge limeziona katika sheria ndogo mbalimbali hivyo kushindwa kutatua kero zilizokusudiwa kuondolewa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo ambazo ziliwasilishwa bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge, yanabainisha jumla ya sheria ndogo 31 kuwa na dosari mbalimbali. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge lako na kuwezesha mjadala mzuri, dosari zilizobainika katika sheria ndogo zilizochambuliwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya kukinzana na masharti ya katiba; sheria ndogo hutungwa kwa madhumuni ya kufanikisha lengo kuu la Sheria Mama. Aidha, sheria ndogo zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni sheria Kuu ya nchi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa sheria ndogo zilikuwa na maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba. Kwa mfano, kifungu cha 5(5) cha sheria ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022 kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo lolote na muda wowote kwa lengo la kukusanya ada au ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka anayopewa afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo lolote na muda wowote usio na kikomo cha ndani ya muda wa kazi yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha. Ikiwa Bunge litaruhusu utaratibu huu uendelee unaowekwa na sheria ndogo hizo, basi litakuwa linabariki uvunjaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo chini ya Ibara ya 16(1) ya Katiba ambayo imeelekeza bayana kuwa kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi

yake na maisha yake binafsi na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna yoyote ile sheria ndogo haipaswi kukinzana na Katiba ya nchi ambayo ni sheria mama ya sheria zote, hivyo iwapo sheria ndogo itakinzana na Katiba inakuwa ni batili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya kukinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi; sheria ndogo hutungwa ili kufafanua au kuwezesha utekelezaji wa malengo ya sheria mama inayoanzisha sheria ndogo inayohusika. Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa, umebaini kasoro ya sheria ndogo kuwa na maudhui yanayokinzana na sheria mama. Mfano wa sheria ndogo yenye maudhui hayo, ni *The Merchant Shipping (Maritime Labour), Regulations 2022*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 83 inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya kanuni ambapo hakuna kanuni mahsusi inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini Shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na Dola za Marekani 500 au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja. Wakati huo huo sheria mama chini ya Kifungu cha 401, imeweka adhabu ya jumla iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo kuwa atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenye thamani ya Dola za Kimarekani 1000 au kifungo cha muda usiopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu iliyowekwa katika kanuni inakinzana na adhabu iliyowekwa na sheria mama ambapo, kukinzana huko ni kwenye kiasi cha faini kilichotajwa kwenye sheria ndogo ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria mama; na

adhabu ya kifungo inayowekwa na sheria ndogo ni kubwa kuliko iliyowekwa katika sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Bunge kuwa, mamlaka za Serikali zilizokasimiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo, zitunge sheria hizo kwa kuendana na matakwa ya sheria mama zilizotungwa na Bunge. Inapotokea sheria ndogo imeweka masharti yanayokinzana na sheria mama, kamwe Bunge haliwezi kufumbia macho dosari hiyo kwakuwa, inaweza kufifisha lengo lililokusudiwa na sheria mama na sheria nyingine za nchi zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya kutoendana na misingi bora ya uandishi wa sheria; sheria za Bunge huandikwa kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa Sheria. Misingi hiyo huwezesha kuweka mawazo ghafi katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana katika masharti ya sheria inayohusika. Bunge hili huzingatia misingi hiyo kutokana na kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria nchini. Hivyo, sheria ndogo pia zinatarajiwa kuzingatia ipasavyo misingi ya uandishi wa sheria nchini. Hata hivyo, kutokana na uchambuzi wa kina, sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa sheria ndogo yenye dosari kutoendana na misingi bora ya uandishi ni *The Banking and Financial Institutions (Mortgage Refinance Companies) Regulations, 2022*. Kanuni ya 6(3) (b) inaweka kiwango cha ada ya usajili ya shilingi milioni tano au kiwango kingine kitakachoamuliwa na Benki Kuu, kwa mtu anayetaka kuanza biashara ya *mortgage re–financing*. Kanuni imetoa mwanya kwa Benki Kuu kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua. Kiasi hicho kilichotajwa hakifafanui ukomo wa chini wala wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inaweza kusababisha kutoeleweka kwa ada halisi ya usajili, uwezekano wa uwepo

wa viwango mbalimbali vya ada ya usajili na kuleta mkanganyiko kwa watekelezaji wa kanuni hizi. Hii pia ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria nchini inayotaka sheria ndogo yeyote inayotaja viwango vya ada na tozo kuainisha viwango kwa namna ambayo haitaleta utata katika utafsiri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya kukosa uhalisia; pamoja na mambo mengine, utungaji mzuri wa sheria huzingatia uhalisia wa utekelezaji wa sheria inayohusika. Mojawapo ya mambo ya uhalisia yanayozingatiwa ni hali halisi ya walengwa wa sheria inayohusika. Lakini uchambuzi wa Kamati umebaini sheria ndogo kuwa na changamoto ya kuwa na masharti yasiyo na uhalisia. Mfano wa sheria ndogo yenye masharti yasiyo na uhalisia ni Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022. Kifungu cha 14(3) cha sheria ndogo hizo kinachukulia kosa la abiria kutupa takataka nje ya chombo cha usafiri, limetendwa na mmiliki au dereva au kondakta wa chombo hicho. Kifungu hicho kinafafanua kuwa, mtendaji wa kosa hilo atalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhalisia adhabu hulenga kumuadhibu mtenda kosa na kuwaogofya wengine wasitende kosa. Kwa namna ilivyoelezwa adhabu katika Kifungu cha 14 (3), mtenda kosa halisi ni msafiri aliyetupa taka nje ya chombo cha usafiri, lakini anayeadhibiwa ni mmiliki au dereva au kondakta wa chombo kinachohusika. Hali hiyo inaonesha lengo la adhabu halimgusi mlengwa wala haliogofyi watu wengine kutenda kosa kwa kuwa watakaoadhibiwa sio watendaji wa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sharti la adhabu lililowekwa katika kifungu cha 14(3) linasababisha usumbufu kwa wasiotenda kosa linalohusika. Kwa namna hiyo, sheria

ndogo hiyo imeweka adhabu kwa masharti yasiyozingatia uhalisia katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dosari za uandishi wa majedwali; uwepo wa Majedwali katika sheria yeyote hulenga katika kutimiza malengo yaliyokusudiwa na kifungu cha sheria inayohusika, hivyo ni matarajio ya msomaji wa sheria ya kuwa majedwali ndani ya sheria kuendana na matakwa ya kifungu wezeshi. Kukiuka lolote kati ya haya katika uandishi wa majedwali ni makosa. Sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi zimeonesha kuwa na makosa katika majedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa sheria ndogo yenye dosari hizo ni sheria ndogo za afya na usafi wa mazingira za Halmashauri ya Mji wa Bunda, 2022. Jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi linaonesha kuwa limetokana na Kifungu cha 25 linahusu ada ya ukaguzi wa afya. Kwa kawaida kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye jedwali husika. Hata hivyo, jedwali la kwanza linarejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 25 ambacho maudhui yake hayahusiani na Jedwali hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida uandishi wa majedwali katika sheria unalenga kutoa ufafanuzi wa ziada wa maudhui yaliyo katika vifungu. Kwa msingi huo, kutokuandika majedwali kwa ufasaha kunasababisha mkanganyiko katika usomaji wa sheria na unaweza kuathiri malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine wa makosa katika majedwali umeonekana katika sheria ndogo za ada za vibali vya burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022. Jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi linarejea kuanzishwa chini ya kifungu cha 4(2) ambayo maudhui yake hayahusiani na jedwali hilo. Urejeaji wa kanuni isiyoendana kimaudhui unakiuka matakwa yaliyowekwa na kifungu cha

11(3) Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayoelekeza urejeaji sahihi wa vifungu katika majedwali. Hali hii inaleta ugumu wa kueleweka kwa masharti ya kanuni na utekelezaji wa sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine ipatikane, matokeo ya matumizi ya madaraka hayo yanapaswa kuzingatia dhamira ya Bunge katika sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili taarifa hii iweze kuwa na mantiki inayoendana na uchambuzi na mapendekezo naomba kudhihirisha maoni ya Kamati yanayotokana na uchambuzi. Kwa ufupi maoni hayo yapo kwenye mambo saba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sheria ndogo kukinzana na masharti ya katiba; dosari ya sheria ndogo kukinzana na Katiba ya Nchi ni dosari kubwa inayoitoa sheria hiyo nje ya misingi ya utungaji wa sheria. Kamati ina maoni kwamba, Bunge ambalo ni mamlaka ya kutunga sheria, halipaswi kuruhusu madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine yatumike kinyume na misingi ambayo lenyewe, halipaswi na haliwezi kuikiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi; dosari ya sheria ndogo kukinzana na masharti ya sheria mama haipaswi kuendelea kuwepo. Dosari hiyo inavuka madaraka yaliyokabidhiwa kwa mamlaka inayohusika na vilevile, ni kinyume na matarajio ya Bunge ambalo limepewa mamlaka yote ya kutunga sheria za nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa, kuendelea kutumika kwa Sheria Ndogo hiyo, si jambo jema kwa desturi na misingi ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria; Bunge hutunga sheria kwa kuzingatia uandishi ulio bora ili kuwezesha malengo iliyoyakusudia katika sheria inayohusika. Ni maoni ya Kamati kwamba, kutungwa kwa sheria ndogo zinazotofautina na misingi ya uandishi bora wa sheria ni jambo lisiloendana na matarajio ya Bunge na linapaswa kurekebishwa inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia; sheria ndogo zenye masharti yasiyozingatia uhalisia zinaweza kukwamisha malengo ya Bunge kutunga sheria mama inayohusika. Ni maoni ya Kamati kuwa, zaidi ya kukwamisha malengo ya sheria mama, sheria ndogo zenye dosari hiyo zinaweza kusababisha kero kwa wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kuona madaraka yake yanayokabidhiwa kwa mamlaka nyingine hayatumiki kusababisha kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo kukosa usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali; dosari ya sheria ndogo kukosa usahihi inaathiri ukamifu wa ufafanuzi wa sheria za Bunge uliotarajiwa kutolewa kupitia sheria ndogo. Ni maoni ya Kamati kwamba sheria ndogo zilizokosa usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali zinatatiza ufafanuzi uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizohusika. Kwa msingi huo, Bunge lenye nia ya kuwa na sheria zinazoeleweka kwa wananchi linatarajiwa kuonesha hatua zinazostahili ili kurekebisha dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uchelewaji katika kutekeleza maazimio yanayohusu kurekebisha sheria ndogo; Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kero kwa wananchi. Bunge ambalo ni sauti ya wananchi halipaswi kutokusema chochote inapotokea dosari hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa kuchelewa

kutekeleza maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za Sheria Ndogo, ni jambo linalochelewesha utatuzi wa kero za wananchi pale ambapo dosari hizo zinasababisha kero kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge; pamoja na mambo mengine Maazimio ya Bunge hutolewa kwa lengo la kuelekeza utekelezaji wa jambo fulani ambalo Bunge limeshughulikia na kutoa uamuzi, ikiwemo maazimio kuhusu marekebisho ya sheria ndogo. Ni maoni ya Kamati kuwa, kutokuzingatia Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo ni jambo linalokumbatia dosari zilizolengwa kurekebishwa. Bunge ambalo ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria halitarajiwi kuunga mkono desturi ya mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kutunga sheria ndogo kuendelea kukumbatia dosari za sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujumuisha maoni ya Kamati, naomba kulikumbusha Bunge hili kuwa dosari zilizobainika zinaathiri tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kuweka kanuni kwa mamlaka nyingine. Madhara mengine ya dosari hizo ni uwezekano hafifu wa kutimia kwa lengo la baadhi ya sheria zilizotungwa na Bunge na kuendelea kwa desturi isiyofaa katika taratibu wa sheria za nchi. Mambo hayo yanahitaji hatua za haraka za marekebisho na hasa kwa kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maslahi ya wananchi katika utekelezaji wa shughuli za umma. Hali hiyo ndio hasa msingi wa mapendekezo ya maazimio ya Bunge katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Mapendekezo ya Kamati ni maoni yake yaliyotokana na shughuli ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kutokana na Maoni ya Kamati kuhusu dosari zilizojitokeza, Kamati inapendekeza mambo saba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukinzana na Masharti ya Katiba;

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kukinzana na masharti ya katiba, suala ambalo ni kinyume na misingi ya Sheria inayotambua Ukuu wa Katiba,

Na kwa kuwa, ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa Sheria yoyote ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba na endapo Sheria nyingine yoyote itakiuka masharti itakua ni batili,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanyiwe marekebisho ndani ya siku 60 kwa ajili ya kutatua dosari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo au sheria nyingine za nchi;

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa sheria mama inayohusika,

Na kwa kuwa, Kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria Ndogo inayokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi ni batili kwa kiwango cha dosari hiyo,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zirekebishe sheria ndogo hizo ndani ya siku sitini ili kuondoa dosari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria;

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zilibainika kutokuzingatia misingi ya uandishi bora wa sheria,

Na kwa kuwa, dosari ya uandishi bora wa sheria inaweza kuharibu urahisi wa kusomeka kwa sheria ndogo, jambo ambalo halina msaada kwa nia ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zinazohusika,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizo kutwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ndani ya sitini kuanzia leo ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti yasiyo na uhalisia;

Kwa kuwa, dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia imebainika katika baadhi ya sheria ndogo, jambo linaloweza kuchangia ugumu wa utekelezaji,

Na kwa kuwa, athari ya ugumu katika utekelezaji wa sheria ndogo ni jambo linalovuruga upatikanaji wa tija ya sheria ndogo hizo na kuondoa maana ya madhumuni ya kukasimu madaraka ya Bunge kutunga sheria,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo, ili kuendana na uhalisia na kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dosari ya uandishi wa majedwali;

Kwa kuwa, majedwali ni sehemu ya ufafanuzi wa sheria uliolenga kurahisisha uelewa na kutoa ufafanuzi wa vifungu vya sheria.

Na kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zina dosari ya uandishi wa majedwali hali inayosababisha changamoto katika utekelezaji vifungu vya sheria ndogo inayohusika,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo na kubainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchelewaji katika kutekeleza maazimio ya kurekebisha sheria ndogo;

Kwa kuwa, Baadhi ya Mamlaka zimechelewa kutekeleza maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya sheria ndogo, jambo ambalo linaendeleza dosari zilizokuwa zimebainika wakati wa uchambuzi,

Na kwa kuwa, kuchelewa huko kunasababisha kuendelea kuwa na sheria ndogo zenye dosari licha ya Bunge ambalo ni chombo kikuu cha kutunga sheria kuelekeza tofauti,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizobainika kuchelewa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutokutekelezwa kwa maazimio;

Kwa kuwa, zipo mamlaka ambazo hazijatekeleza kabisa maazimio ya Bunge kuhusu Marekebisho ya sheria ndogo hadi muda huu,

Na kwa kuwa, kutokutekelezwa kwa maazimio ya marekebisho ya sheria ndogo kama yalivyotolewa na Bunge ni ishara ya kuendeleza kuwabebesha mzigo wananchi wanaoguswa na sheria ndogo zinazohusika,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizobainika kutotekeleza maazimio ya Bunge zitekeleze maazimio hayo ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo na hatimaye kufanikisha taarifa hii. Naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nimshukuru Mheshimiwa George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Halikadhalika, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali pamoja na watendaji kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*

kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald S. Magili kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Emmy Peter, Ndg. Gwantwa Alex Mwakijungu, na Ndg. Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na msaidizi wa Kamati Ndg. Imelda Ntimba kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2022 HADI JANUARI 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako, Taarifa hii ya mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023.Taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge inayoweka sharti kwa kila Kamati

kuwasilisha Bungeni Taarifa ya mwaka ya shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inaelezea kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kwa kuwa Kanuni hizo zimefafanua majukumu maalumu ya Kamati hii, naomba kubainisha kwamba, shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi kinachotolewa taarifa zilihusu udhibiti wa madaraka ya Bunge ya kutunga Sheria yanayokasimiwa kwa mamlaka ya utendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi chote kinachotolewa taarifa, Kamati ya Sheria Ndogo imeendelea kutekeleza majukumu iliyopewa na Bunge katika eneo la udhibiti wa Sheria Ndogo. Leo naomba kulijulisha Bunge hili kuhusu shughuli zilizofanyika, yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo na mapendekezo kuhusu nini Bunge lifanye au lisifanye kutokana na mambo yaliyobainika kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa madhumuni ya Taarifa hii ni kutoa fursa kwa Bunge kuijadili na hatimaye kupokea na kufanyia kazi Mapendekezo ya Kamati, naomba kutanguliza maelezo ya awali kuhusu muundo wa Taarifa hii. Naamini kwa kufanya hivyo, mawanda (*scope*) na mtiririko utakuwa bayana na rahisi kufuatiliwa kwa ajili ya kujadili ili hatimaye Bunge liamue inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni hayo Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza ni ya utangulizi ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu taarifa hii ili kujenga msingi mzuri wa majadiliano;

(b) Sehemu ya Pili inahusu ufafanuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi kinachohusika ambayo inatoa maelezo kuhusu shughuli hizo, msingi wake na mambo yaliyobainika;

(c) Sehemu ya Tatu inafanya majumuisho ya maoni kutokana na shughuli zilizotekelezwa. Lengo la sehemu hii ni kujenga msingi wa mapendekezo katika hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inayojadiliwa Bungeni leo; na

(d) Sehemu ya Nne na ya mwisho inahitimisha hoja ili kuliomba Bunge lifanye uamuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni ya kumbukumbu na rejea thabiti inayotokana na majadiliano ya hoja hii ya Kamati ya Sheria Ndogo, naomba Bunge lako liipokee na kuijadili Taarifa hii ikiwa na Viambatisho vyake viwili. **Kiambatisho Na. 1** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita, na Mkutano wa Saba). **Kiambatisho Na. 2** (Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa) linaloonesha Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

### 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa shughuli zote za Kamati hii, ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (Katiba). Madaraka hayo yanahusu matumizi ya mamlaka ya Bunge katika utungaji wa Sheria kwa namna iliyoelezwa

kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.1*) na kuwekewa utaratibu katika Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Ufafanuzi kuhusu madaraka ya Bunge kwenye eneo la utungaji wa sheria, masharti yanayopaswa kuzingatiwa katika utungaji wa sheria na utaratibu unaohitaji kufuatwa ni mambo yanayofaa kuongoza majadiliano kuhusu Taarifa hii. Ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo: -

**1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya nchi ni hati kuu inayotoa idhini kwa mambo yote ya kisheria, kisiasa na kijamii katika Taifa. Kwa maana hiyo, Katiba ni msingi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati kutokana na kueleza dhamira ya shughuli zote za umma nchini zinazotungiwa Sheria na kuweka mgawanyo wa madaraka. Aidha, Katiba imekuwa msingi wa shughuli za Kamati hii kwa kuonesha shabaha ya utungaji wa sheria na msingi wa Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zingine.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4** ya Katiba inagawanya Shughuli zote za Mamlaka ya Nchi katika Jamhuri ya Muungano kwenye vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki, na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Katika mgawanyo huo, Bunge ni chombo cha kutunga sheria, Ibara hii pia ndio chimbuko la mantiki ya shughuli za Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli zote hizo zilizogawanywa kwa vyombo vyenye mamlaka tofauti nchini, zinafafanuliwa katika Ibara ya **Ibara ya 8(1)** ya Katiba. Kwa mujibu wa Ibara hiyo, msingi wa mamlaka yote ya nchi yaliyogawanywa kwenye vyombo mbalimbali ni wananchi na kwamba, Serikali inapata mamlaka na madaraka yake yote kutoka kwa

wananchi. Aidha, Ibara ya 8 (1) (b) inasisitiza lengo la Serikali kuwa ni ustawi wa wananchi. Kwa sababu hiyo, haitarajiwi mamlaka yoyote ya nchi itumike kwa namna inayovuruga au inayozuia ustawi wa wananchi. Hali hiyo imekuwa msingi mkuu wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwa na mamlaka ya kutunga Sheria, chini ya Ibara ya 97 (5) ya Katiba, Bunge limepewa uwezo wa kukasimu kwa mtu yeyote au kwa idara yoyote ya Serikali, madaraka ya kuweka Kanuni za nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Msingi wa kukasimu madaraka hayo ni kuwezesha utekelezaji wa Sheria zinazotungwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge linapotekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria za nchi huzingatia mambo yote muhimu katika utungaji wa Sheria hizo ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kwa mantiki hiyo, ni matarajio kuwa Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria na Bunge zitaakisi namna Bunge linavyotekeleza madaraka hayo. Matarajio hayo yanahusiana na maneno ya Profesa Kenneth Bailey, aliyewahi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali ya Australia (1930) ambaye alisema:

**NANUKUU**
*"It is for the Executive in making regulations to declare what parliament itself would have laid down had its mind been directed to the precise circumstances''*
**MWISHO WA KUNUKUU**

Kwa tafsiri ya Kiswahili, tunaweza kusema kwamba:-

"….katika utunzi wa kanuni zake, Serikali inatakiwa kutamka kile ambacho Bunge lenyewe lingeweza

kutamka kama lingeelekeza nguvu zake katika utunzi wa kanuni hizo kwa kuzingatia mazingira yanayohusika….”

**Mheshimiwa Spika,** Bunge la Tanzania kama yalivyo Mabunge mengine duniani linapaswa kuendelea na utaratibu wa kufuatiliana na kwa kufanya hivyo litaweza kujiridhisha iwapo madaraka yaliyokasimiwa yametumika kwa namna ambavyo Bunge lingeweza kuyatumia. Ili kutimiza azma hiyo, uwezo wa kuunda Kamati za Bunge chini ya Ibara ya 96 ya Katiba umetumika kuunda Kamati ya Sheria Ndogo. Lengo la kuwa na Kamati hii ni kuwezesha utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge, ikiwemo kufuatilia utungaji wa Sheria Ndogo nchini. Shabaha kubwa ni kuona kama madaraka ya kutunga Sheria Ndogo yanatumika kwa namna ambayo Bunge lisingeliweza kuyatumia tofauti.

**1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Bunge zinatoa mwongozo kuhusu utaratibu, desturi na uendeshaji wa shughuli zote zinazohusu utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Kwa Tanzania, Kanuni za Bunge ni zao la Ibara ya 89 ya Katiba ya Tanzania. Kanuni hizo zimezingatia masharti ya Ibara ya 96 (1) kwa kuanzisha Kamati za Kudumu za Bunge kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 137 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 11 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimefafanua majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Majukumu hayo ni kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo hazikinzani na Katiba, Sheria inayoruhusu kutungwa kwa Sheria Ndogo zinazohusika na Sheria nyingine za nchi. Kukamilisha jukumu hilo Kamati hutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge lakini kwa lengo la kufaulisha udhibiti wa Sheria Ndogo.

### 1.3.3. Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1

**Mheshimiwa Spika,** Msingi mwingine wa Shughuli za Kamati ya Sheria Ndogo ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Masharti ya Sheria hii ni kitovu cha shughuli za Kamati zinazohusu Udhibiti wa Sheria Ndogo nchini. Imekuwa hivyo kwa sababu, Sheria hii ndiyo inayojumuisha masharti yanayohusu muundo, matumizi, tafsiri, utumikaji wa Sheria za nchi na mambo mengine yanayoendana na hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na madhumuni yake, Sheria ya Tafsiri ya Sheria imeweka masharti yanayohitaji kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo. Masharti hayo yanayohusu misingi ya uandishi wa sheria zikiwemo Sheria Ndogo na utaratibu wa kuzingatiwa katika mchakato wa uandaaji wa sheria hizo, utangazaji wake kwenye Gazeti la Serikali, kutumika kwake na nafasi ya Bunge katika mchakato huo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na masharti hayo, Sheria Ndogo huwekwa Mezani Bungeni kwa mujibu wa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Kifungu hicho kimeweka sharti la kuweka Mezani Sheria Ndogo zote ndani ya siku sita za Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya kuwa zimechapishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, Bunge linaweza kuona iwapo Sheria Ndogo inayohusika inahitaji kubadilishwa, kurekebishwa au kuongezwa masharti mengine.

**Mheshimiwa Spika,** Mantiki ya uwezo huo wa Bunge inatokana na umuhimu wa Sheria Ndogo kukidhi malengo ya Sheria Mama au Sheria nyingine zilizotungwa na Bunge. Maelezo hayo yanazipa Shughuli za Kamati mashiko ya kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo zinaendana na masharti ya Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi. Jumla ya shughuli hizo ni Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo ambao ni jambo la lazima kwa Bunge lenye tija na ufanisi unaloliongoza.

## 1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, imeilazimu Kamati kubainisha njia na mbinu zilizotumika wakati wa kutekeleza majukumu yake. Kufanya hivyo, ni kutimiza masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayotaka Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni kuonesha njia au mbinu zilizotumiwa na Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Kwa masharti hayo naomba kubainisha njia au mbinu zilizotumika kama ifuatavyo: -

(a) Kupitia Magazeti ya Serikali yaliyowasilishwa Mezani ili kupata orodha na jumla ya Sheria Ndogo zote. Lengo la mbinu hiyo ni kupata taswira ya wigo wa kazi ya uchambuzi na kubaini sekta zinazohusika;

(b) Kufanya uchambuzi wa awali wa Sheria Ndogo ili kubaini masharti yanayowekwa na Sheria hizo. Lengo ni kupima uzingatiaji wa masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria zingine za Nchi;

(c) Kuhakiki mtiririko wa maudhui kwa kulinganisha masharti yanayowekwa katika Sheria Ndogo ikiwa ni pamoja na ukamilifu wa Majedwali. Lengo ni kubaini ukamilifu uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka ya ufafanuzi kwa kutumia Sheria Ndogo;

(d) Kuoanisha masharti ya Sheria Ndogo inayohusika na misingi iliyowekwa katika Katiba na Sheria Nyingine za nchi. Lengo ni kujiridhisha na ukubalifu wa Sheria Ndogo kwa misingi ya Sheria za nchi inayopaswa kuzingatiwa;

(e) Kupatanisha maudhui ya Sheria Ndogo na madhumuni ya Sheria Kuu iliyoruhusu kutungwa kwa Sheria Ndogo inayohusika, ili kuhakikisha kuwa maudhui ya Sheria Ndogo hayakinzani na madhumuni ya Sheria Mama. Lengo ni kulishauri Bunge kwa misingi iliyowekwa na Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria; na

(f) Kufanya mahojiano na mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo kwa idhini ya Bunge kwa ajili ya kupata maelezo kuhusu hoja zilizobainishwa. Lengo ni kupata ufafanuzi wa ziada na kufananisha uelewa kuhusu matokeo ya uchambuzi kati ya Kamati na Mamlaka inayohusika. Aidha, njia hii iliwezesha kuchuja hoja zilizotokana na uchambuzi kabla ya kutoa Taarifa hii Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo hayo, naomba kulihakikishia Bunge kwamba, njia na mbinu nilizozitaja, ziliiwezesha Kamati kupata matokeo ya uchambuzi kwa namna inayotoa matumaini. Niwashukuru Mawaziri waliohusika na Sheria Ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao, uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kukidhi matarajio ya uchambuzi wa Sheria Ndogo na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Kamati hii ni kuripoti Bungeni shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari, 2023. Lengo ni kuliwezesha Bunge kubaini mafanikio na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa madaraka ya kuweka Kanuni yaliyokabidhiwa kwa Mamlaka nyingine kwa kipindi hicho. Madhumuni hayo yatatimia kwa kubainisha Shughuli zilizotekelezwa kabla ya kuonesha yatokanayo na shughuli hizo. Kwa urahisi wa kufuatilia mtiririko, shughuli hizo zimegawanyika katika makundi makuu mawili:-

(a) Shughuli za Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo; na

(b) Shughuli za Uchambuzi wa Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa kila shughuli ni chanzo cha mapendekezo katika hoja ya Kamati, naomba kufafanua Shughuli hizo. Ufafanuzi huo unahusu Kamati ilivyofanyia kazi na matokeo ya kazi hiyo kama ifuatavyo: -

**2.1.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari 2023, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ishirini na nne (24) ambazo ziliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne. Matokeo ya ufuatiliaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo hizo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 21 Septemba, 2022 wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba, matokeo yake yanaelezewa katika Taarifa hii. Lengo ni kulionesha Bunge hatua inayofikiwa katika kutekeleza maazimio yake kuhusu madaraka linayokasimu kwa mamlaka zingine kutunga Sheria Ndogo na kulishauri jambo la kufanya au la kutokufanya.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli hiyo ilikamilishwa kwa mambo yafuatayo: -

(a) Kupokea Taarifa za Utekelezaji kabla ya kukutana na mamlaka zilizohusika ili kuoanisha na Maazimio yaliyopitishwa na Bunge. Lengo ni kubaini hatua iliyokuwa imefikiwa katika utekelezaji;

(b) Kuoanisha hatua iliyofikiwa na madhara ya dosari au hitilafu iliyokuwa imebainika. Lengo ni kulionesha Bunge iwapo utekelezaji umeendana na matarajio yake kuhusu madhara ya dosari yaliyopaswa kuondolewa; na

(c) Kukutana na Mamlaka zinazohusika ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusu mashaka yaliyopatikana wakati wa uchambuzi wa taarifa hizo. Lengo ni kuzingatia utaratibu mzuri wa misingi ya asili kisheria ili kufikia msimamo wa kutumainiwa juu ya jambo linalohusika.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hizo zimechangia uthabiti wa matokeo ya uchambuzi yaliyotolewa taarifa hapo awali na mengine yanayoripotiwa leo hii. Kwa hakika ni utaratibu unaostahili kuendelezwa ili kuwawezesha wananchi kupata tija ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge ambalo, kimsingi ni chombo chao cha uwakilishi.

**2.1.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni**

**Mheshimiwa Spika,** Kundi la pili la Shughuli zilizotekelezwa na Kamati zinahusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kwa kuwekewa utaratibu chini ya Kanuni ya 43(2) ya Kanuni za Bunge. Shughuli zilizotekelezwa na Kamati linahusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge yalikwisha wasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane, mnamo tarehe 21 Septemba, 2022. Taarifa hii inaeleza matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa ambayo hayajawasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli mahususi zilizotekelezwa katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizingatia umuhimu wa kubaini iwapo kuna dosari au hakuna dosari katika kutumia madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka zingine. Aidha, utaratibu wa kupata maelezo ya mamlaka zinazohusika ulizingatiwa. Lengo lilikuwa ni kukidhi masharti ya

Kanuni za Bunge yanayohusu majukumu ya Kamati na utaratibu wa kutekeleza majukumu hayo.

### 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako linao wajibu wa kuhakikisha kwamba, madaraka yake ambayo yamekabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Ili kutimiza wajibu huo ni jukumu la Bunge lenyewe kufuatilia ipasavyo namna madaraka hayo yanavyotumika. Kwa maneno mengine, Bunge halipaswi kuishia kwenye kubainisha dosari katika Sheria Ndogo na kuamua kwa njia ya maazimio. Kwa kawaida, Bunge linapaswa kujiridhisha iwapo dosari hizo zimerekebishwa kwa namna ilivyoazimiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Sheria Ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, dosari zinazojitokeza katika Sheria hizo, zinapaswa kufanyiwa kazi kwa utaratibu unaoendana na desturi za Bunge. Bila kufanya hivyo, madhara ya dosari zote yanavyoendelea yanaweza kuliweka Bunge kwenye kulaumiwa na wananchi. Bunge hili ambalo ni chombo halisi cha wananchi haliwezi kuacha kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari katika Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuwezesha tija ya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ulizingatia hatua iliyoripotiwa kuwa imefikiwa kwa kudadisi wa mambo yafuatayo:-

(a) Iwapo hakuna Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyoandaliwa;

(b) Iwapo marekebisho yaliyoazimiwa yamezingatiwa katika Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo inayohusika;

(c) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo imepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki;

(d) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefikia hatua ya kusubiri kutangazwa; na

(e) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo inayohusika imetangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** udadisi kwa kuegemea katika vigezo hivyo, uliiwezesha Kamati kutathmini hali ya utekelezaji wa kila azimio lililotolewa na Bunge na hatimaye kupata matokeo halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Matokeo hayo yataliwezesha Bunge kuamua kuhusu hatua inayofuata.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge yanafaa kuripotiwa. Matokeo hayo yanaonesha kwamba, hatua za utekelezaji zilizoripotiwa zinagawanyika katika makundi makuu sita yafuatayo: -

(a) Hatua ya kutotekeleza Maazimio ya Bunge;

(b) Hatua ya Kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho;

(c) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki;

(d) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;

(e) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali; na

(f) Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kufafanua hatua hizo za utekelezaji ili kuliwezesha Bunge kufuatilia ipasavyo na hatimaye kutoa maazimio yanayostahili. Katika kufanya hivyo, naomba kubainisha Wizara saba (7) zinazohusika na Sheria Ndogo zilizopata maazimio ya Bunge. Wizara hizo ni: -

(a) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliyokuwa na Sheria Ndogo nne (4) zilizobainika kuwa na jumla ya hoja tisa (9);

(b) Wizara ya Fedha na Mipango iliyokuwa na Sheria Ndogo nne (4) zilizokuwa na hoja saba (7);

(c) Wizara ya Afya iliyokuwa na Sheria Ndogo Mbili ambazo zilibainika kuwa na jumla ya hoja tisa (9);

(d) Wizara ya Nishati iliyohusika na Sheria Ndogo tatu zenye hoja tano (5);

(e) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliyohusika na Sheria Ndogo moja (1) ambayo ilikuwa na hoja sita (6);

(f) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliyohusika na Sheria Ndogo nne (4) zenye hoja kumi na moja (11); na

(g) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyokuwa na Sheria Ndogo tatu (3) zenye hoja sita (6).

**Mheshimiwa Spika,** Taswira halisi ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inabainishwa katika **Kiambatisho Na. 1** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita, na Mkutano wa Saba). Jedwali hilo ambalo ni

sehemu ya Taarifa hii linafafanua hatua iliyofikiwa na kila Wizara. Pamoja na hivyo, kwa madhumuni ya kuweka mtiririko unaowezesha majadiliano juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:

**2.1.1 Hatua ya Kutotekeleza Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini Kutotekelezwa kwa sehemu ya Maazimio ya Bunge, ambapo baadhi ya Wizara zimeandaa Marekebisho ya Sheria Ndogo ambazo yamefika katika hatua mbalimbali pasipo kuzingatia maazimio yaliyotolewa na Bunge. Wizara zilizobainika kuwa katika hatua hii ni:-

(a) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara;
(b) Wizara ya Afya;
(c) Wizara ya Fedha na Mipango; na
(d) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Maazimio ambayo hayajatekelezwa yanafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii na yapo katika Sheria Ndogo zifuatazo: -

(a) *The Standards (Cooperation in Execution of Powers and Functions) Regulations* (TS. Na. 680 24/09/2021);

(b) *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021 (TS Na. 685 24/9/2021);*

(c) *The Mining (Government Minerals Warehouse) Regulations (TS Na. 58 28/01/2022);* na

(d) *The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020 (TS Na. 795 3/12/2021).*

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya kutotekeleza Maazimio ya Bunge inaweza kuwa na taswira ya kutokuyapa uzito Maazimio ya

Bunge. Hatua ya kutotekeleza maazimio ni kufifisha dhamira ya Bunge ya kuondoa dosari katika Sheria Ndogo zinazohusika hivyo kuendeleza dosari hizo ambazo zinasababisha changamoto.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa changamoto inayoendelea kutokana na kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge ipo Sheria Ndogo ya *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021 (TS Na. 685 24/9/2021)*. **Kanuni ya 22(2)** ya Sheria Ndogo hizi, inaonesha kuwa iwapo sampuli zilizochukuliwa kwa lengo la kufanyiwa uhakiki na kubainika hazina madhara zitagawiwa kama msaada kwa taasisi za umma na vituo vya afya. Bunge liliona kuwa, masharti ya Kanuni hizi hayaoneshi uwezekano wa sampuli hizo kurejeshwa kwa mzalishaji au msambazaji ili aendelee na utaratibu wa kuzifanyia biashara kama alivyokusudia.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge hili liliazimia dosari hiyo irekebishwe ili kuonesha utaratibu wa kurejesha kwa mmiliki sampuli zilizohakikiwa na kubainika hazina madhara kwa matumizi. Kwa minajili hiyo, kutokuwepo kwa hatua yoyote ya utekelezaji wa azimio hili kunaendeleza kero kwa walengwa, jambo ambalo Bunge haliwezi kuacha dosari hiyo iendelee.

**2.2.2 Hatua ya kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho**

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho inaonesha kuwa nyuma katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Kwa maneno mengine hatua hiyo ni kwamba inaendeleza dosari zilizobainishwa na madhara yake yanaendelea kuwepo bila kuwa yamefanyiwa kazi. Jambo hili linaleta mashaka makubwa kwa Kamati kuhusu tija ya madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya kutokukamilika kwa Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ambayo chimbuko lake ni Maazimio ya Bunge inaweza kuwa na taswira kuchelewesha

utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Ikumbukwe kuwa Maazimio ya Bunge yanalenga kusimamia madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine. Hatua ya kuchelewa katika utekelezaji wa maazimio inafifisha dhamira ya Bunge ya kuondoa dosari katika Sheria Ndogo zinazohusika hivyo kuendeleza dosari hizo ambazo zinasababisha changamoto mbalimbali miongoni mwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara zilizobainika kuwa katika hatua hii ni : -

(a) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; na

(b) Wizara ya Utamuduni Sanaa na Michezo.

Dosari za Sheria Ndogo ambazo bado zipo katika hatua ya kurekebishwa zinafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 1** kwenye Sheria Ndogo zifuatazo ni:

(a) *The Tanzania Meteorological Authority (Cost Recovery on Meteorological Services) Regulations* (TS Na. 642 03/09/2021); na

(b) *The Copyright and Neighbouring Rights (Licensing and Rights to Benefit from Re-Sale), Regulations* (TS Na. 137 18/3/2022)

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa changamoto inayoendelea kutokana na kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho kuhusu Maazimio ya Bunge inayohusu eneo la kukiuka Sheria ya Mikataba. Changamoto hiyo inatokana na Sheria Ndogo ya *The Copyright and Neighbouring Rights (Licensing and Rights to Benefit from Re-Sale), Regulations 2022* iliyo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3(2) (3)** cha Sheria kilikuwa na dosari ya kuweka sharti la lazima kuwa, kabla ya kuanza

kutumika kwa Mkataba wowote ulioingiwa nchini Tanzania kati ya mwenye hakimiliki na kampuni au Taasisi, Mkataba huo utapaswa kupelekwa COSOTA, ili iupitie na kushauri, ambapo COSOTA itatoza 1% ya thamani ya Mkataba unaohusika kama gharama za huduma iliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliona kuwa, masharti ya Kanuni hii yanalazimisha kutokuanza kwa makubaliano kati ya wahusika hadi COSOTA itakapoamua, hali inaweza kutafsiriwa kuwa ni kuingilia makubaliano. Bunge hili liliazimia dosari hiyo irekebishwe ili kuondoa sharti la lazima la kuwasilisha Mkataba COSOTA kabla Mkataba unaohusika haujaanza kufanya kazi na kuonesha utaratibu wa kupitia Mkataba kwa atayetaka kufanya hivyo, ufanyike kabla ya Mkataba unaohusika haujafungwa. Aidha iliazimiwa kuwa, Kanuni iainishe muda ambao COSOTA itatumia wakati mapitio ya Mikataba inayohusika ili kuondoa uwezekano wa kuchelewesha utekelezaji wa shughuli za wanaohusika na Mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa minajili hiyo ni vema Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoa msukumo wa haraka kukamilisha Kanuni kuhusu mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vya wasanii (CMOs). Aidha, Wizara nyingine zinazohusika na hatua hii, pia ziweke msukumo kwa hatua zilizobaki ili kutekeleza maazimio ya Bunge.

### 2.2.3 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kusubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kusubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki inaonesha kufanyika juhudi za awali kurekebisha dosari. Hali hiyo ni mwelekeo wa kuepusha madhara yatokanayo na dosari hizo. Kwa kufanya hivyo, Mamlaka zinazohusika zimeanza kuzingatia maazimio ya Bunge ili kutatua changamoto. Hata hivyo, kasoro zilizobainishwa na kutolewa Maazimio na Bunge bado zingali zinaendelea kutokana na kutokufikia mwisho kwa mchakato wa

marekebisho. Kamati inaamini kuwa kazi iliyoanza itahitimishwa inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua hii ya Utekelezaji wa Maazimio inafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa. Wizara zilizohusika katika hatua hizo ni kama ifuatavyo: -

(a) Wizara ya Nishati; na

(b) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo zinazohusika katika hatua hii ni: -

(a) *The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022(TS Na. 113 4/3/2022);*

(b) *The Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, 2022* (TS Na. 15025/3/2022);

(c) Kanuni za Anwani za Makazi katika Mamlaka za Miji za Mwaka, 2022 (TS Na. 109 25/2/2022);

(d) Kanuni za Anwani za Makazi katika Mamlaka za Wilaya, 2022 (TS Na. 110 25/2/2022);

(e) Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 (TS. Na. 127 4/3/2022); na

(f) Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 (TS Na. 128 4/3/2022).

**Mheshimiwa Spika,** hatua iliyofikiwa na Wizara zinazohusika bado haijatatua changamoto zilizobainishwa. Mfano wa **Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 (TS Na. 128 4/3/2022)** ambayo chini ya

Kifungu cha 3(1) (a) iliweka sharti kuwa mfugaji anayefuga ndani ya Halmashauri atapaswa kufuga mifugo kwa idadi itakayoamuliwa na Halmashauri. Azimio la Bunge lililenga kufuta uwezo wa Halmashauri kuamua kuhusu idadi ya mifugo itakayofugwa na mtu anayeishi ndani ya eneo la Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa azimio la Bunge ulilenga kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza kwa Halmashauri kuamua idadi ya mifugo watakayopaswa kufugwa. Hivyo hatua iliyofikiwa katika kutekeleza Maazimio ya Bunge inaendeleza changamoto zilizobainishwa katika Sheria Ndogo.

**2.2.4 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki**

**Mheshimiwa Spika,** kufikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ni kiashiria cha hatua muhimu. Hatua hiyo inaonesha nia ya kuzingatia maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa changamoto mbalimbali zilizobainishwa katika Sheria Ndogo zinazohusika. Wizara zilizofikia hatua hiyo ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika Sheria Ndogo zifuatazo:-

(a) *The Tanzania Meteorological Authority (Complaints Handling Procedures) Regulations, 2021* (TS Na. 643 3 Septemba, 2021); na

(b) *The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020* (TS Na. 795 3/12/2021).

**Mheshimiwa Spika,** Kuwasilishwa kwa Rasimu ya Marekebisho ili ihakikiwe ni hatua ya pili kuelekea kutimiza azimio la Bunge kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo yenye lengo la kuondoa dosari. Mfano wa dosari iliyotolewa azimio na ambayo utaratibu umefikia hatua hii ni kuhusu sharti kwa mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri binafsi wa kukodi

kuhakikisha kwamba, utoaji huo wa huduma hauingilii huduma ya mabasi ya daladala lililowekwa chini ya **Sheria Ndogo ya *The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020* (TS Na. 795 3/12/2021).**

**Mheshimiwa Spika,** Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hii lilikuwa ni kuitaka mamlaka inayohusika ifanyiwe marekebisho kwa kuweka tafsiri ya neno "*interfere*" kwa lengo la kuondoa utata unaoweza kujitokeza kuhusu mantiki ya neno "kuingilia". Hivyo, hatua iliyofikiwa iwapo ikikamilika itaondoa mkanganyiko wa tafsiri ya kuingilia huduma ya vyombo vya usafiri wa umma.

**2.2.5 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** kukamilisha Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na inayosubiri Namba ya Tangazo la Serikali ni hatua ya juu kabla ya kuchapishwa kwa marekebisho yatokanayo na utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Ingawa inaonekana ni hatua iliyochelewa kwa kiasi fulani, lakini ni utekelezaji na uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge unaoelekea kuondosha dosari na madhara yatokanayo na dosari hizo. Wizara zilizofikia hatua hiyo ya utekelezaji ni Wizara ya Afya, yenye Sheria Ndogo zinazorekebishwa ambazo ni:-

(a) *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021* (TS Na. 685 24/9/2021); na

(b) *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Fees and Charges) Regulations, 2021* (TS Na. 686 /24/9/ 2021).

**Mheshimiwa Spika,** Hatua iliyofikiwa na Wizara hiyo kwenye Sheria Ndogo zinazohusika, inafanikisha dhamira ya Bunge kuondoa dosari katika Sheria Ndogo. Lengo ni kuondoa changamoto inayoweza kusababishwa na Sheria Ndogo

katika hali halisi ya utekelezaji. Kwa mfano wa changamoto inayogusa hali halisi ambayo imetatuliwa kutokana na hatua ya marekebisho iliyofikiwa na Wizara ya Afya katika Sheria Ndogo ya ***The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021*** **(TS Na. 685 24/9/2021).**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo hizo zilikuwa na dosari ya kuvuka mipaka iliyowekwa na Sheria Mama. Kanuni ya 2 ilionesha mipaka ya TMDA kufikia uwekaji wa utaratibu wa namna ya kuendesha shughuli za uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama. Bunge hili liliazimia dosari hiyo irekebishwe kwa kuwa jukumu la kushughulikia uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama lililowekwa katika Kanuni hizo ni kinyume na lengo la Sheria Mama ambalo ni udhibiti wa dawa, vifaa tiba, dawa za asili pamoja na sumu.

**Mheshimiwa Spika,** hatua ya utekelezaji wa azimio hili iwapo itakamilika itaboresha Kanuni hizi ili kuendana na Majukumu ya TMDA yaliyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Hata hivyo, matokeo ya utekelezaji wa Azimio la Bunge yangekuwa na manufaa makubwa zaidi iwapo mamlaka zinazohusika zingekuwa zimekamilisha hatua hiyo mapema.

**2.2.6 Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho ya Sheria Ndogo Kutangazwa katika Gazeti la Serikali ni hatua iliyokamilishwa na Mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo hizo. Kwa ujumla hatua hii ni ya juu ya uzingatiaji wa maazimio ya Bunge. Kwa kufanya hivyo, mamlaka zinazohusika zimeweka juhudi katika usahihishaji wa dosari zilizobainishwa. Kwa kufanya hivyo madhara ya dosari hizo yameondoshwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara zilizofikia hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali ni:-

(a) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara;

(b) Wizara ya Nishati;

(c) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; na

(d) Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo zinazohusika katika hatua hii ni: -

(a) *The Standards (Imports Registration and Batch Certification) Regulations, 2021* (TS Na. 681 24 Septemba, 2021);

(b) *The Standards (Recall, Seizure and Disposal of Product) Regulations, 2021* (TS Na. 682 24 Septemba, 2021);

(c) *The Tanzania Shipping Agencies (Performance Benchmarks) Regulations, 2022* (TS Na. 116 4/3/2022);

(d) *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) Rules* (TS Na. 57 28/01/2022);

(e) *The Banking and Financial Institutions (Development Finance) Regulations (TS. Na. 766 29/10/2021);*

(f) *The Mining (Government Minerals Warehouse) Regulations (TS Na.58 28/01/2022);*

(g) *The Tax Administration (Administration of Tax Ombudsman Services) Regulations (TS Na. 105 05/02/2022);* na

(h) *The Tax Administration (Tax Ombudsman Services Complaint Procedures) Regulations (TS Na. 106 25/02/2022)*.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa dosari ambayo imeondoshwa kutokana na kutekelezwa kwa azimio la Bunge kwa hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ni dosari za Sheria Ndogo ya ***The Standards (Recall, Seizure and Disposal of Product) Regulations, 2021*** **(TS Na. 682 24 Septemba, 2021).** Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hizi lililenga kuondoa kasoro ya kutooneshwa utaratibu wa kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa ambazo hazina viwango na kwamba, kutooneshwa kwa utaratibu huo, kungeliweza kusababisha kuendelea kusambaa zaidi kwa bidhaa zisizofaa pasipo kufahamika katika jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imetekeleza azimio la Bunge kwa kuongeza **Kanuni 4 (3) (b)** inayoweka utaratibu wa namna ya kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa zisizokidhi viwango. Marekebisho haya yanawezesha utekelezaji wa madhumuni ya usimamizi wa viwango na ubora wa bidhaa na huduma yaliyowekwa na Sheria Mama iliyotungwa na Bunge. Vilevile, marekebisho yaliyofanyika yatasaidia umma wa watanzania kupata taarifa kuhusu bidhaa zisizokidhi viwango ambazo wanazitumia katika maisha ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti ambayo imefikiwa na Wizara zinazohusika ni mwitikio mzuri wa maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa changamoto zilizobainishwa katika Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Ufafanuzi huo kuhusu hatua za utekelezaji wa Maazimio, umeonesha taswira halisi ya hatua mbalimbali zilizofikiwa na mamlaka zinazohusika. Taswira hiyo italiwezesha Bunge hili kujadili na kutafakari na hatimaye kuazimia kwa kuzingatia matokeo ya tathmini kuhusu kila hatua ya utekelezaji iliyofikiwa.

### 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa

### 2.3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na nyongeza zake zikiwemo jumla ya Sheria Ndogo mia moja hamsini na nane (158). Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo yanabainisha jumla ya Sheria Ndogo Thelathini na Moja (31) kuwa na dosari mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa urahisi wa kufuatilia dosari hizo, Taarifa hii imeambatisha Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa ambalo ni **Kiambatisho Na. 2.** Naomba Majedwali yote yaliyoambatishwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ili kuweka kumbukumbu za mtiririko mzuri wa mchakato wa udhibiti wa Sheria Ndogo zilizochambuliwa.

### 2.3.2 Mchanganuo wa Dosari zilizobainika

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inaonesha mchanganuo wa Sheria Ndogo pamoja na dosari ambapo baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari zaidi ya moja. Kwa sababu hiyo, jumla ya idadi ya Sheria Ndogo 31 zilizochambuliwa inaweza isifikiwe kwa kujumlisha idadi katika mchanganuo huo. Kwa ujumla, mchanganuo wa dosari hizo unaonesha kuwa: -

(a) Jumla ya Sheria Ndogo Kumi na Tatu zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(b) Jumla ya Sheria Ndogo Kumi zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi;

(c) Jumla ya Sheria Ndogo Ishirini na Saba zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi. Makosa hayo nia

kama vile kutorejea vifungu sahihi, kurejea vifungu ambavyo havipo, kutokukamilika kwa Sheria Ndogo kwa kutokuepo kwa baadhi ya vipengele muhimu vya kisheria ili kukamilisha sheria husika;

(d) Jumla ya Sheria Ndogo Kumi na Mbili zinaweka masharti yasiyo na uhalisia ambayo yataleta changamoto katika utekelezaji wake; na

(e) Sheria Ndogo Kumi na Tano zina makosa ya maudhui ya majedwali kutofautiana na vifungu vinavyoyaanzisha au makosa ya kutokukamilika kwa majedwali au kuanzishwa kwa majedwali yasiyokuwepo ama kukosekana kwa majedwali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge lako, mifano ya dosari zilizobainika katika Sheria Ndogo zilizochambuliwa inafafanuliwa kwenye aya za 2.3.3 - 2.3.7 zinazofuata.

**2.3.3 Dosari ya Kukinzana na Masharti ya Katiba**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo hutungwa kwa madhumuni ya kufanikisha lengo kuu la Sheria Mama. Aidha, Sheria Ndogo zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni sheria Kuu ya nchi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zilikuwa na maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba. Kwa mfano, **Kifungu cha 5 (5) cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022 (TS Na. 586 30/09/2022)** kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo lolote na muda wowote kwa lengo la kukusanya ada au ushuru.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka anayopewa afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo muda wowote usio na kikomo cha ndani ya muda wa kazi yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki

ya msingi ya faragha. Hali hiyo inasababisha kero kwa wananchi wanaowakilishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** mfano mwingine wa Sheria Ndogo iliyo na masharti yanayokinzana na Katiba **ni Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022, (TS Na. 219 15/04/2022).** Kifungu cha 4(1) (a) cha Sheria Ndogo hii, pamoja na mambo mengine kinaweka sharti kwa mtu anayetaka kufanya shughuli ya kilimo ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri. Masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi yana muonekano usiofaa kwa umma kwa kuondoa mnyumbuko wa shughuli za kilimo. Hii ni kutokana na kuwabana wananchi ili watekeleze shughuli za kilimo zilizopangwa na halmashauri, na matokeo yake kukiuka **Ibara ya 8(1)** ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inayolinda ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa Bunge litaruhusu utaratibu unaowekwa na Kanuni hizo, basi litakuwa linabariki uvunjaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo chini ya **Ibara ya 16 (1)** ya Katiba ambayo imeelekeza bayana kuwa kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake na maisha yake binafsi na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake, na **Ibara ya 8(1) (b)** inayotambua lengo kuu la Serikali kuwa ni ustawi wa wananchi. Hivyo, Sheria Ndogo haipaswi kukinzana na Katiba ya nchi ambayo ni Sheria mama ya Sheria zote na hivyo iwapo Sheria Ndogo itakinzana na Katiba basi Sheria Ndogo hiyo inakuwa ni batili.

### 2.3.4 Dosari ya Kukinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za nchi

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo hutungwa ili kufafanua au kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Sheria Mama inayoanzisha Sheria Ndogo inayohusika. Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa, umebaini kasoro ya Sheria Ndogo kuwa na

maudhui yanayokinzana na Sheria Mama. Mfano wa Sheria Ndogo yenye maudhui hayo, ni ***The Merchant Shipping (Maritime Labour), Regulations 2022*** **(TS Na. 228 22 Aprili 2022). Kanuni ya 83** inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna Kanuni mahsusi inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola za marekani 500 au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja. Wakati huo huo sheria mama chini ya **Kifungu cha 401,** imeweka adhabu ya jumla iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo kuwa atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenye thamani ya dola za kimarekani 1000 au kifungo cha muda usiopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu iliyowekwa na Sheria Mama ambapo, kukinzana huko ni kwenye kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama na adhabu ya kifungo inayowekwa na Sheria Ndogo ni kubwa kuliko iliyowekwa katika Sheria Mama.

**Mheshimiwa Spika,** ni matarajio ya Bunge kuwa, Mamlaka za Serikali zilizokasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, zitunge sheria hizo kwa kuendana na matakwa ya Sheria Mama zilizotungwa na Bunge. Inapotokea Sheria Ndogo imeweka masharti yanayokinzana na Sheria Mama, kamwe Bunge haliwezi kufumbia macho dosari hiyo kwakuwa, inaweza kufifisha lengo lililokusudiwa na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi zilizotungwa na Bunge.

### 2.3.5 Dosari ya Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Sheria za Bunge huandikwa kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa Sheria. Misingi hiyo

huwezesha kuweka mawazo ghafi katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana katika masharti ya sheria inayohusika. Bunge hili, huzingatia misingi hiyo kutokana na kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Nchini. Hivyo, Sheria Ndogo pia zinatarajiwa kuzingatia ipasavyo misingi ya uandishi wa sheria nchini. Lakini, kutokana na uchambuzi wa kina, Sheria Ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa Sheria Ndogo yenye dosari hii ni **Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022, (TS Na. 217 15 Aprili 2022), Kifungu cha 8** kinachohusu muda wa kusafirisha mazao kinaonesha mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 12:00 asubuhi. Kifungu kimekosa ukamilifu wa sentensi, hivyo hakipo wazi kuhusu muda uliotajwa iwapo ni wa kusafirisha au unaokataza kusafirisha. Kutokukamilika kwa sentensi na maelezo kuhusu muda wa kusafirisha mazao kunatatanisha masharti hayo kuhusu muda.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo nyingine yenye dosari kutoendana na misingi bora ya uandishi ni ***The Banking and Financial Institutions (Mortgage Refinance Companies) Regulations, 2022*. (TS Na. 559 16 Septemba 2022). Kanuni ya 6(3) (b)** inaweka kiwango cha ada ya usajili ya shilingi milioni tano au kiwango kingine kitakachoamuliwa na Benki Kuu, kwa mtu anayetaka kuanza biashara ya *mortgage re – financing*. Kanuni imetoa mwanya kwa Benki Kuu kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua. Kiasi hicho kilichotajwa hakifafanui ukomo wa chini wala wa juu.

**Mheshimiwa Spika,** Hali hiyo inaweza kusababisha kutoeleweka kwa ada halisi ya usajili, uwezekano wa uwepo wa viwango mbalimbali vya ada ya usajili na kuleta mkanganyiko kwa watekelezaji wa kanuni hizi. Hii pia ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayotaka

Sheria Ndogo yeyote inayotaja viwango vya ada na tozo kuainisha viwango kwa namna ambayo haitaleta utata katika utafsiri wake.

**2.3.6 Dosari ya Kukosa Uhalisia**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mambo mengine, Utungaji mzuri wa Sheria huzingatia uhalisia wa utekelezaji wa sheria inayohusika. Mojawapo ya mambo ya uhalisia yanayozingatiwa ni hali halisi ya walengwa wa sheria inayohusika. Lakini uchambuzi wa Kamati umebaini Sheria Ndogo kuwa na changamoto ya kuwa na masharti yasiyo na uhalisia. Kwa mfano, **Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022, (TS Na. 216 15 Aprili 2022) Kifungu cha 14(3)** cha Sheria Ndogo hizo kinachukulia kosa la abiria kutupa takataka nje ya chombo cha usafiri, limetendwa na mmiliki au dereva au kondakta wa chombo hicho. Kifungu hicho kinafafanua kuwa, mtendaji wa kosa hilo atalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uhalisia adhabu hulenga kumuadhibu mtenda kosa na kuwaogofya wengine wasitende kosa. Kwa namna ilivyoelezwa adhabu katika Kifungu cha 14 (3), mtenda kosa halisi ni msafiri aliyetupa taka nje ya chombo cha usafiri, lakini anayeadhibiwa ni mmiliki au dereva au kondakta wa chombo kinachohusika. Hali hiyo, inaonesha lengo la adhabu halimgusi mlengwa wala haliogofyi watu wengine kutenda kosa kwa kuwa watakaoadhibiwa sio watendaji wa kosa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile sharti la adhabu lililowekwa katika Kifungu cha 14 (3) linasababisha usumbufu kwa wasiotenda kosa linalohusika. Kwa namna hiyo, Sheria Ndogo hiyo imeweka adhabu kwa masharti yasiyozingatia uhalisia katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

**Mheshimiwa Spika,** dosari ya kukosa uhalisia pia imebainika katika **Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, 2022 (TS Na. 605 21 Oktoba 2022). Kifungu cha cha 8 (2)** kinaeleza kwamba, itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi. Aidha Kifungu kidogo cha (3) kinaeleza kuwa mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini baada ya kujaziwa fomu ya ilani na afisa mwidhiniwa wa Mji endapo abiria aliyeko ndani ya gari lake atatupa uchafu katika barabara au kituo cha mabasi.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu hiki kinawapa adhabu watu kwa makosa ya wengine. Wanaoadhibiwa hawana namna ya kumzuia mkosaji halisi na wala sio waliomshawishi mkosaji kutenda kosa. Hali hiyo haitimizi lengo la kuzuia kosa kurudiwa na mfanyaji wa kosa wala mtu mwingine kwa sababu atakaye adhibiwa siye mtenda kosa.

**2.3.7 Dosari za Uandishi wa Majedwali**

**Mheshimiwa Spika,** uwepo wa Majedwali katika Sheria yeyote hulenga katika kutimiza malengo yaliyokusudiwa na kifungu cha Sheria inayohusika, hivyo ni matarajio ya msomaji wa Sheria ya kuwa Majedwali ndani ya sheria kuendana na matakwa ya kifungu wezeshi. Kukiuka lolote kati ya haya katika uandishi wa Majedwali ni makosa.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa Sheria Ndogo yenye dosari hizo ni **Sheria Ndogo (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Bunda, 2022, (TS Na. 375/ 27 Mei 2022).** Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi linaonesha kuwa limetokana na Kifungu cha 25 linahusu ada ya ukaguzi wa afya. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika. Hata hivyo, Jedwali la Kwanza linarejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 25 ambacho maudhui yake hayahusiani na Jedwali hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kawaida uandishi wa Majedwali katika sheria unalenga kutoa ufafanuzi wa ziada wa maudhui yaliyo katika vifungu. Kwa msingi huo, kutokuandika majedwali kwa ufasaha kunasababisha mkanganyiko katika usomaji wa sheria na unaoweza kuathiri malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano mwingine wa makosa katika Majedwali umeonekana katika **Sheria Ndogo za Ada na Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022 (TS Na. 560/ 16/09/2022).** Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi linarejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 4(2) ambayo maudhui yake hayahusiani na Jedwali hilo. Urejeaji wa kanuni isiyoendana kimaudhui unakiuka matakwa yaliyowekwa na Kifungu cha 11 (3) Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayoelekeza urejeaji sahihi wa vifungu katika Majedwali. Hali hii inaleta ugumu wa kueleweka kwa masharti ya kanuni na utekelezaji wa Sheria Mama.

**Mheshimiwa Spika,** Ili tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine ipatikane, matokeo ya matumizi ya madaraka hayo, yanapaswa kuzingatia dhamira ya Bunge katika Sheria Mama.

**2.4 Majumuisho kuhusu yatokanayo na Shughuli zilizotekelezwa**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla shughuli zilizotekelezwa na Kamati zilitokana na misingi ya majukumu ya Kamati kuanzia masharti ya Katiba, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Kanuni za Bunge. Shughuli hizo zililenga kulisaidia Bunge katika wajibu wake wa Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo. Mambo yaliyobainika kutokana na Shughuli hizo ni pamoja na dosari katika maeneo matano ya Sheria Ndogo. Maeneo hayo yanahusu kutokuendana na masharti ya Katiba, kukinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za nchi na Kutozingatia misingi ya Uandishi bora wa Sheria. Mengine ni

kutokuzingatia uhalisia pamoja na makosa katika uandishi wa majedwali.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo hayo yanaonesha athari hasi katika utaratibu wa Bunge kukasimu kwa mtu au Mamlaka nyingine kutunga kanuni kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 97 (5) ya Katiba. Hali hiyo inalihitaji Bunge kusema jambo linaloweza kuondoa athari hiyo. Aidha, athari nyingine hasi inatokana na kubainika kwa hatua za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zinazoweza kuainishwa katika makundi matano kulingana na athari zake. Makundi hayo ni: -

(a) Hatua ya kutotekeleza Maazimio ya Bunge;

(b) Hatua ambayo Rasimu ya Marekebisho haijakamilika;

(c) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki;

(d) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;

(e) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali; na

(f) Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua nzuri na ya kupongezwa ni ile ya kukamilisha marekebisho na kutangazwa katika Gazeti la Serikali, kwa sababu hatua hiyo inajielekeza kwenye kuondoa hitilafu zilizobainishwa. Kundi hili linahusu baadhi ya Sheria Ndogo za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nishati.

**Mheshimiwa Spika,** Kundi jingine linajumuisha hatua za Utekelezaji uliochelewa ambazo nayo inarekebisha hitilafu zilizobainika lakini kwa kuchelewa. Hatua hizo si mbaya ingawa ingelifaa kukamilisha mapema ili kupunguza muda wa athari hasi za dosari zilizobainishwa. Wizara zilizofikia hatua hizo ni:-

(a) Wizara ya Afya, iliyofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali;

(b) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, iliyofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;

(c) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iliyofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki; na

(d) Wizara za Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambazo bado zinaendelea kukamilisha mchakato wa Rasimu ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika baadhi ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** kundi la mwisho linahusu Wizara ambazo hazijatekeleza Maazimio ya Bunge katika baadhi ya Sheria Ndogo. Wizara hizo ni Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Mipango; na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Kutokutekelezwa kwa maazimio kunaendeleza changamoto ambazo Bunge limeziona katika Sheria Ndogo mbalimbali hivyo kushindwa kutatua kero zilizokusudiwa kuondolewa na Bunge.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 136 (15)** ya Kanuni za Bunge, inaweka ulazima wa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bunge la Bajeti. Nia ya utaratibu huu wa kikanuni ni kuliwezesha Bunge kujadili na kutoa uamuzi juu ya shughuli hizo kama zinavyoelekezwa na Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo imepewa majukumu ya kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria inayotekelezwa na Sheria Ndogo husika pamoja na sheria nyingine za nchi ili kusimamia adhma ya matumizi sahihi ya madaraka ya Bunge ya kutunga sheria iliyokasimisha kwa mamlaka nyingine, mjadala wa taarifa hii unahitaji umakini wa hali ya juu ili kufanikisha lengo lilikusudiwa na Bunge wakati linakasimisha madaraka yake kwa mtu au mamlaka zingine. Aidha, ikizingatiwa kuwa Sheria Ndogo hugusa maisha ya wananchi moja kwa moja katika utekelezaji wake, ninaliomba Bunge lako lipokee mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na kuifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili Taarifa hii iweze kuwa na mantiki inayoendana na uchambuzi na mapendekezo naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaotokana na uchambuzi. Kwa ufupi mtazamo huo upo kwenye mambo saba kama ifuatavyo:-

#### 3.1.1 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika,** Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na Katiba ya Nchi ni dosari kubwa inayoitoa Sheria hiyo nje ya Misingi ya Utungaji wa Sheria. Kamati ina maoni kwamba, Bunge ambalo ni Mamlaka ya kutunga Sheria, halipaswi

kuruhusu Madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa Mamlaka nyingine yatumike kinyume na misingi ambayo lenyewe, halipaswi na haliwezi kuikiuka.

### 3.1.2 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi

**Mheshimiwa Spika**, Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na Masharti ya Sheria Mama haipaswi kuendelea kuwepo. Dosari hiyo inavuka madaraka yaliyokabidhiwa kwa mamlaka inayohusika na vilevile, ni kinyume na matarajio ya Bunge ambalo limepewa mamlaka yote ya kutunga Sheria za nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa, kuendelea kutumika kwa Sheria Ndogo hizo, si jambo jema kwa desturi na misingi ya Sheria.

### 3.1.3 Sheria Ndogo kutozingatia Misingi ya Uandishi bora wa Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Bunge hutunga Sheria kwa kuzingatia uandishi ulio bora ili kuwezesha malengo iliyoyakusudia katika Sheria inayohusika. Ni maoni ya Kamati kwamba, kutungwa kwa Sheria Ndogo zinazotofautina na misingi ya uandishi bora wa sheria ni jambo lisiloendana na matarajio ya Bunge na linapaswa kurekebishwa inavyostahili.

### 3.1.4 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yasiyozingatia Uhalisia

**Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo zenye Masharti yasiyozingatia uhalisia zinaweza kukwamisha malengo ya Bunge kutunga Sheria Mama inayohusika. Ni maoni ya Kamati kuwa, zaidi ya kukwamisha malengo ya Sheria Mama, Sheria Ndogo zenye dosari hiyo zinaweza kusababisha kero kwa Wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kuona madaraka yake yanayokabidhiwa kwa mamlaka nyingine hayatumiki kusababisha kero kwa wananchi.

### 3.1.5 Sheria Ndogo kukosa Usahihi na Ufasaha katika Uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika,** Dosari ya Sheria Ndogo kukosa usahihi inaathiri ukamifu wa ufafanuzi wa Sheria ya Bunge uliotarajiwa kutolewa kupitia Sheria Ndogo. Ni maoni ya Kamati kwamba, Sheria Ndogo zilizokosa usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali zinatatiza ufafanuzi uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizohusika. Kwa msingi huo, Bunge linatarajiwa kuonesha hatua zinazostahili ili kurekebisha dosari hizo.

### 3.1.6 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio yanayohusu Kurekebisha Sheria Ndogo

**Mheshimimiwa Spika,** Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika Sheria Ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kero kwa wananchi. Bunge ambalo ni sauti ya wananchi halipaswi kutokusema chochote inapotokea dosari hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa kuchelewa kutekeleza maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za Sheria Ndogo, ni jambo linalochelewesha utatuzi wa kero za wananchi pale ambapo dosari hizo zinasababisha kero kwa watu.

### 3.1.7 Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mambo mengine Maazimio ya Bunge hutolewa kwa lengo la kuelekeza utekelezaji wa jambo fulani ambalo Bunge limeshughulikia na kutoa uamuzi, ikiwemo Maazimio kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo. Ni maoni ya Kamati kuwa, kutokuzingatia Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ni jambo linalokumbatia dosari zilizolengwa kurekebishwa. Bunge ambalo ndilo Mamlaka kuu ya Utungaji wa Sheria halitarajiwi kuunga mkono desturi ya mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kutunga Sheria Ndogo kuendelea kukumbatia dosari za Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kujumuisha maoni ya Kamati, naomba kulikumbusha Bunge hili kuwa dosari zilizobainika

zinaathiri tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kuweka kanuni kwa mamlaka nyingine. Athari hizo ni pamoja na kuweka ugumu wa kueleweka kwa sheria na kusababisha kero kwa wananchi kutokana na hitilafu kwenye Sheria Ndogo. Madhara mengine ya dosari hizo ni uwezekano hafifu wa kutimia kwa lengo la baadhi ya Sheria zilizotungwa na Bunge na kuendelea kwa desturi isiyofaa katika utaratibu wa Sheria za nchi. Mambo hayo yanahitaji hatua za haraka za marekebisho na hasa kwa kuwa Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maslahi ya wananchi katika utekelezaji wa shughuli za umma. Hali hiyo ndio hasa msingi wa mapendekezo ya maazimio ya Bunge katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile kuchelewa kutekeleza Maazimio ya Bunge yanayohusu marekebisho ya dosari za Sheria Ndogo ni jambo lenye madhara kwenye nia ya Bunge kukasimu mamlaka nyingine uwezo wa kufafanua Sheria Kuu kupitia Sheria Ndogo. Madhara hayo ni pamoja na kuendeleza kero kwa wananchi licha ya kuwa zimebainishwa na chombo chao cha Uwakilishi. Aidha, hali hiyo inasababisha kuendeleza hitilafu ambazo Bunge ambalo ni chombo kikuu cha Utungaji wa Sheria nchini lisingeliweza na kamwe halitarajiwi kudumisha hitilafu hizo pale zinapobainikana. Kwa sababu hiyo Taarifa hii inajumuisha Mapendekezo ya Maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa hitilafu hizo.

**3.2 Mapendekezo**

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Mapendekezo ya Kamati ni maoni yake yaliyotokana na shughuli kubwa mbili. Shughuli hizo nilizitaja kuwa ni Uchambuzi wa Sheria Ndogo na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kutokana na Maoni ya Kamati kuhusu dosari zilizojitokeza katika Sheria Ndogo, Kamati inapendekeza mambo saba kwa njia ya hoja kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.2.1 Kukinzana na Masharti ya Katiba

**KWA KUWA,** baadhi ya Sheria Ndogo zimebainika kukinzana na masharti ya katiba, suala ambalo ni kinyume na misingi ya sheria inayotambua Ukuu wa Katiba,

**NA KWA KUWA,** ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa sheria yoyote ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti itakua ni batili,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanyiwe marekebisho ndani ya siku sitini kwa ajili ya kutatua dosari hiyo.

### 3.2.2 Kukinzana na Masharti ya Sheria inayotoa Mamlaka ya Kutungwa kwa Sheria Ndogo au Sheria nyingine za Nchi

**KWA KUWA,** baadhi ya Sheria Ndogo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria Mama inayohusika,

**NA KWA KUWA,** Kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria Ndogo inayokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi ni batili kwa kiwango cha dosari hiyo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zenye kukinzana na masharti ya Sheria mama na Sheria nyingine za nchi, zirekebishe Sheria Ndogo hizo ndani ya siku sitini ili kuondoa dosari hiyo.

### 3.2.3 Kutozingatia Misingi ya Uandishi Bora wa Sheria

**KWA KUWA,** baadhi ya Sheria Ndogo zilibainika kutokuzingatia misingi ya uandishi bora wa sheria,

**NA KWA KUWA,** Dosari ya uandishi bora wa Sheria inaweza kuharibu urahisi wa kusomeka kwa Sheria Ndogo, jambo ambalo halina msaada kwa nia ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zinazohusika,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zilizo kutwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ndani ya sitini kuanzia leo ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo.

### 3.2.4 Masharti Yasiyo na Uhalisia

**KWA KUWA,** dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia imebainika katika baadhi ya Sheria Ndogo, jambo linaloweza kuchangia ugumu wa utekelezaji,

**NA KWA KUWA,** Athari ya ugumu katika utekelezaji wa Sheria Ndogo ni jambo linalovuruga upatikanaji wa tija ya Sheria Ndogo hizo na kuondoa maana ya madhumuni ya kukasimu madaraka ya Bunge kutunga Sheria,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo, ili kuendana na uhalisia na kurahisisha utekelezaji wake.

### 3.2.5 Dosari ya Uandishi wa Majedwali

**KWA KUWA,** Majedwali ni sehemu ya ufafanuzi wa Sheria uliolenga kurahisisha uelewa na kutoa ufafanuzi wa vifungu vya Sheria,

**NA KWA KUWA,** baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari ya uandishi wa Majedwali hali inayosababisha changamoto katika utekelezaji vifungu vya Sheria Ndogo inayohusika,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo na kubainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo.

### 3.2.6 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo

**KWA KUWA,** Baadhi ya Mamlaka zimechelewa kutekeleza maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo, jambo ambalo linaendeleza dosari zilizokuwa zimebainika wakati wa uchambuzi,

**NA KWA KUWA,** kuchelewa huko kunasababisha kuendelea kuwa na Sheria Ndogo zenye dosari licha ya Bunge ambalo ni Chombo kikuu cha kutunga sheria kuelekeza tofauti,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizobainika kuchelewa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

### 3.2.7 Kutokutekelezwa kwa Maazimio

**KWA KUWA,** zipo mamlaka ambazo hazijatekeleza kabisa maazimio ya Bunge kuhusu Marekebisho ya Sheria Ndogo hadi muda huu,

**NA KWA KUWA,** kutokutekelezwa kwa maazimio ya marekebisho ya Sheria Ndogo kama yalivyotolewa na Bunge ni ishara ya kuendeleza kuwabebesha mzigo wananchi wanaoguswa na Sheria Ndogo zinazohusika,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizobainika kutotekeleza maazimio ya Bunge zitekeleze Maazimio hayo ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge na hatimaye kufanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – Mwenyekiti;
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb)-Makamu Mwenyekiti;
3. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb) Mjumbe;
4. Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, (Mb) Mjumbe;
5. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb) Mjumbe;
6. Mhe. Sylvia Francis Sigula, (Mb) Mjumbe;
7. Mhe. Emmanuel Mageni Kasalali, (Mb) Mjumbe;
8. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, (Mb) Mjumbe;
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, (Mb) Mjumbe;
10. Mhe. Judith Salvio Kapinga, (Mb) Mjumbe;
11. Mhe. Santiel Erick Kirumba, (Mb) Mjumbe;
12. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb) Mjumbe;
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, (Mb) Mjumbe;
14. Mhe. Esther Edwin Malleko, (Mb) Mjumbe;

15. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb) Mjumbe;
16. Mhe. Esther Lukago Midimu, (Mb) Mjumbe;
17. Mhe. Minza Simon Mjika, (Mb) Mjumbe;
18. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb) Mjumbe;
19. Mhe. Nicholaus George Ngassa, (Mb) Mjumbe;
20. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, (Mb) Mjumbe;
21. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani,(Mb) Mjumbe;
22. Mhe. Eng.Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, (Mb) Mjumbe;
23. Mhe. Ally Yahaya Mhata, (Mb) Mjumbe;
24. Mhe. Francis Isack Mtinga, (Mb) Mjumbe; na
25. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, (Mb) Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. George Simbachawene (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika Vikao vya Uchambuzi wa Sheria Ndogo na Vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald S. Magili kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Gwantwa Alex Mwakijungu, Ndg. Emmy Peter na Ndg. Ganjatuni Kilemile

wakisaidiwa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Imelda Ntimba kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**
8 Februari, 2023

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, naona hoja yako imeungwa mkono.

Haya sasa kabla hatujaanza uchangiaji kuna tangazo muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa CCM. Wabunge Wanawake wa CCM wanatangaziwa kikao baina ya Mwenyekiti wa UWT Taifa Mheshimiwa Mary Chatanda na Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa Mheshimiwa Zainabu Shomary, kikao hicho ni pamoja na Wabunge Wanawake wa CCM leo tarehe 8 Februari, 2023 mchana, kuanzia saa saba mara baada ya Kikao hiki cha Bunge; na Ukumbi ni wa Msekwa. Hii imetolewa na Mheshimiwa Subila Mugalu kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, kila mmoja amuarifu mwenzake.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaanza na mjadala wa jumla na tutaanza na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Yahaya Massari wajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya mimi kuchangia au kutoa mawazo yangu kwenye hoja za kamati zilizowasilisha ripoti zao za mwaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Kamati ya Sheria Ndogo. Kwa hiyo zilizoko mezani ni taarifa za mwaka za kamati mbili naomba mchango wangu niuelekeze wenye Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jukumu na mamlaka ya kutunga sheria za nchi hii ni mamlaka ya Bunge. Hii ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Ibara ya 4 ikisomwa sambamba na Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake yote. Kwa hiyo, mamlaka yote ya kutunga sheria za nchi hii yako kwenye chombo hiki cha Bunge ambacho sisi tunakitumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Katiba hiyo hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikatoa mamlaka ya kukasimu madaraka hayo ya Bunge kwa vyombo visivyokuwa Bunge ili vilisaidie Bunge kutengeneza Sheria kwa ajili ya kuleta mustakabari mzuri wa maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Hiyo ipo kwenye Ibara ya 97(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu unatolewa kwenye sheria za nchi *(principal laws)*, ambapo kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria *CAP* 1 kwenye Kifungu cha 37 na 38 kinatoa utaratibu, vipi vyombo visivyokuwa Bunge vitatunga Sheria na vitapita katika utaratibu gani. Kwa hiyo, baada ya

sheria kutungwa, kwa utaratibu uliopo, sasa kwa sheria zetu ni kwamba zitaingia mtaani na zinaanza kutumika baada ya kupata sahihi za waliopewa mamlaka ya kutunga sheria; aidha mawaziri au wakurugenzi, kwa zile sheria zinazotoka kwenye taasisi, na baada ya kutangazwa kwenye gazeti rasmi la Serikali, sheria hizo zinaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo inakuja kukutana na sheria hizo wakati sheria zikiwa zimekwisha ingia mtaani na zinafanya kazi. Sasa sisi tunatekeleza wajibu wetu wa kisheria wa kuzisimamia na kuzipitia sheria hizo ili kuona kwamba tuliowakasimu madaraka hayo hawayavunji? Hawayatumii wanavyotaka wao? Huo ndio wajibu wetu namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zinavyokuja mbele yetu sisi tunazipitia halafu tunatoa mapendekezo yetu na marekebisho kwa hizo taasisi zilizotunga kanuni hizo. Kwamba tunapoona sheria hizo zimevunja aidha Katiba au sheria mama au haziendani na uhalisia, tunawambia nendeni karekebisheni au nendeni kafuteni hii wekeni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumezuka tabia ambayo si nzuri kidogo na ni lazima kama Bunge tuikemee. Maazimio ya Bunge kwa Serikali ya kurekebisha baadhi ya kanuni tunazowambia hayarekebishwi. Hilo ni jambo baya sana sana sana sana; kama taasisi hatutakiwi tuliache hata siku moja. Tuiachie Serikali wasirekebishe marekebisho tunayowapa aidha Kamati au Bunge zima linapofanya Maazimio baada ya Kamati kuleta taarifa yake ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo tumeyabaini kwamba tangu kikao cha Bunge la 5, 6, 7 mpaka leo Bunge la 10 hayajarekebishwa; bado yako mtaani na yanaumiza watu. Kuna kanuni hazifai kabisa hata kuziona, ziko mtaani na zinaumiza watu. Kwa sababu hizi kanuni tunazozipitia ndiyo maisha ya watu ya kila siku huko mtaani na wananchi wetu.

Kwa hiyo sisi tunaposema zikarekebishwe kunapita zaidi ya miezi 6, 7, 8 hazijarekebishwa hivi tunategemea nini? Ni kanuni zinaendelea kuumiza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi nataka nitoe mfano mmoja. *COSOTA* walituletea kanuni moja hivi, walikuwa na kanuni yao inaitwa *Copyright and Neighboring Right Regulation GN 137*. Kwenye kanuni yao hiyo *COSOTA* walikuwa wana kipengele kwenye Kanuni ya 3 (2) na (3); ya kwamba mikataba yote ya wasanii wa nchi hii wanayoingia aidha na taasisi au ma-*promoter* au mtu yeyote lazima mikataba hiyo ipite *COSOTA*. Sasa walivyokuja kwenye kanuni tukawauliza mnataka kutibu nini? Mbona kama vile sheria itashindwa kutekelezeka? Unataka msanii aliyeko Geita Vijijini achukue mkataba wakati Geita hakuna hata Ofisi ya *COSOTA* aulete Dar es salaam ili wewe uje uipitie wewe nani? Mnataka kutibu nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakatuambia malalamiko yamekuwa mengi sana ya wasanii kuwa wanadhulumiwa kwenye mikataba, hawajui, wanasaini mikataba wakiwa hawavijui vipengele. Kwa hiyo sisi tunataka tuwasaidie wasanii. Hata hivyo, *behind* wameweka kila mkataba watakaoupitia wata-*charge* asilimia moja ya *value* ya mkataba huo iende *COSOTA* ili wao wapate hiyo nafasi ya kutibu. Tukasema hii sio sahihi. Msanii akiona iko haja ya mkataba wake anadhulumiwa atatafuta mwanasheria. Kama ninyi *COSOTA* kama taasisi ya Serikali mnataka kusimamia msiweke ulazima, anayetaka aje, lakini si lazima. Kuna wengine wameshatoka huko wana wanasheria wao binafsi, unamlazimishaje aje *COSOTA?* kwa hiyo, toka Mkutano wa Tano jambo hilo halijarekebishwa hadi leo. Lipo hivyo na linaendelea kuumiza wasanii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria tukishasema, tukishatoa maazimio kuna tatizo lingine la kukaa muda mrefu sana kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Zinakaa kwa

muda mrefu zikisubiri uhakiki au zikisubiri zipate *GN*. Ziko sheria za tangu Mkutano wa Sita na wa Saba mpaka leo. Serikali wakija kwenye Kamati yetu tukiwauliza mmefikia wapi kwenye kurekebisha yale mliyoambiwa mrekebishe na Bunge? Wanakwambaia sheria sisi tulikwisha rekebisha zilishapata saini ya Waziri lakini hadi leo zipo kwa Mwanasheria Mkuu hazijapata *GN* au nyingine zinasubiri uhakiki. Si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kanuni za halmashauri ndogo ya hifadhi ya mazingira ya Itigi. Kanuni hizi kwa mfano zilikuja na mapendekezo kwamba mtu yeyote anayekaa kwenye Halmashauri ya Itigi anayetaka kufuga, atafuga kwa idadi ambayo halmashauri itamwambia afuge. Kwa hiyo, walivyoleta kwenye sheria yetu tukawaambia hii sio sahihi, haiwezejkani kuwa hivi. Kwa nini halmashaurri mumpangie mtu mifugo? Hata kama mnataka ku-*control* mazingira mnaweza kuweka kwenye kanuni idadi ya mifugo mnayotaka lakini si maamuzi ya Mkurugenzi au Mtu yeyote kwenye halmashauri Kwenda kusema sasa wewe ng'ombe fuga 50, wewe utafuga 30, wewe kuku fuga hivi, si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukawambia kwamba nendeni karekebisheni. Wamekuja kwenye Kamati ya Bunge hili tunauliza mmefikia wapi? Wanasema sisi tumekwisha saini rasimu ya marekebisho lakini hadi sasa rasimu hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, iko kwa Mwanasheria Mkuu haijapata *GN Number*. Hili ni jambo ambalo linaendelea kuwaumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ipo mingi sana kwa sababu zinakuja kanuni nyingi ambapo kanuni nyingine hazitekelezeki, kanuni nyingine wanaleta masharti ambayo yamepitwa wakati. Kwa hiyo ni jambo ambalo ni lazima tuchukue hatua kama Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ikishamaliza kufanya kazi yake na taarifa yake ikishasomwa ndani ya Bunge, Bunge

linatoa maazimio ya jambo hilo likarekebishwe, likafanywe; sasa wewe unakuja kwenye Kamati kuja ku-*negotiate* Maazimio ya Bunge wewe nani? Bunge lishasema nenda karekebishe, karekebishe si wakati tena wa kuja kutuambia sisi tulivyoona hii ilikuwa si sahihi. Wabunge wote hawa 396 jambo hilo baada ya kuliazimia waliona si sahihi nyie watu wawili tu wa Wizara mkalione ni sahihi kweli jamani…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhan, ahsante sana.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:…** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja kwa taarifa zote mbili. Ahasante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana Nilimtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita**,** Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa hotuba yake nzuri sana, ametuwakilisha vizuri Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni siku ya Katiba na Sheria ndogo; ni Sheria tu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vitu ambavyo nachangia leo, naanza na suala la ajira na kazi kwa sababu liko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini ni jambo ambalo limekuwa na Changamoto nyingi sana. Vijana wetu wengi wako hapa wanahangaika wakitafuta ajira. Kila Mbunge hapa kila wakati analetewa majina, *CV* za vijana wengi wakitafuta kazi. Wakati *interview* zinafanyika, aidha nafasi ni 30 wanaletwa watu hapa 4000, 5000; si, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeona wameanza kubadilisha kidogo, sasa wameanza kugawa kwa *zone,* ili kuwaondolea vijana usumbufu kuhangaika k wenda sehemu moja wako 3000, 4000 halafu nafasi ni 50 tu. Kwa hiyo, ndilo jambo moja tu ambalo nilitaka nishauri Serikali mbadilishe na mje *model* ambayo itawasaidia kuwaondolea usumbufu vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge hapa, ukisikia ajira zimetoka 10,000 hesabu za haraka haraka ni kwamba unachukua idadi ya majimbo unagawa ili walau kila Mbunge kwake kule aone vijana wake kadhaa wamepata ajira. Hilo ndilo tegemeo la kila Mbunge hapa na tunataka hivyo. Hatutaki tusikie ajira ziko 10,000 lakini ajira zinavyoenda unashangaa humuoni mtoto wa Kiteto ama kutoka jimbo lolote la Mbunge hapa; mnatugombanisha na wananchi. Kwa hiyo, tengenezeni *model* nzuri sana itakayotusaidia. Kama mnavyogawa poesa za miradi, kwa mfano kama ilivyokuwa UVIKO; mbona imewezekana na miradi imekwenda kila mahala. Tunataka kwenye ajira pia Mlete *Model* ambayo itatusaidia wote tuone kwamba tumejumuishwa na suala la ajira na Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine muanzishe, anzisheni mijadala; mnajua hatusemi hili ni la kwenu peke yenu, tuanzishe nijadala ya mara kwa mara ya namna ya kuboresha suala la ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni ofisi au idara inayoitwa ya Mpigachapa wa Serikali *(Government printer);* sijui wabunge wangapi wanafahamu hii *Government printer*; hata sisi Kamati yetu kwa mara ya kwanza tumefahamu jana zaidi baada ya kuja kutuonesha na tukaona; lakini kazi kubwa inayofanywa na idara hii ni kubwa zaidi. Inasimamia Nembo na Bendera ya Taifa inasimamia kuchapisha nyaraka za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mahakama na Bunge. Hata

bendera tulizonazo; na mwaka jana hapa tulirumbanarumbana kidogo kujua ipi bendera sahihi ya Bunge; na siku hizi vipeperushi vingi sana vipo mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ofisi hii haijawezeshwa ipasavyo Serikali imekuja na mkakati mzuri sana wa kuboresha ofisi hii ama idara ya Mpiga Chapa wa Serikali; ni Ofisi muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kwa mfano walikuwa wanatuambia kwamba, kama wangeweza kupata pesa wangeweza kuchapisha nakala milioni sita ambayo ingeweza kupatia Serikali bilioni 20. Lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti sasa hivi wanapata nakala laki sita peke yake. Kwa hiyo ni muhimu wabunge wafahamu kwamba ofisi hii muhimu sana ya Serikali inayohifadhi nyaraka na alama za Taifa letu ni muhimu iwezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP)* vilevile haipati pesa za kutosha ili iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi. Mimi nilipata nafasi ya kumtembelea *DPP* siku moja, nilishangaa sana, ofisi yake ni ya ajabu sana. Najua sasa hivi wanajenga ofisi yao; lakini ni vyema Serikali ikatenga pesa ili watu hawa wanaofanya kazi kubwa wapate kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *Law School of Tanzania*. *Law school* of Tanzania; na mimi ni mwanafunzi wa *Law School of Tanzania, first cohort*. Ukisikia mambo yanayoendelea huko wakati mwingine unasoma vijana wale wanenda kufungua kesi; mahakamani ni dhahiri kwamba kuna jambo la kufanywa na Serikali. Kwa mfano ripoti ya Dkt. Mwakyembe muilete bungeni tuangalie, tu-*interrogate* ili na sisi tuweze kushauri namna bora; na Mheshimiwa wakili msomi, Mavunde tulikuwa *cohort* moja *first cohort*; lazima, hata wewe unajua unamawazo mazuri ya namna ya

kuboresha hiyo zaidi ili vijana wetu wasisumbuliwe lakini tuwatengeneze Wanasheria wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Kamati imesema hapa labda kuna haja ya kuanzisha ile *entry exam*. Lakini sheria ile iliyounda *law school* ni kama ilimlazimisha kila mtu kwenda *Law School of Tanzania,* ambayo si sawa. Waende wale ambao wanataka kuwa mawakili. Kwa hiyo kama kuna haja ya kufanya hivyo basi ni vizuri tuangalie mifumo ile. Na pengine baadhi ya *courses*, kwa mfano Mheshimiwa Mavunde wakati tunasoma *accounting for lawyers;* sawa ni *important* lakini kwa nini, *but why do you examine me on accounting for lawyers* inanisaidia nini? Halafu baadaye inanishushia tu *grade* zangu hainisaidii chochote. Kuna *course* nyingine ni muhimu lakini ukini-*examine accounting for lawyers* kweli? Na mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lugha ya uandishi wa sheria; Bunge hili lilipitisha sheria hapa ya kusema tutumie Kiswahili, jambo ambalo ni jema sana; Watanzania wengi lazima wafuatilie, waweze kusoma sheria tunazotunga na waweze kuelewa kwa lugha hiyo. Hta hivyo kwa sababu Tanzania si kisiwa peke yake, ni vyema kama walivyoshauri Kamati, tupate sheria hizi zote kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili, Kwa sababu si kwamba sheria zetu tunazotunga zina Mahakamani peke yake bali pia zinatumika kufundisha wanafunzi; na wanafunzi wanatoka kila mahali duniani kuja kwenye Mahakama zetu na kwenye vyuo vyetu. Kwa hiyo ni muhimu sana ili tuondokane na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nitazungumzia habari za Mahakama. Hii *program* mliyoanzisha Mahakama ya-*integrated justice,* ile Mahakama Jumuisho, ni *program* nzuri sana. Siku hizi mahakama zetu unatembelea mahakama utafikiri ni hoteli kabisa. Hata ukitembelea *judiciary square* hapa naambiwa ni jingo sijui la sita ama la kumi *Southern of* Sahara, ni nzuri sana, *program* ile ni nzuri

sana. Lakini sasa tunataka haki zitoke kwenye majengo yale. Sisi hatutaki kwa sababu ni jengo refu tu, *no, challenge* sasa ni kwamba *we want justice* kutoka kwenye Mahakama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa na sheria ndogo; wakati mwingine Bunge linashauri kuhusu jinsi tunavyotafsiri sheria zetu. Hakuna kitu kibaya sana kama Serikali msipofahamu bunge lilimaanisha nini kwenye sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la mifugo, ina-*touch* hii Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na vifungu vinavyotumika kila wakati ni Kifungu cha 116 cha Sheria ya Wanyamapori kwenye ku-*compound offenses.* Kama juna eneo ambalo tunafanya hovyo kuliko yote ni kwenye *compounding of offenses*. Sheria, na Bunge lilisema hivi, *Section 116,* na ninaomba kunukuu; "*This section shall apply to offenses committed under the Act in relation to protected areas, the director may compound an offense by requiring a person to pay a sum of money provided that such money shall not be less than two hundred thousand shillings and not exceeding ten million shillings*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo Bunge lilivyosema; a person. Lakini wanakaa waswahili fulani tu kule wanaanza kuhesabu vichwa vya mifugo halafu wanasema lipa laki moja moja; *that is not the intention of the law*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili likinyamazia vitu kama hivi; na si Bunge kabisa, ni mtu mmoja bingwa tu, alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo hapa. Haya makosa yaliyogundulika takriban kanuni 31 zenye kasoro za kiuandishi zinakwenda kinyume na Katiba. Haya ni makosa tu yamegundulika kwa kusoma zile sheria, lakini wangekwenda *field* leo wakajua ni watu wangapi wameumia kwa sababu ya sheria hizo ni mbaya zaidi *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Sheria ya *TANAPA Section 20A* bado inazungumzia kwamba *fine* kama unataka ku-*compound should not exceed one hundred thousand, should not exceed;* lakini *a person pays*. Sasa, wakati Bunge linatunga sheria *definition of livestock* maana yake ni mbuzi kondoo nguruwe farasi kuku ndama hata mayai. Sasa laki moja leo ng'ombe ni wa laki moja na nusu ama laki moja halafu unataka kutoza *fine* ya shilingi laki moja utafanya Bunge hili lisiaminike hata kidogo. Lakini kumbe wala sio sisi, ni wale wanaosimamia sheria. Kwa hiyo Waheshimiwa Mawaziri muwe wakali sana. Bunge hili likisema na likishauri kanuni hii haifai ama hii *compounded* haifai ni vyema mkasimamia kwa nguvu zote ili Bunge liendelee kuheshimika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana kengere ilishalia muda mrefu.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mko hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Yahaya Massare Mheshimiwa Simaye Hassan Sadick na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi; na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa yetu ya Kamati ambayo itakuja kwenye Bunge hili. Tunaendelea kuishauri wabunge wenzetu waiunge mkono liwe Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nina jambo dogo katika suala zima la ajira. Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Ajira na

Vijana imebeba majukumu makubwa sana katika nchi hii. Suala la ajira sasa limekuwa ni mzigo kwa jamii. Vijana wetu wanasoma na wengi wamehitimu vyuo vikuu lakini nafsi za ajira eneo lililo rasmi zimekuwa ni chache sana, na hata zinapotoka zinakuwa na changamoto. Msemaji aliyetangulia Mheshimiwa Ole-Lekaita hapa amezungumzia ni namna gani bora sasa Serikali ifanye. Mimi naendelea kushauri Serikali ione namna bora ya kufanya mgawanyo wa ajira hizi, aidha kwa mikoa au kwa wilaya na hata kwa majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza mwaka 2023 hakuna jimbo ambalo halina wasomi, hakuna jimbo ambalo vijana wake wamekaa wanasubiri wamepata ajira; majimbo yote Tanzania. Hata hivyo, zinapotoka nafasi za ajira utaona tu wametoka kwenye *zone* fulani au kwenye eneo moja fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Halmashauri 184; kama nafasi zipo hata kama ni 2000 ukazigawanya kwa hizi halmashauri halafu yale majiji ambayo pengine yanapendelewa zaidi yakaongezewa na manispaa shida iko wapi? Juzi tu hapa tumeona watu wa Idara ya Polisi, wamefanya vizuri sana wamegawanya ajira zile kwa mikoa na kule mikoani wakazigawa kwa wilaya, maana yake zimegusa eneo kubwa. Je, upande wa ajira hizi za walimu na madaktari, wauguzi na maeneo mengine ya Serikali mnashindwaje kuzigawanya katika mfumo huu ambao *IGP* wa sasa aliyepata nafasi juzi ameonesha njia? Naomba sana Serikali ilione jambo hili kuwa ni la kuigwa na la mfano; ajira hizi zizingatie uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge miongoni mwetu hapa hakuna Mbunge kwa inapotoka nafasi za ajira anakosa meseji kumi au kumi na tano za watu ambao wantaka kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti ule mfumo wenyewe mimi naona kama hauko sawa, ule ambao unahusika na ajira za watu. Unaambiwa mfumo ndio unachagua, utachagua kutona miaka, lakini unakuta ameajiriwa mtu wa mbele yake wa nyuma ameachwa; na mfumo huohuo unaangalia wanasema huwa tunazingatia miaka unaangalia mtu mwenye miaka mingi ameachwa nyumbani kijana mdogo amechukuliwa. Huu mfumo nini faida yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Serikali ione changamoto hizi zinaumiza wananchi vijana wetu wanaanza kukosa imani na Serikali yao kwa sababu ya matukio kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili lisilo rasmi la kurasimisha vijana wale wanye ufundi. Hapa kulikuwa na ya wanagenzi wanaitwa na Ofisi ya Waziri Mkuu walikuwa wanarasimisha vijana wale wenye ujuzi, wanawapatiwa mafunzo kidogo na kuwapatia vyeti ili watambulike katika jamii na katika maeneo rasmi ya Serikali pengine ya ajira lakini pa waweze kupata kazi zinazotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa na faida sana; vijana wengi wamerasmishwa wanaitwa wanagenzi na sasa tunaona matokeo mazuri. Hata hivyo bado liko jambo ambalo leo, na hata jana na juzi hapa tumeona changamoto kubwa zavijana wengi ambao wanategemewa kusaidiwanaserikali yetu hii kupitia wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo. Na kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inasimamia Wizara hizi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unachukuaje mtu ambaye hakuwahi kulima? Eti unamchukua akalime, na wakulima wanaolima kila siku wapo, na vijana wa maeneo yale wapo, ardhi iko pale; kwa nini usichukue wale vijana walioko maeneo ilipo ardhi ukawawezesha kutokana na mipango yako ile kuliko kumchukua mtu ambaye maisha yake

amekuwa anaangalia katuni na bongo fleva halafu leo unamwambia akalime? Baba yake hakuwahi kulima mama yake hakuwahi kulima leo umwambie akalime inawezekana wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo tunatakiwa tujifunze. Unamchukua mtu ambaye hajwahi kuvua, maisha yake yeye ni kijijini kulima, hajawahi kupiga kasia unamwambia leo eti ukamfundishe uvuvi kwa sababu Serikali ina fedha za uvuvi, umpe na chombo; akizamia kwenye maji kwa kushindwa kuogelea unamsaidia nini mtu kama huyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamchukua mtu, eti ume-*recruit* vijana kutoka JKT ukawapa *block farm* walime ilhali wakulima wanaolima kila siku wapo? Tunafanya biashara gani hapa? Kuna mambo mengi ambayo tumekosea huko nyuma tujifunze kutokana na makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafugaji wako huko vijijini kwetu, njoo Itigi watu wanafuga; na hata hapa amezungumza mzungumzaji wa kwanza amesema Itigi walitunga sheria watu wasifuge mifugo mingi; kwa sababu mifugo iko mingi labda ndyio maana wakakosea. Lakini mtu yule ambaye anafuga kila siku unampa elimu gani zaidi ya kumuongezea uwezo? Mjengee josho, muwekee ardhi bora ya malisho, mfundishe kulima nyasi, kesho atazalisha ng'ombe walio bora zaidi na kama ni nyama atauza, kwa nini umchukue mtu kutoka JKT ambaye baba yake hajawahi kufuga na yeye mwenyewe hajui hata tabia ya kukaa na ng'ombe halafu unamwambia aende akafuge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukaa na binadamu tu hapa lazima ujue tabia za watu sembuse kukaa na mifugo? Wafugaji wapo tuchukue wafugaji wakafanye yale masuala yanayohusu mifugo. Tusichukue watu kwa sababu tu wamepita JKT mme-*recruit* watu na mna hela mkawape kazi

ambayo hawataiweza. Tumeona hili katika Azimio la Arusha, tulichua mashamba tukawapa watu waiokuwa na ujuzi, mashamba yakafa baadaye tukashindwa tukaanza kubinafsisha. Tumechukua viwanda tukawapa watu ambao hawana uwezo leo tunalalamika bado tunataka turudie makosa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu hawana ajira lakini wapo kule vijijini unachukua mtu ambaye alikuwa anakaa mjini amesoma kwa sababu amepita JKT eti akapewe *block farm* kweli tutafika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tilikuwa na kilimo cha kufa na kupona hivyohivyo kilifeli kwa sababu tulikuwa tunachukua watu ambao si wahusika. Juzijuzi tulikuwa na kilimo kwanza imeletwa imeleta mabovu watu wetu wakawa wanashindwa kulima na matrekta yale hata spea hamna baadaye wakawa na madeni makubwa wanadaiwa na hawawezi kulipa kwa sababu tuliwapa vitu ambavyo havifai. kwa nini tusiwanyanyanyanyue watu ambao wanaweza kufanya kazi zao? Nenda kule Madaba msaidie mkulima wa Madaba, njoo Itigi msaidie mfugaji wa Itigi afuge kwenye ardhi yake. Kwa nini umchukulie ardhi umpe mtu mwingine kwa sababu tu eti ametoka JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hili jambo tuliache, na Serikali iache kufanya vitu ambavyo ni vya makisio. Hakuna mahali tumefaulu kwenye hilo toka tumeanza na bado tunakwenda kwa sababu pesa zinatengwa na Serikali basi tunataka tuwape watu. Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya vizuri sana wameweka yale vitalu nyumba wakapewa vijana wakaelimishwa na wanendelea kwa sababu waliwapa watu wanaolima. Unampa mtu unamnyanyua kutokana na elimu yake lakini na jinsi jiografia ya eneo husika ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sekta nyingine zipo ambazo bado kuna changamoto kwa vijana, wanatakiwa

waendelee kupata ajira hizi lakini namna bora ya kuwawezesha ni kupitia Ofisi hii ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pesa zinazotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu bajeti tu ya mwaka jana iliyopita tulitenga bilioni moja tu lakini zilizotoka ni milioni mia mbili na tano asilimia 20. 5, leo tunawasaidiaje vijana wetu? Hebu tuwe *serious* kwenye hili. Natamani kuona leo vijana wa Tanzania wasilalamike kipindi sisi tuko katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tuendelee kushauri vizuri kwa maslahi mapana ya jamii yetu tusiende kwa mihemko tuna mihemko ambayo inakuja kutugharimu baadaye.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya kuna taarifa

**T A A R I F A**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea vizuri na mchango wake. Nilitaka nimpe tu taarifa. Amesema vizuri juu bilioni moja iliyotengwa kwenda kwenye mfuko wa maendeleo ya vijana kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu lakini hela yote imepelekwa kwenye Wizara hiyo au Ofisi hiyo lakini imetoka milioni mia mbili na tano tu asilimia ishirini au kumi na tisa asilimia 79 haijatoka na hela iko pale. Hii inashangaza, Watanzania vijana wengi wanashida wanasema wamekosa vigezo vya kupewa hela hiyo. Kwa nini hela imeenda sasa? Si ingeendelea kubaki hazina ili iendelee kufanya kazi nyingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare umepokea hiyo taarifa?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio naipokea taarifa. Ni jambo linalokera bajeti imetengwa na watu wanahitaji wenye mahitaji wapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa Mheshimiwa Yahaya kuna taarifa nyingine hapa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilikuwa naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kwa fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya vijana fedha tulizopata ilikuwa ni bilioni moja; na ilikuwa haitoki katika kipindi kile kwa sababu zinatokana na *SDL,* kwa maana ya fedha ambazo zinachangwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fedha hiyo iliyotelewa, bilioni moja mpaka kipindi kile cha Bunge lile linakaa katika Bunge la Sita la Saba mpaka sasa tunavyozungumza fedha hizo zilikwishakwenda katika Halmashauri hizo zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha shilingi bilioni moja hakionekani sana katika maeneo kwenda kule kwa sababu inachagiza tu katika mfuko wa maendeleo ya vijana fedha nyingi zinatoka kwenye mfuko ambayo inatolewa kwenye halmashauri zile asilimia nne kwa vijana nne kwa wanawake na mbili kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Sasa hii bilioni moja huwa ni ya kuchagiza kwa vikundi vilivyofanya vizuri zaidi. Mpaka ninavyozungumza sasa tayari fedha hizo zimetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini urejeshaji wake pia ninayo taarifa kwamba tayari tuna zaidi ya bilioni moja ambayo imekusanywa na Mwenge wa uhuru. Kwa hiyo nilitaka tu kusema hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii kidogo ina ukakasi. Kwa sababu, taarifa ya Mheshimiwa Waziri wakati anasoma hapa mbele alituambia kwamba fedha ile waombaji walikosa vigezo, ndiyo taarifa ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo ni vizuri tukasahihisha ili tusaidie watu wetu. Tuko hapa kuishauri Serikali kwa maslahi mapana; kwamba inapotengwa fedha itoke na kama haikutoka zije sababu. Vijana wangu wa Itigi kule wanahitaji hizo fedha, hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kuishauri Serikali, kwamba ione namna bora ya kubeba hili ambalo baadaye tunapata dhana kwamba vijana wetu watakuja kukosa imani yao kwa sababu ya hizi changamoto ndogo ndogo. Kule kwenye halmashauri akina mama wanapata zile fedha, kwa kweli hakuna shida, lakini vijana bado ni changamoto. Kwa hiyo tuendelee kusaidia hawa vijana ili nao siku moja wasaidie hili Taifa. Tutakuja kuwa na vijana ambao ni nguvu kazi lakini hawafanyi kazi kwa sababu fursa hizi zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anachukuliwa kutoka JKT anapelekwa Itigi eti akalime, akalime majani. Wale wa Itigi hawapewi. Kweli hii fursa hii haifanani katika sura hii na ndiyo maana tunashauri ajira za Serikali zilenge kwenye majimbo kama alivyosema Mheshimiwa Olelekaita au zije kwenye Wilaya, zitakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya. Nilimtaja Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, halafu Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Khadija Taya ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye taarifa ya mwaka ya Kamati ya Katiba na Sheria kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea masuala kama matatu, muda ukiruhusu masuala manne. La kwanza kabisa nipende kuongelea suala la lugha mbili…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanyika nilimtaja Mheshimiwa Simai Sadiki lakini kwa vile umeanza, endelea, Mheshimiwa Simai ataendelea baadaye.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na samahani kwa hilo. Kwa hiyo nilipenda niongelee masuala mawili, la kwanza masuala ya lugha katika mahakama zetu. Kama wanakamati walivyosema, mimi sipo kwenye Kamati hii lakini kama Wanakamati walivyosema, mimi niko katika Kamati ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata nafasi ya kuongea na wawekezaji walio wengi; wakati tunapitisha sheria mpya ya uwekezaji, moja ya jambo lililojitokeza kama *concern* kubwa ya wawekezaji ilikuwa ni kwamba; kuwa na sheria kwa Kiswahili ni jambo jema lakini ni vizuri sana sheria zile badala ya kungoja *translation,* zikatafsiriwa halafu wawekezaji wakapewa au zikatumika kuwavuta wawekezaji kwa kuzisoma huko waliko, ilionekana ni vyema na itakuwa na tija kama sheria zetu zitakuwa kwa Kiswahili na Kingereza. Hilo linaendana na dhima nzima ya kutaka kuona kwamba tunapata wawekezaji na kwa kweli tuko katika ushindani wa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata mifano mingi iliyoonesha kwamba kuna nchi nyingi ambazo zimekwenda kwenye lugha zao kutunga sheria lakini vile vile zimetumia lugha ya Kingereza kama moja ya lugha ambazo zitatumika pamoja na lugha ya nchi ile. Nchi kama Rwanda na India zina utaratibu huo. Kwa hiyo mimi niungane na kuiomba sana Serikali kwamba kwa maslahi mapana ya kuangalia kwamba tunakwenda kuwa-*include* watu wote na vile vile tunajaribu kupunguza migogoro. Tukumbuke kwamba tafsiri ya sheria kwa lugha moja kama itatumika na watu wengi kuna uwezekano mkubwa, pamoja na kwamba sisi tunaifahamu lugha hiyo ikaleta mgogoro kwenye tafsiri. Ukishakuwa na mgogoro ni gharama. Kwa hiyo ni vizuri basi wazo hilo likatiliwa maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; kuna suala la taasisi ambayo iko katika utekelezaji na inasimamiwa na Wizara hii, Taasisi ya Baraza la Biashara. Taasisi hii ya Baraza la Biashara imeundwa kwa mujibu wa Waraka Namba Moja wa Mheshimiwa Rais wa mwaka 2001. Moja ya changamoto ambazo Kamati imeziona katika baraza hili ni suala zima la maamuzi kutotekelezwa. Baraza hili halikutani kila siku, halikutani kila mwezi linakutana kwa mwaka mara mbili; na ni baraza ambalo limeundwa kwa ajili ya kuwa ni *forum* ya *dialogue* kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maamuzi yanapokuwa yamefikiwa yanataka utekelezaji. Haitakuwa inatutendea haki kama nchi iwapo tutakuwa na baraza kama hili. Litafanya maamuzi yanayotaka utekelezaji, maamuzi hayo yasitekelezwe. Niombe sana Serikali, kwamba ihakikishe kwa kweli baraza hili likishafanya maamuzi, maamuzi yale yanatendewa haki. Tulichobaini kingine katika utafiti wangu wa haraka ni kwamba wanapokwenda kwenye kikao kingine wanaanza kuongelea *regulations* mpya ambazo zimetungwa ambazo hazi - *encourage* uwekezaji; kwa hiyo imekuwa

kama *vicious cycle*. Kwa hiyo ningeomba sana baraza hili lifanye kazi kama vile ilivyokusudiwa na Waraka wa Rais, kwa maana ya kuwa ni *dialogue, forum* ya maongezi na *forum* ya kutatua matatizo na changamoto za wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilipenda niongelee ni suala zima la Ofisi ya Mashtaka. Kamati imetuambia hapa kwamba ofisi hii imefanya kazi kwa mafanikio. Kuna ukweli pengine kama imefanya kazi kwa mafanikio, lakini vile vile wameonesha kwama bado kuna matatizo hasa ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa hukumu. Suala hili ni suala ambalo lina *impact* kwenye kutenda haki na kwenye kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Hii ni kwa sababu sisi tunaangaliwa na mataifa mengi pamoja na tunaangaliwa na wawekezaji kwamba ni nchi ambayo inathamini sheria zake. Sasa hukumu inapotoka na inapokuwa *DPP* ameshindwa kesi ni suala la *governance* kwamba hukumu hiyo itatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende mbali zaidi, hatuwezi kufumbia macho, kwamba ofisi hii ya *DPP* imekuwa na sintofahamu nyingi kubwa katika utekelezaji wa majukumu yake. Jambo hili limeongelewa na Mheshimiwa Rais mwenyewe, na amekwenda mbali zaidi akataka akaunda Tume ya Jinai ili iweze kwenda kuangalia haki jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi hii ni ofisi muhimu sana katika utawala bora. Nipende kumuongelea Jaji Samatta ambaye wengi tunamfahamu, ni jaji ambaye alifanya kazi kama *DPP* miaka ya 1970 lakini akawa Jaji Mkuu ambaye alistaafu mwaka 2007. Yeye alisema maneno yafuatayo; "*DPP* na maofisa walio chini yake ni watumishi wa nchi ambao wajibu wao ni kulinda maslahi ya umma, yakiwemo yale yanayohitaji mtu asiyeonyeshwa na ushahidi kuhusika na utendaji wa kosa la jinai hashitakiwi na mshtakiwa ambaye

ushahidi dhidi yake hauthibitishi kwamba alitenda kosa hatiwi hatiani."

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ni ya msingi sana na ofisi kama ingezingatia maneno haya nadhani tusingekuwa na sintofahamu ambazo Mheshimiwa Rais ameziongelea kwa kina. Nipende kusema, wahasibu wao tunasema wanajumlisha na kutoa lakini wanasheria wana mambo matatu. Unaangalia *facts,* unaangalia *evidence,* una-*apply law*. Inasikitisha kuona kwamba inawezekanaje tukawa na ofisi ya *DPP* ambayo inakwenda kwenye kesi, inashindwa kwa sababu kesi ambayo hawatakiwi washindwe, hawatakiwi hata waipeleke mahakamani kwa sababu hizo ni *basic principles* za sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nipende kusema kwamba suala la kutokutekeleza hukumu ingekuwa ni vizuri hii Tume ya Haki Jinai itakapofanya tathmini yake ichunguze kwa kina kuona maofisa ndani ya ofisi ya *DPP* ambao kwa makusudi wanafanya mambo ambayo yanaitia nchi hasara na inasababisha wao washindwe kesi halafu inapofika kwenye kulipa, wao wenyewe tena hawataki kutekeleza hukumu kwa kutolipa. Jambo hili lina madhara kwenye uwekezaji wa nchi, lina madhara kwa kuonyesha kwamba sisi hatuwezi kutekeleza mikataba; na hukumu ni kama mkataba ambao mahakama imeutoa ili utekelezwe kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus. Nilimtaja Mheshimiwa Simai.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa fursa ya kuwa mchangiaji siku hii ya leo. Mchango wangu mimi nitauelekeza zaidi katika kuangalia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

yaliyotolewa wakati wa Mkutano wa Tano, Sita na Mkutano wa Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke ya kwamba Bunge ndicho chombo kinachohusika katika utaratibu wa kutunga sheria za nchi hii. Ila, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kipengele namba 97 (5), sambamba na Sheria ya Tafsiri ya Sheria *(The Interpretation of Law Act)* Bunge hili limepewa mamlaka ya kukasimu mamlaka yake kwa taasisi nyingine za Serikali ili kuweza kutunga sheria. Kwa hiyo ni wajibu wa Bunge kuhakikisha mamlaka ilizozikasimu kwa idara au taasisi nyingine zinatumia mamlaka hayo kama inavyostahili. Ili kutimiza wajibu huo, ni jukumu la Bunge kufuatilia kwa karibu namna taasisi au Wizara hizo zinavyotumia mamlaka hayo. Kwa maana ya kwamba au kwa maneno mengine ni kwamba Bunge haliishii katika kuainisha au kubainisha tu dosari zilizotekea katika kanuni au sheria kwa njia ya maazimio, isipokuwa linatakiwa lifuatilie kwa karibu namna maazimio hayo yalovyoenda kutekelezwa na Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulijaribu kufanya ufuatiliaji wa karibu sana wa Maazimio ya Bunge. Ni ukweli kabisa usiopingika kwamba tuliweza kubaini mambo mengi mno. Kuna Wizara ambazo zimeweza kukamilisha utaratibu mzima wa kutekeleza Maazimio ya Bunge yaliyotolewa. Nisingependa nizizungumzie Wizara hizo kwa sababu hizo zimetekeleza wajibu na taratibu zilizowekwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Wizara nyingine ambazo zimejaribu kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa kiwango fulani; kwa maana ya kwamba wapo katika michakato hawajakamilisha utekelezaji wote. Ila, cha kusikitisha ni kwamba muda tuliotoa, kwa sababu tuzingatie sheria hizo ziliwasilishwa hapa na maazimio hayo yalitolewa

hapa tangu wakati wa Mkutano wa Tano na wa Sita maana yake ni muda mrefu. Kutokukamilisha kwao kwa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge maana yake nini, sheria zile bado zinaendelea kuwakandamiza wananchi kule chini. Wananchi bado wanaendelea kulalamika. Tunawaomba waweze kukamilisha jitihada zile za ukamilishaji wa Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalohuzunisha zaidi ni kundi la tatu. Kamati ya Sheria Ndogo katika ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge ilibaini wazi kwamba zipo Wizara ambazo hazijatekeleza hata kwa kiwango chochote Maazimio ya Bunge hili. Ni jambo ambalo linasikitisha sana. Masuala tumeweza kuyapitisha katika Bunge hili, yakajadiliwa katika Bunge hili, sote kwa umoja wetu tuliokuwepo hapa tukatoka na azimio moja. Leo hii unaita Wizara mbele ya Kamati kujibu kwanini wameshindwa kutekeleza azimio hili, wanakwambia kwamba Bunge wakati linaazimia halikuwa sahihi na usahihi wake badala ya kukaa sisi tuliona upo hivi; kitu ambacho kilitakiwa kifanyike hata kabla ya kuletwa kama azimio; kwa sababu kabla ya kuletwa azimio tunakutana na Wizara, tunakutana na Serikali kujadiliana, tunakutana nao kubadilishana nao mawazo, tunaleta hapa kama ni azimio. Inakuwaje yale tunayo yaazimia Bunge bado yaendelee kuwa na mjadala kwa Wizara za Serikali? Hii inasikitisha sana na inawezekana Serikali inafanya hivi kwa kuwa katika kanuni zetu za kudumu za Bunge wanajihisi pengine hatuna kipengele cha kuweza kuwaadhibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kama maamuzi ama Maazimio ya Bunge hayakutekelezwa, inawezekana kanuni zetu zipo wazi, hazisemi kitu gani kitafuta kwa Waziri au kwa Wizara ambayo haikutekeleza Maazimio ya Bunge. Labda tubadilike na tuige kwa wenzetu. Wenzetu wao wana utaratibu kwamba kama maazimio yaliyotolewa na Bunge kwa Wizara fulani na Wizara badala yake haikutekeleza maazimio hayo basi bajeti yao haiwezi ikajadiliwa mpaka

waende wakakamilishe. Labda tuende katika mfumo huo. Kwa sababu chombo hiki kieleweke ni chombo ambacho kina ukubwa wa aina yake, ni chombo ambacho kina umuhimu wa aina yake na kina hadhi na heshima, sawa sawa na Mihimili mingine ya dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifurahishwa sana juzi na kauli ya kaka yangu Mwiguli Nchemba. Kusema kweli alinifurahisha sana aliposema kwamba chombo hiki akiwa anaashiria Bunge, chombo hiki kina nafasi kubwa sana. Hakina jukumu la kujadili matukio tu, lakini kina wajibu wa kuishauri Serikali namna gani ya kuweka utaratibu wa kuhakikisha Watanzania wanaondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana nisieleweke nini ninamaanisha, lakini kiukweli kabisa duniani kote sababu kubwa ya umaskini inaanza na kuwa na kanuni na sheria mbovu. Yule tunayemwita maskini, maana yake ni maskini kwa mujibu wa sheria, yule tunayemwita tajiri, huyo ni tajiri kwa mujibu wa sheria. Tanzania tumekuwa na maskini wengi kwa sababu tumekuwa na kanuni nyingi na sheria nyingi ambazo zinahubiri zaidi umaskini kuliko utajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa na utaratibu wa kuendelea kutunga sheria ambazo zaidi zinaenda kuwakandamiza watu wa tabaka la chini, tukitunga sheria za ku-*deal* zaidi na masuala ya mafungu ya mihogo, basi tusitarajie kwamba lengo na dhamira ya Serikali ina uwezo wa kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Bunge kazi yake kubwa ni kutunga sheria na kuzipa mamlaka nyingine kukasimu madaraka hayo, na tumekasimu madaraka kwa halmashauri zitunge sheria lakini halmashauri zinatunga sheria kinyume na taratibu. Ieleweke kwa mujibu wa taratibu za kisheria yeyote anayetoa mamlaka ya kufanyika jambo fulani basi jambo hilo likifanyika inahesabika sawa sawa limefanywa na

aliyetoa mamlaka hayo. Bunge limetoa mamlaka kwa halmashauri kutunga sheria, halmashauri zimetunga kanuni mbovu, maana yake Bunge limehusika katika kanuni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wangu kwa upande wa Serikali, nashauri tuzidishe umakini kwa taasisi zetu, kwa Wizara zetu, wakati ambapo tunaenda kutekeleza Maazimio ya Bunge; lakini vile tuzidishe umakini wakati ambapo tunakaa na kutengeneza sheria mpya. Kwa sababu sheria ndogo hizi za halmashauri ndizo *automatically, directly* zinaenda kugusa maisha ya Watanzania… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simai, nilimtaja Mheshimiwa Khadija Taya. Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa hii leo kuchangia taarifa ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai mpaka sasa, na jana nimeongeza mwaka mwingine, mwaka ambao mwaka umeinifanya nitafakari mambo mengi sana, leo hii nataka nizungumze na Bunge hili Tukufu lakini na Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu fika kwamba Tanzania yetu inachukua hatua mbali mbali za kusaidia watu wenye ulemavu. Nafahamu fika Serikali imeleta mwongozo mzuri juu ya kuimarisha, kusaidia hali ya watoto ya watu wenye ulemavu. Hata hivyo, naomba niliambie Bunge hili Tukufu hali ya watu wenye ulemavu ni ngumu zaidi kuliko tunavyofikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika likizo ya ya mwezi wa 11 na wa 12, nilipata kufanya ziara kwenda katika vituo mbalimbali vya watu wenye ulemavu. Mambo niliyoyaona kule ni magumu sana hata kuayelezea. Mfano tu mzuri nichukue hapa Kongwa nilenda katika Kituo cha Mlali, nimekuta kuna watoto wenye ulemavu wa viungo wako pale wanalelewa na Kanisa Katoliki la pale Mlali. Hali niliyokuta pale inatia huruma sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wamepelekwa pale kwa ajili ya kupata huduma ya afya ya kunyooshwa viungo mbalimbali lakini pia kupata huduma ile ambayo kuna madaktari wa *KCMC* na madaktari wengine kutoka nje ya nchi wanakuja pale kwa ajili ya kusaidia au wanajitoa. Wazazi wamekuwa wakipeleka watoto wao pale lakini wazazi wengine wameshindwa kwenda kuwaona watoto wao katika vile vituo kwa sababu kile kituo kina chaji shilingi 130,000 kwa ajili ya mtoto kupata huduma katika eneo lile. Sasa najiuliza, kwa Mtanzania wa kawaida anaweza kumudu hii shilingi 130,000 kwa ajili ya mtoto wake kupata huduma katika kituo kile? Mtanzania wa kawaida kila mwezi, 130,000 anaweza? Hilo ni swali la kujiuliza sisi Wabunge humu ndani ambapo katika maeneo yetu vituo kama hivi vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia tu, mzazi anayeshindwa kulipia hiyo anamwacha mtoto wake pale anaondoka harudi tena kumwona, watoto wanatelekezwa katika vituo vile kwa sababu huyu mzazi anaona fika kabisa kwamba mimi sina hii fedha, naendaje pale. Nitakabidhiwa huyu mtoto, nitawezaje kumhudumia? Ningeomba sana Serikali iangalie hili jambo kwa upande wa pili waone kabisa zaidi. Wazazi wanaozaa watoto, wenye watoto wenye ulemavu wanapata shida ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mama yangu aliwahi kuniambia wakati nazaliwa, kabla baba yangu hajaja kuniona hospitali. Kuna mtu aliwahi kumuuliza kwamba hivi,

unafikiri Shabani ataweza kumpokea huyu mtoto? Atamkubali kweli? Hii ni changamoto ambayo wazazi wengi wanakutana nayo, lakini cha kushangaza baba yangu aliponiona alinifurahia na kunikumbatia na leo hii nimefika hapa nilipo. Kwa sababu familia yangu iliweza kunikubali na kunilea na leo hii mimi sijioni kama ni mtu mwenye ulemavu; na watu wengi humu ndani wananiambia kwamba wewe mbona siyo mlemavu? Ni kwa sabau nimelelewa vizuri na familia ambayo ilinikubali na changamoto zangu na kunilea hadi nilipofika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie, ni familia ngapi zinamudu? Akina mama wengi wamekuwa wakitelekezwa na mababa kwa ajili ya kuzaa watoto wenye ulemavu na wanabaki na watoto wale wanawalea wenyewe. Wanapata shida nyingi mno. Leo hii Bunge hili, hapa akija mtu mwenye ulemavu wanatoa huduma ya msaidizi, kwa sababu wanafahamu fika kabisa huyu mtu mwenye ulemavua ana changamoto, hawezi kujihudumia mwenyewe lazima apate msaidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujiulize, yule mzazi ambaye yupo nyumbani, amezaa mtoto mwenye ulemavu, ni msaidizi gani, ni familia gani au ni ndugu ugani ambaye anaweza akakaa na huyu mtoto ambaye ana ulemavu atakulelea wewe? Ina maana huyu mzazi hana budi akae nyumbani, aweze kumlea huyu mtoto, amhudumie mwingine hawezi hata kujilisha mwenyewe. Hawezi hata kuoga mwenyewe. Je, Serikali inamfikiria vipi huyu mama ambaye hawezi kufanya shughuli nyingine zaidi ya kumlea mtoto wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naona kabisa Serikali ione namna na haja ya kuona fika kabisa kwamba waone hawa wazazi *either* watafutiwe wasaidizi, kwamba Serikali ichukue jukumu la kulea au watafute namna ya kuwawezesha hawa wazazi waweze kupata fedha kupitia zile

asilimia mbili. Asilimia mbili ile isaidie akina mama ambao wana watoto wenye changamoto ya ulemavu waweze kujikwamua kiuchumi ili tuone namna gani tuweze kuona hawa watu waweze kulea watoto wao, waone fika kabisa na wao ni *part* ya Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri upo pale katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtu mwenye ulemavu akifika pale anapata msaidizi kwa siku analipiwa shilingi 10,000. Anapata bajaji ya kwenda kumpeleka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Hivi vitu vyote tunafanya juu huku. Bunge linafanya, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya; lakini vipi huku chini kwenye ngazi ya familia? Kwa sababu kama huyu mzazi ameweza kutelekezwa na mwanaume kwa ajili ya kulea, ndugu pia wanaweza kuona kwamba huu ni mkosi kwenye familia yetu. Analeaje huyu mtoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, Bunge hili naamini kabisa, watu wote sidhani kama kuna mtu ambaye hajawahi kufuatwa na shida za watu wenye ulemavu; na ukiangalia fedha ya jimbo haiangalii kusaidia watu wenye ulemavu. Watu wanaingia kwenye mifuko yao kusaidia watu wenye ulemavu. Juzi tumepata takwimu ya sensa lakini bado majibu hatujayapata ya kujua idadi gani ya watu wenye ulemavu ambao wapo katika hii nchi ili Serikali sasa iweze kusaidia. Sasa tunahitaji zile takwimu ili tujue katika kila jimbo kuna watu wangapi wenye watoto wenye ulemavu wanawalea ili sasa Serikali ione haja na Bunge hili lishauri namna gani ya kusaidia hawa wazazi wenye hawa Watoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii naamini kabisa jambo lolote likija *whether* kwa kukatwa tozo, *whether* kwa kukatwa mishahara yetu sidhani kama kuna mtu humu ndani ataweza kuwa na sauti ya kusema kwamba jambo hili hapana, wananchi watakasirika kwa ajili hawataki kuhudumia watu wenye ulemavu. Sasa hivi tumeona kabisa watu wanatafuta

namna ya kujikwamua kiuchumi wanatumia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna tamthiliya ya Juakali. Ukiangalia mazingira ya ile tamthiliya mule ndani Mtu ana *NGO* yake anaita watu wenye ulemavu anatengeneza *story* apate fedha halafu anajinufaisha yeye na familia yake. Yale ndiyo maisha halisi ya huku nchini, siyo tamthiliya ile. Kuna mzazi mwingine ana mtoto wake mwenye ulemavu amemficha ndani, anashindwa namna ya kutoka kwenye jamii, anaona ni aibu, anaona ni mikosi. Hivi vitu si kwenye tamthilia, ni maisha halisi ya Watanzania. Sasa Bunge hili lione namna halisi ya kusaidia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais. Amekuja na huu mwongozo, ni mwanzo mzuri mno, Serikali mmeanza vizuri mno. Sasa kwa Serikali hii mama, kama Mheshimiwa Rais unanisikia, ninakuomba usije kuondoka katika Serikali hii kama haujatatua shida za watu wenye ulemavu kuona namna gani ya kusaidia. Kwa sababu ukiangalia idadi ya watu wenye ulemavu katika nchi hii ni wachache mno na Serikali hii ikiipa kipaumbele, hatushindwi kitu. Kuna kampuni nyingi tu ambazo zinafanya kazi katika nchi hii. Kuna fedha nyingi wanazo, *CSR* sijui nini na nini. Mfuko wa watu wenye ulemavu ni muhimu kulea watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Bunge hili Tukufu, endapo sheria hii itakuja muiunge mkono, kwa sababu naamini kila mtu hapa ni mlemavu mtarajiwa. Kwa sababu naamini kuna Wabunge humu ndani wamekuja wakiwa wazima na sasa hivi ni watu wenye ulemavu na leo hii sisi tuna watu tunawazaa humu ndani, tutazaa watoto wenye ulemavu. Leo hii tukitengeneza msingi mzuri au tathmini nzuri ya watu wenye ulemavu kuishi vizuri, tunajitengenezea sisi wenyewe na kizazi chetu cha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo naunga mkono hoja nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Shaban Taya. Tunamalizia na mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa hai na kuiona siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuipongeza Kamati ya Sheria Ndogo; kiukweli wamefanya kazi kubwa na ninawapongeza sana. Pia ninampongeza Mwenyekiti wetu kwa namna alivyowasilisha vizuri taarifa ya kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajielekeza kwenye mambo machache ya upande wa sheria ndogo. Tumebahatika kuchambua sheria nyingi, na ni ukweli usiofichika bado sisi kama Bunge hili tuna kazi ya kufanya. Tumekasimu madaraka haya kwa baadhi ya taasisi zenye uwezo wa kutunga hizi kanuni lakini tunaona bado changamoto ya hizi sheria ndogo ni nyingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo nyingi zinakosa uhalisia, hazitekelezeki na zinaleta changamoto sana kwa maisha ya wananchi. Ukiangalia sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya Wilaya ya Misungwi ya mwaka 2022 inatoa katazo la watu kufanya shughuli yoyote ya maendeleo kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa nne asubuhi kwa lengo la kufanya usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo linaweza likawa zuri la kufanya usafi lakini kutoa katazo la kufanya shughuli yoyote

ya maendeleo, hili si sawa. Sisi tunadhani kama taifa tulitakiwa tufikirie kwenda mbele na si kufikiria kurudi nyuma. Kama lengo likiwa ni kufanya usafi tuondoe hili zuio la kusema shughuli za maendeleo zozote zisifanyike kwa masaa haya matano. Sheria hii inaleta usumbufu sana kwa wananchi. Jiulize, wewe eneo la biashara kila siku uko hapo unafanya biashara, ni usafi gani huo utakaohitaji kuufanya kwa masaa matano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu ambao wanaweza wakafanya usafi kwa nusu saa, waruhusiwe kuendelea na shughuli zao za maendeleo. Wapo watu ambao wanaweza wakafanya usafi kwa muda wa saa moja, waruhusiwe kuendelea na shughuli zao za maendeleo. Kuna mama zetu hawa ambao wanafanya biashara ndogo ndogo. Mama anapika vitumbua, biashara yake anatakiwa afanye asubuhi. Unapomwambia kuanzia saa 12 mpaka saa nne asifanye shughuli yoyote tunarudisha uchumi nyuma wa Watanzania hawa masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii haiko tu Misungwi, sheria hii iko maeneo mengi; na moja ya maeneo ambayo sheria hii inatumika, hata hapa Dodoma sheria hii inatumika. Sheria hii inatumika Ikungi, Nsimbo na maeneo mengi ya nchi yetu. Sisi kama Kamati tunaona sheria hii imepitwa na wakati, tunarudisha nyuma maendeleo ya wananchi wetu kwa kuweka sheria hii ambayo ina usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiitazama sheria ndogo hii kwenye utekelezaji wake, haiwezekani. Hata kwenye *practice* huko mitaani watu hawaendi kufanya usafi kama tulivyotarajia; wanachokifanya ni kufunga biashara zao ifike saa nne waweze kufungua ili wasikamatwe na kupigwa faini. Sasa tujiulilze, sisi kama taifa tunataka nini? Tunataka usafi au tunataka watu wafunge biashara kusubiri saa nne ndipo wafungue?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe, kama kamati ilivyoshauri jambo hili kamati imekataa na haikubaliani nalo. Ukija sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi inazungumzia ni kosa kwa abiria kutupa takataka nje ya chombo cha usafiri. Kweli kila mtu anakubaliana na jambo hilo; lakini kusema tukio hilo au kosa hilo litachukuliwa kama limefanywa na mmiliki wa chombo hicho, hiyo siyo sawa. Kwanza ni kinyume cha sheria, ni kinyume cha misingi ya sheria lakini pia kinapingana na sheria mama. Ukisoma kifungu cha 40 cha Sheria ya Mazingira kinazungumzia *principle* ya mtu aliyefanya kosa ndiye awajibike. Haiwezekani leo abiria atupe takataka, faini alipe mwenye basi, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama kamati tumeshauri, kama kosa litafanywa na abiria, basi awajibishwe abiria, kama kosa litafnywa na kondakta, basi awajibishwe kondakta na kama kosa litafanywa na mwenye chombo, basi awajibishwe mwenye chombo; huo ndio uliokuwa usahuri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi ndogo sisi kama Bunge tunazipitisha hapa; na tumetoa mamlaka, ukisoma *Cap 1* kifungu kile cha 37 kinatoa mamlaka ya sheria hizi kuanza kutumika kabla hazijapitishwa na Bunge. Shida kubwa ya changamoto hii inaanzia hapo. Kwa kuwa tumeruhusu sheria hizi zianze kutumika kabla hazijapitishwa na Bunge, hicho ndicho kimekuwa kichaka cha wananchi wetu kuteswa na sheria hizi mbovu, kukandamizwa na kanuni hizi mbovu na mwisho wa siku zinaletwa tayari wananchi wameshaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina ombi kwa Bunge hili. Kama itakupendeza kuna haja sisi kama Bunge kufanyia marekebisho Kifungu cha 37 cha Sheria ya Tafsiri. Kifungu cha 37 kiondoe ile hali ya kuiruhusu sheria hizi kuanza kutumika kabla hazijapitiwa na Bunge. Kwa sababu unaona changamoto hizi, unapozungumzia Misungwi wana sheria hii.

Pia Halmashauri ya Nsimbo ime-*copy* sheria hizi nao wana sheria hizi hizi. Kwa hiyo ukifanya tathmini utagundua kuna sheria nyingi ndogo mbovu zinazoumiza wananchi na bado zinaendelea kutumika zikisubiri mpaka Bunge lije liziite, lizichambue na lizipitishe. Kwa hiyo mimi niombe Waheshimiwa Wabunge, kama itawapendeza kuna haja ya Serikali kuleta sheria ili sisi tuifanyie marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kusema yafuatayo. Mwaka 2019, sisi kama Bunge tulipitisha sheria ndogo, na sheria hiyo ilikuwa ni kanuni ya kukataza mifuko ya *plastic*. Leo ni takribani miaka mitatu tu tangu zuio hilo litokee lakini naomba nikupe taarifa, mifuko ya *plastic* sasa iko mitaani na inatumika, na Serikali iko kimya haitoi tamko lolote kuhusu kitendo hicho kinachoendelea. Sasa hii inashangaza. Sisi kama Bunge tunakaa hapa, tunapitisha sheria, tunatoa maazimio yetu lakini utekelezaji wake ndio unakuwa na changamoto hizo. Mimi niombe, niiombe Serikali. Kwanza inajukumu la kufanya kujua kwamba taarifa ya mifuko inayo au haina.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi? Mheshimiwa Ramadhan.

**T A A R I F A**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji dada yangu Sylvia na mwanakamati mwenzangu kwamba Zanzibar ilipitisha kanuni kama hiyo anayoisema ya kuzuia mifuko ya *plastic,* leo Zanzibar mifuko ya *plastic* ni historia. Kama wenzetu wanataka kwenda kujifunza waende Zanzibara wakajifunze, wao wamewezaje, huku tushindwe tuna nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo taarifa kwa mikono miwili, si jambo baya kujifunza kwa waliofanikiwa. Kwa hiyo hata sisi kama tumeona changamoto ya utekelezaji wa mifuko hii ya *plastic* bado tuna nafasi ya kwenda kujifunza kwa wenzetu, kwa hiyo siyo jambo baya kujifunza kwa waliofanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kusema, ninaipongeza Kamati; lakini nilikuwa na ombi maalum kama Kamati itaona inafaa kuongeza azimio kwenye Maazimio ya Kamati tuitake Serikali ilete sheria *cap 1, interpretation of laws act,* ije hapa tuifanyie marekebisho hicho kifungu cha 37. Kwa sababu kifungu hicho ndicho kinacholeta changamoto zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja za Kamati zote mbili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sylvia Francis. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemuahidi Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, namkaribisha sasa kwa ajili ya mwongozo wake aliokuwa anataka kutoa. Karibu Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunisikiliza na kunipa nafasi nisimame, na ninasimama kwa mujibu wa kanuni namba 54(1) ili utoe nafasi Bunge lako tukufu lijadili jambo ambalo inaliona ni zito na linahitaji kidogo mjadala wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na maswali ya Wabunge mengi kuhusu migogoro ya ardhi, migogoro ya mipaka kati ya hifadhi zetu na wananchi, na jambo hili pia

likaibuka kwenye taarifa za Kamati za Kisekta. Mwisho ilibainika kwamba hiyo migogoro bado inaendelea kusumbua wananchi pamoja na kwamba ilikuwa imeundwa Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta ambao jukumu lao ilikuwa ni kuzunguka na kukutana na wananchi na kuona namna gani Serikali itakuja na suluhisho la hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule jimboni kwangu Arumeru Mashariki, tunavyozungumza sasa hivi wananchi wa Kitongoji cha Momela ambao wanapakana na Hifadhi ya Arusha, wanalazimishwa kusaini hati ya fidia ili waondolewe kwenye maeneo ambayo walikuwa wanaishi kwa miaka mingi ambayo ni mashamba mawili namba 40 na namba 41. Mashamba haya yalikuwa yanamilikiwa na mlowezi na akaamua kuondoka na akaachia Serikali ya Kijiji. Baadaye yale mashamba yalitwaliwa na hifadhi kwa shughuli za uhifadhi kinyume cha taratibu kwa sababu Serikali ya Kijiji haikuhusishwa. Matunda yake sasa wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017, mipaka ilirekebishwa kwa nguvu nyingi, wananchi wakapigwa mabomu, nyumba zao zikawa *annexed,* zikaingia kwenye hifadhi. Leo hii ng'ombe wakitoka ndani wanasemekana wameingia hifadhini kwa hiyo wengine wanauwawa na wananchi wanafanyiwa fujo. Mbaya zaidi kwa sababu sasa hivi tumeshapitisha sheria ya jeshi usu ni kwamba hata maisha yao yako hatarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, ukiachana na tatizo la Momela, kuna eneo la *KIA (Kilimanjaro International Airport)*. Kiwanja hiki kilijengwa miaka ya 1969 na kilifunguliwa mwaka 1971. Wakati wa ujenzi wake, kuna wananchi walikuwa wanaishi yale maeneo yanayozunguka kile kiwanja na walishiriki kuchanganya zege kwa ajili ya ujenzi wa kile kiwanja. Mwaka 1998, kile kiwanja kilibinafsishwa, uendeshaji wa kiwanja ulibinafsishwa kikapewa *KADCO.* Ni wakati huo sasa iliibuka suala la mipaka ambayo ilitolewa kwa *GN 269;*

kwamba eneo la *Kilimanjaro International Airport* ni *square kilometer 110,* kwa maana hiyo kuna vijiji ambavyo vilikuwa vinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi, nilijaribu kuchunguza chunguza nikakuta uwanja mkubwa wa Heathrow ambao uko *very busy,* ukubwa wake ni kilometa za mraba 12. Uwanja wa Amsterdam ambao uko *very busy* una kilometa za mraba 27. Uwanja wa *Charles De Gaulle* wa Ufaransa ambao pia nao ni mkubwa na uko *busy,* kilometa za mraba 32. Sasa sisi kiwanja chetu eneo lake ni kilometa za mraba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia hoja yako naona una hoja zaidi ya moja.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, nakushukuru sana. Ninachotaka kusema hapa ni kukuomba, wale wananchi ambao wanasainishwa hati za fidia, hilo zoezi lisitishwe. Bunge lako likae, lijadili kidogo na kutoa maamuzi kwamba lile zoezi lisitishwe na hata kule *KIA,* wananchi wameshindwa, wamenyimwa kuendeleza mashamba yao na ni kipindi cha msimu wa kilimo sasa hivi, hilo zoezi pia nalo lisitishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mbona mnasimama? Bado mimi sijasema chochote.

Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo alitakiwa kutoa mwongozo kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 54 baada ya maswali lakini kwa vile nilimuahidi kwamba nitampa baadaye ndiyo maana nimemruhusu aweze kusimama na kutoa mwongozo wake.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni kwamba, kwanza amezungumza mambo ambayo ni zaidi ya moja kwenye dharura hiyo. Kwa hiyo jambo la dharura linatakiwa liwe moja la kujadiliwa. Hata hivyo nasema kwamba migogoro ya ardhi na mipaka ya hifadhi imejadiliwa kwa kina wakati tunajadili Kamati ya Ardhi na Maliasili. Kwa hiyo mapendekezo yametolewa na Serikali imepokea. Hata hivyo kwa sababu kuna hiyo changamoto ambayo umeitaja na mimi kwa mujibu wa kanuni ya 55(4) nalielekeza hilo kwa Serikali kwa ajili ya mwongozo na hatua zaidi za utekelezaji na huo ndiyo mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11: 00 jioni.

*(Saa 7:05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022**
**na**
**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

Haya tunaendelea na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, wote niliowataja muda ule wajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii ya kwanza kabisa kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja za Kamati hizi mbili za Kudumu za Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayofanya ya kuiendeleza nchi yetu. Hakika ustawi wa nchi yetu sasa uko kwenye mikono salama, kutokana na jitihada anazozifanya Rais katika kujenga umoja wa kitaifa, kulinda muungano wetu, kutafuta uwezo kutoka nje na uwezo wa ndani ili kuleta ustawi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi Mheshimiwa Rais ameendelea kusaidia nchi yetu kuongozwa katika misingi ya kidemokrasia, misingi ya haki inayojali utu wa binadamu na ndio maana Mheshimiwa Rais amekataza watu wengine kufikishwa mahakamani, bila kesi zao kukamilika au upelelezi kukamilika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wote wawili wa Kamati zote za kudumu kwa taarifa zao nzuri pamoja na Wabunge wanaounda Kamati hizo zote mbili wamefanya kazi nzuri na taarifa zao zote ni nzuri na nitamke bayana kwamba ninaziunga mkono taarifa zote mbili za Kamati hizo mbili za kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee na hata pamoja na malalamiko mengi ambayo yametoka katika ukumbi huu leo asubuhi, kulalamikia baadhi ya maeneo ambayo mambo hayaendi vizuri na hasa baadhi ya taasisi ambazo zimekuwa zimepewa mamlaka ya kutunga sheria hizi ndogo na kwa bahati mbaya wakawa wanatunga sheria

ambazo kimsingi zinakinzana na sheria za Bunge na hata wakati mwingine kupingana au kukinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jaji Feleshi, kwa kiwango kikubwa tangu ameingia katika ofisi hiyo, kwa kweli naona utulivu mkubwa na ushirikiano wake mkubwa sana wa kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Sisi wengine tunaojua rekodi yake akiwa *DPP,* akiwa Jaji na hatimaye Jaji Kiongozi tunaamini kabisa ofisi hiyo iko salama na nampongeza yeye pamoja na *DPP* wa sasa. *DPP* wa sasa anafanya kazi nzuri na nina hakika haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza katika Bunge hili la leo zitarekebishwa na viongozi wetu hawa wawili ambao wanaongoza taasisi hizo muhimu sana. Pia kwa namna ya pekee nawapongeza pia Mawaziri wa Wizara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze sasa katika baadhi ya maeneo ambayo ni ya maana sana na ni ya msingi pia katika hoja za Kamati zilizowasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko mengi juu ya baadhi ya mambo ambayo hayajakaa vizuri na hasa katika maeneo yale ambayo yanahusiana na dhamana tuliopewa Kikatiba kwamba Bunge lako tukufu lina mamlaka ya kutunga sheria, lakini bahati mbaya sana kwa jinsi ilivyo tena hizi sheria ndogo ndogo wakati mwingine zinatungwa na kutumika kabla hazijaingia katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kwamba ipo haja ya kubadilisha sheria na kulitizama jambo hilo upya ili sheria hizi ambazo zimegeuka kuwa kero kwa wananchi ziwe zimepitia katika Bunge lako tukufu. Bunge lako tukufu halina nafasi ya kulalamika wala

Serikali haina nafasi ya kulalamika. Mimi siamini katika kiongozi anayepewa dhamana au mamlaka yoyote inayopewa dhamana badala ya kukalia kile kiti walichopewa na kujaa, unakaa upande mmoja kama una jipu. Ni vizuri siku zote unapopewa dhamana ukajaa katika kiti chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Bunge lako tukufu halina nafasi ya kulalamika kwa sababu kwanza linaongozwa na Spika mahiri, makini, mwanasheria aliyebobea, kiongozi madhubuti na ni kijana ambaye bado akili yake iko vizuri zaidi. Pia ana Wenyeviti wasaidizi na Naibu Spika wa viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi kwa sababu mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali ni ya kwetu kwa mujibu wa Katiba. Lakini Ibara ya 151(1) inaweka tafsiri bayana ya mamlaka ya nchi kwamba ni pamoja na Serikali na Bunge sisi tumetajwa bayana, Mahakama haikutajwa kinagaubaga katika Ibara ya 151 katika tafsiri ya mamlaka ya nchi. Kwa hiyo, sisi ni mamlaka ya nchi pamoja na *executive*. Sisi katika Ibara ya 63 tumepewa mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwa sisi ndio chombo kikuu kwa mujibu wa Katiba kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siamini katika Bunge ambalo linaona kuna tatizo pale mbele, tunashauri kupitia Kamati za Kudumu za Bunge, tunashauri kapitia Bunge, bado zipo taasisi na maafisa wa umma ambao wanaelekezwa kubadili sheria zinazokinzana na sheria za Bunge, wanaelekezwa kubadilisha sheria zinazokinzana na Katiba ambazo ni batili moja kwa moja kwa mujibu wa Katiba bado wanaendelea kunyamaza na kupuuza maelekezo ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kabisa kwamba siku 30 zilizotolewa na siku 60 zilizopendekezwa na Kamati

tutaziheshimu na kuziunga mkono kupitisha maazimio hayo leo na baada ya hizo siku 60 ninaamini kabisa na wale waliopewa siku 30 watarekebisha madhaifu yaliyoonekana na Kamati zetu mbili za kudumu ambazo zimeshughulikia na hasa Kamati inayoshughulikia sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba Bunge hili ni Bunge madhubuti na kwa kweli halipaswi kulalamika. Miaka ya 1990 Bunge hili hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipokuwa imekuja na hoja ya Tanganyika ya *G55* ambayo ilikuwa ni kinyume na sera za CCM, kinyume na *Article of Union,* lakini bado ndani ya muda mfupi wana-CCM walisimama na Wabunge walisimama wakakataa na Mkutano Mkuu wa Chimwaga ulikataa, lakini baadaye wakarudi tena na kuleta hoja hiyo kutokana na hasira walizokuwa nazo na kutaka kutuingiza katika muundo wa Serikali tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema hasira zenu zisielekezwe kwenye kutuundia jambo linalokinzana na sera, jambo linalokinzana na *Article of Union* ambayo ndio msingi wa Muungano wa nchi zetu mbili na Mwalimu alitumia maneno haya yafuatayo na mimi naomba niyanukuu katika kitabu cha Mwalimu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania na hili nalisema kwa taasisi hii na nalisema kwa taasisi zingine zote naomba kunukuu; "Kukubali kufanywa vikaragosi vya viongozi ni dalili ya woga, si dalili ya heshima na woga na heshima ni vitu viwili mbalimbali. Maadili mema hayatudai tuwaogope viongozi wetu na viongozi makini hupenda kupata heshima ya wananchi wenzao, lakini hawapendi kuogopwa. Kuogopwa ni sifa na ada ya madikteta. Viongozi halisi hawapendi kuishiriki, kujenga mazoea ya kutii viongozi hata katika mambo haramu ni dalili ya woga ni kukaribisha udikteta." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayatumia maneno haya kwa sababu sifurahii kuona Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likilalamika juu ya maamuzi ambayo mlikwishayafanya. Ningependa tutoke na maazimio kwamba wale walioagizwa wayafanye tuwajue ni akina nani walipaswa kusimamia katika sekta hizo na Bunge hili lielezwe ni nani hao wanaokaidi.

Kwa hiyo, sisi tuko hapa kwa niaba ya wananchi tuchukue hatua, kama hatuna mamlaka ya kuchukua hatua dhidi ya Waziri mmoja mmoja, dhidi ya mtendaji mmoja mmoja, tuchukue hatua kwa wale ambao tuna mamlaka nao ili wawasimamie hao ambao wamepewa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto alibainisha juu ya dhahama wanazozipata wafugaji sasa kutokana na tafsiri ambazo hazijakaa vizuri. Nchi yetu au Bunge letu lipitie Sheria Namba 5 ya Uhifadhi ya Wanyamapori ya mwaka 2009 na marekebisho mengine ya mwaka 2022, yapo maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria iliyokuwepo hayakuwa yanatajwa kama ni maeneo ya uhifadhi, lakini kwa sheria ya sasa ni maeneo yaliyohifadhiwa, ni ardhi ya hifadhi. Lakini unakuja kuhifadhi wakati tayari kuna binadamu walioko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tukae pamoja kwa sababu ulindaji, uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za nchi ni jukumu la kila raia wa nchi hii, ni jukumu la kila Mbunge aliyeko katika ukumbi huu, ni jukumu la kila kiongozi. Tukae ili pale ambapo ardhi za vijiji ambazo sasa mnataka kufanya kwa *Wildlife Migratory Route, Wildlife Dispersal Area, Breeding Areas* mnataka kufanya kuwa *Game Controlled Area,* katika maeneo ambayo yako kwenye ardhi za vijiji hakuna namna unaweza kuichukua

ardhi ya kijiji ambayo imekataliwa na sheria ukaifanya kuwa *Game Controlled Area.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiacha hii kwa sababu yako mazungumzo na malalamiko niliyowasilisha nikiamini nitakaa na viongozi wenzangu tuyafikie mwisho, lakini kikubwa ninachosema hamuwezi kuendelea kutoza ng'ombe faini ya shilingi 100,000 badala ya ku-*compound* kama sheria inavyosema katika kifungu cha Sheria ya *TANAPA (National Parks)* kifungu cha 20A imeweka bayana kabisa juu ya ku-*compound* lile kosa na kwa yule muhusika ndio anayepigwa faini, ng'ombe hawezi kupigwa faini, anapigwa mmiliki wa ng'ombe.

Kwa hiyo. rai yangu ni vizuri tukazingatia ushauri uliotolewa na Wabunge ili kuepusha adha hii ya kuwatoza wananchi ada zisizokuwa na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi sote ni mashahidi juu ya hukumu ya Mheshimiwa Elenina ambaye alimaliza kesi yake mwaka 2018 na akashinda, yule mfugaji ambaye amefilisiwa na mnamwona kwenye mitandao ambaye ameshinda kesi yake Mahakama Kuu. Bado *DPP* aliweza kung'ang'ania wale ng'ombe kwamba akate rufaa abaki na ng'ombe. Jaji wa Mahakama Kuu Jaji Kalombola alikataa na baada ya kukataa bado walikaidi na wale ng'ombe wamekufa na yule mfugaji alikuja kupewa ng'ombe 90 kati ya ng'ombe 265 ambao walikaa nao kwa muda wa miaka mitatu. Ng'ombe 265 wakizaa kila mwaka kwa miaka mitatu ni ng'ombe wangapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo, na kwa kweli naishauri Serikali iendelee kuwa sikivu katika eneo hilo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunashukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Waheshimiwa ikishapiga kengele ya kwanza jiandae ku-*summarize* hoja yako, ikipiga ya pili unakatishwa hapo hapo.

Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka amemaliza sasa namwita Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel wakati huo Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo wanajiandaa.

**MHE. NOAH L. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Taarifa ya Kamati zote mbili ya Katiba na Sheria na Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kama tujuavyo Bunge lako limepewa mamlaka chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 64 na Ibara ya 97 yenyewe ndiyo imepewa mamlaka katika kuhakiisha kwamba sheria inatungwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba hakuna chombo kingine chochote chenye mamlaka labda Bunge ikasimu madaraka haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo imekuwa ikifanyika vyema na Bunge lako na Kamati pia tumeendelea kufanya kazi nzuri ya kuchambua miswada mbalimbali ambayo imekuwa ikiletwa na Serikali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kupata sheria nzuri, Sheria ambayo inakuwa ni ya matumaini, sheria ambayo inaweza kujenga uchumi na mambo ambayo yanaleta matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia katika jambo lolote tulipokuwa kwenye mjadala mbalimbali kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati, ambayo sasa kama tunataka kujenga uchumi lazima tutizame sheria zetu, kama tunataka kuhakikisha wananchi wetu wanapata nafuu ya maisha kwa maeneo mbalimbali lazima tuangalie sheria zetu, kwa mfano kama tunataka kuhakikisha kwamba mali za Serikali zipo salama lazima tuendelee tena kuangalia sheria hii ya manunuzi *(Public Procurement Act)* sasa inatakiwa irekebishwe kwa sababu imekuwa kama ndiyo yenye kutoa mwanya wa wale wahalifu wa wizi na masuala ambayo hayafai katika ubadhirifu wa mali za umma. Sheria hii inatoa mwanya mkubwa sana, lakini sheria hii imeendelea kuchelewesha miradi mbalimbali ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ni kwa nini hatutaki kuirekebisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kutokutaka kurekebisha simaanishi kwamba katika utaratibu wa kutunga sheria tunajua kwamba lazima Serikali ilete muswada kwenye Kamati na baadae tuje kwenye Bunge, sasa hii ni changamoto kubwa kwa sababu Serikali lazima ione kwamba hiyo sheria imekuwa na mapungufu makubwa; kwa nini hatutaki kurekebisha au tunataka kuendelea kuwalea hawa wezi, hawa wanaoweka mwanya wa ujambazi, hawa ambao wanataka kutafuna fedha ambazo zinatafutwa na Mheshimiwa Rais usiku na mchana? Hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sheria hizo zinatakiwa zirekebishwe, lakini pia hata Sheria ya TAKUKURU bado na yenyewe ina madhaifu makubwa, watu wenye kesi za kuku sijui na kesi ndogo ndogo za kupigana ndiyo wanaoshughulikiwa zaidi kuliko wale ma-*giants* wanaofanya ufisadi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima sheria hizi ziangaliwe kama kweli tuko *seriously* katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inataka kusonga mbele kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mheshimiwa Rais,

amekuwa akijitahidi sana ku-*harmonize* mambo mengi sasa na sisi wasaidizi wake tujitahidi kuhakikisha kwamba tunakwenda kwa *spirit* hiyo hiyo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria pia ambayo inatakiwa irekebishwe sheria iliyoanzisha *TEMESA*. Hii nayo ni kidonda ndugu kwenye halmashauri zetu, sheria ile inasema gari ikatengenezwe *TEMESA,* lakini halmashauri inalazimishwa wakishapeleka gari pale wao *TEMESA* wanapeleka kwenye *garage* za uchochoroni. Sasa gharama inakuwa kubwa kuliko hata halmashauri ingetengeneza, hii nayo ni changamoto kubwa ambayo lazima Serikali ifike mahali iweze kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la utunzi wa sheria kwa lugha ya Kiswahili. Tumepitisha sheria hapa tukasema ile sheria imeeleza bayana kwamba katika mjadala lazima katika maamuzi yetu au utungaji wa sheria lazima sheria iwe kuna Kiswahili na Kiingereza ili iweze kusaidia wananchi wetu waweze kupata haki zao na waweze kuelewa hasa tukizingatia kwamba Tanzania sisi siyo kisiwa, sisi ni miongoni mwa nchi za *Commonwealth* ambayo tunatumia *precedent* za Jumuiya ya Madola na kama unavyojua kuna maneno mengine kwenye sheria ambayo hata Kiingereza haina, maneno kama *mandamus*, *certiorari*, *obiter dictum* na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ngumu sana kwa hiyo tunataka tuombe Serikali ifike mahali ituletee na tumeshauri kama Kamati, tunapoletewa miswada uje muswada wa Kiingereza na Kiswahili kwa sababu kama jinsi ambavyo ilikuwa *intention* ya Bunge wakati wa kutunga ile sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona nisiache suala la Marekebisho ya Sheria ya Ndoa, nataka niiulize Serikali; nini chanzo cha kurekebisha sheria hiyo? Kwa nini tunataka kwenda kuangalia sheria nzima ya ndoa kama ndiyo ni

mbaya zaidi? Mahakama imetoa hukumu mwaka 2016 kwamba vifungu namba 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa inakiuka Katiba, sasa kama Mahakama imetoa Serikali ikakata rufaa mwaka 2019, Mahakama ya Rufaa Tanzania ikakataa; sasa Serikali imeenda tena zaidi inataka tena kuchukua maoni kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wadau wamefungua kesi ya kutokukubali maoni hayo yachukuliwe; sasa je, Serikali haioni katika kukataa kutekeleza uamuzi wa Mahakama yenyewe inakosa uhalali wa kuweza kuendelea kusimamia sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali inataka kuangalia sheria nzima ya ndoa kama ni mbaya badala ya kuangalia vifungu viwili ambayo Mahakama imesema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kusababisha mgogoro pasipo na sababu, hii siyo sawa, lazima muangalie vifungu viwili tu ambayo Mahakama ndiyo imesema. *(MakofI)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Noah Mollel, nilimwita Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda aweze kuchangia.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kabla ya yote kwanza naunga mkono hoja zilizotolewa na wote Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo na kukubaliana na taarifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pili ningependa kujielekeza katika kuchangia kidogo kwenye Sheria Ndogo. Kama

unavyofahamu sheria ndogo ndiyo sheria ambazo zinatekelezwa huko chini kabisa kwenye maisha ya watu ya kila siku. Inawezekana sheria moja ikazaa sheria ndogo hamsini hata mia na ndiyo zinazotekelezwa kila siku huko, na zipo sheria ndogo ambazo katika utungaji wake zimeonekana kupitia Kamati ya Sheria Ndogo kwamba zinakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa jambo hili ni jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wa nchi inayofuata utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano ipo Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Manispaa ya Temeke ya mwaka 2022 kifungu cha 5(5) kinampa uwezo Afisa Muidhiniwa wa kukusanya ada na ushuru kuingia jengo lolote, wakati wowote.

Narudia kuingia jengo lolote, wakati wowote kwa ajili ya kukusanya ada na ushuru. Sasa ukiangalia sheria ndogo hii inapingana na Katiba, ukisoma Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Ibara ya 16(1) Katiba inasema hivi naomba ninukuu; "Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi, familia yake na unyumba wake na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake binafsi."

Sasa kama unampa Afisa Muidhiniwa kukusanya kodi na ushuru kuingia jengo lolote, wakati wowote maana iwe saa sita, saa saba na anawakuta wakati mwingine watu wako kwenye shughuli nyingine muhimu majira ya saa nane yeye anataka ushuru na kodi utaona kabisa kwamba sheria hii haiendani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hiyo tu zipo sheria, ipo sheria ndogo ambayo ni Sheria Ndogo za Udhibiti wa Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ambayo ilitangazwa kwa Tangazo la Serikali Namba 564; kifungu cha 8(4) kinaweka masharti ya kwamba ikiwa

chombo kama gari ambalo limekutwa na madini hayo ya ujenzi mawe/mchanga, likakamatwa na mwenye nalo hakuonekana ndani ya siku 30 basi sheria hii ilikuwa inatoa mamlaka kunadiwa hiyo gari na pesa za halmashauri ziweze kuchukuliwa.

Sasa ukiangalia gari ya shilingi milioni arobaini/hamsini ninyi mnadai ushuru wa *trip* moja ya mawe, kwa sababu siku thelathini mwenye nalo hakuonekana, sasa mnachukua sheria na katika kuchukua sheria mnanadi mali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inapingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 13(1) hadi (6) ambacho kinazungumzia usawa mbele ya sheria nitanukuu sheria hiyo inasema hivi; "Haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu yanalindwa na kuamuliwa na Mahakama na vyombo vinginevyo vya mamlaka vilivyowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria." Sasa wewe una nadi gari ya mtu ya shilingi milioni hamsini kwa madai ya *trip* moja ya mawe bila kumpeleka mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, Katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 13(6)(a) kinazungumza hivi; "Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa Mahakama au chombo kingine kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa umakini na haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo kingine kinachousika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vifungu hivi vya Katiba na ukaangalia sheria hizi ndogo ambazo zinatungwa na halmashauri zetu, utaona kabisa kwamba zinakinzana na kutofautiana mbali kabisa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, kuna sheria inayohusu masuala ya mazingira ya udhibiti wa mifuko ya plastiki na vifungashio ambayo kifungu cha 32 kinasema kwamba; "Iwapo mtu aliyeingiza vifungashio na vikakamatwa basi mtu huyo atakuwa na haki ya kukata rufaa ndani ya siku thelathini kwa Waziri mwenye dhamana." Lakini kanuni hiyo haisemi Waziri mwenye dhamana itamchukua muda gani kutoa haki au kumaliza shauri hilo na kwa vyovyote vile jambo hili linaweza likafika mahala likapoteza haki ya muhusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema haya kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 64(5) inasema; "Katiba itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano wa Tanzania na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba basi Katiba itakuwa na nguvu na sheria hiyo nyingine kwa kiasi inachoathiri Katiba itakuawa ni batili."

Kwa hiyo, sisi katika kuchambua sheria ndogo tuliona kabisa kwamba sheria ndogo hizi nyingine zinatungwa na zinakinzana na Katiba na kwa mamlaka haya ya Katiba kwa mujibu wa kifungu cha 64(5) basi sheria hizi au kanuni hizi zinazotungwa zinakuwa zimekufa zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango wangu huo, basi naomba kuendelea kuunga mkono hoja na nawapongeza sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na kwa kuzingatia muda zaidi pia.

Nilimwita Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina wakati huo Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray wanajiandaa.

**MHE LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Taarifa ya hizi Kamati mbili; Kamati ya Katiba na Sheria, Kamati ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hoja zote za Kamati naziunga mkono japo kuna baadhi ya maeneo taongezea ushauri wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni madai na usuluhishi; Serikali yetu imekuwa ikiendesha kesi mbalimbali za madai na usuluhishi Kitaifa na Kimataifa na tulipewa taarifa kwamba na labda kwa kuanzia mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na tulipewa taarifa kwamba Serikali imeweza kuokoa shilingi trilioni 13.33 katika haya mashahuri ya madai na usuluhishi yaliyokuwa yakiendeshwa Kitaifa na Kimataifa. Lakini kiwango hicho ni kikubwa, lakini pia ni cha kupongezwa kwa Serikali kuweza kuokoa matrilioni hayo ya shilingi ya Watanzania katika madai na usuluhishi yaliyokuwa yakiendeshwa sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto moja tu; kiwango tu ni cha fedha, lakini bango kitita sasa linaloeleza kwa kina ni kesi gani, zilifunguliwa mwaka gani, kwa mkataba gani, juu ya nani, tulishtakiwa na kampuni gani mpaka tukaokoa hizi fedha ili tuweze kujua kwanza tuliingiaje kwenye mikataba hiyo na mpaka leo tumeendesha mashauri ya madai na mashauri ya usuluhishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili; Serikali haijatuambia katika kipindi hiki cha ripoti hii wakati inawasilishwa ni mashauri mangapi ya madai na usuluhishi ambayo Serikali imeshindwa? Na yalikuwa kwenye maeneo gani? Tulikuwa tunashtakiwa kwenye nini? Ni fedha kiasi gani tulicholipa mpaka sasa hivi? Hii itatuwezesha Wabunge kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Bunge hili likawa linaletewa tu tumeshindwa kesi Mahakamani, mmeshindwa kesi hiyo juu ya nini? Mmeshindwaje shindwaje na lazima uwepo utaratibu mzuri wakuwa wanawasilisha haya mashauri kama sasa hivi tunavyozungumza wewe unajua kwamba ndege yetu moja ya *Airbus* imekamatwa juu ya mkataba mbovu, imeshikiliwa kwa sababu tunadaiwa. Sasa hilo nalo tunapaswa tuelezwe hatima ya hiyo ndege yetu mpaka sasa hivi ikoje? Lakini pia…

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, nimekuona Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

## KUHUSU UTARATIBU

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 71; shauri analoliongelea Mheshimiwa Luhaga Mpina kuhusu kukamatwa kwa ndege bado lipo Mahakamani kwenye Mahakama ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kiuwekezaji. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 71 ni shauri ambalo haliwezi kuwa na sifa ya kujadiliwa kwa sasa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti unilindie muda wangu. Sijadili, lakini Bunge hili linalo haki ya kupewa taarifa kama alivyoisema sasa hivi ambayo haina siri yoyote, tujue, unaambiwa tu ndege imekatwa, ndege imekamatwa kwa jambo gani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, taarifa ni muhimu sana na yeye kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitakiwa kuleta kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ikaelewa nini kinachoendelea juu ya mambo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na usiri huu utakuja kushtukia mambo yanatokea mengine ndege imetaifishwa, ndege imefanya nini? Tuwe tunapeana taarifa juu ya mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo na changamoto hapa ya muda ninachoweza kusema tu kuanzia sasa hivi tuongeze azimio moja la kuitaka Serikali mashauri yote ambayo Serikali imeshindwa Mahakamani wayalete kwenye Kamati husika, tujue wameshindwa kwenye jambo gani, kabla ya kulipa hizo fedha za Watanzania. Hatuwezi kuendelea kulipa fedha za Watanzania katika mchezo, mchezo tu ambao baadhi ya watumishi wa umma wanaenda kunufaika na hizo kesi na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais amelalamikia sana juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Katiba na upatikanaji wa Katiba mpya; Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa mwongozo kuanzia Juni, 2022 kuhusiana na kuanza mchakato wa maandalizi ya marekebisho ya Katiba tuliyonayo, lakini pia hata mapendekezo ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mpaka sasa hivi Wizara ya Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuna mwongozo wowote, hakuna *deadline* yoyote, hakuna utafiti wowote, hakuna jambo hili mpaka sasa hivi toka kiongozi wa nchi atoe maelekezo leo ni miezi saba halijawekwa mahala popote kwa hiyo huwezi hata kuona linafanyika kazi kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninafikiri na ninaungana kabisa na Mheshimiwa Rais kwamba muda muafaka wa kuangalia Katiba yetu na moja ya eneo ambalo ni muhimu sana ni kwamba Katiba tuliyonayo haina nguvu za kutosha kulinda na kusimamia fedha na rasilimali za umma kwa sasa na ndiyo maana sasa hivi Wabunge wote hapa walivyokuwa

wakichangia Kamati hizi za kifedha wote wamelalamika fedha zimeibiwa, fedha zimeliwa, kila mtu Taarifa za *CAG,* Taarifa ya TAKUKURU, Taarifa ya *PPRA* zote watu wanalalamikia juu ya wizi wa fedha lakini wizi wa fedha ambao hauna dawa inawezekana kabisa tobo kubwa lipo kwenye Katiba ndiyo maana hatujaweza kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matobo unaweza kuyaona, Taarifa ya *CAG* hapa Bungeni, Taarifa ya *PPRA* na Taarifa ya TAKUKURU hazipati muda wa kutosha kujadiliwa na Wabunge juu ya hatua mahususi zinazochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia usiri wa mikataba; kuna usiri mkubwa sana wa mikataba, matokeo yake usiri huu wa mikataba ndiyo imekuwa tobo la kusababisha fedha za Watanzania kupotea. Hapa kuna mkataba ule wa *SGR* kipande cha Tabora – Kigoma ambao tayari una mashaka ya shilingi trilioni 1.7 malipo ambayo yanatarajiwa kwenda kulipwa yenye mashaka, lakini tuna Mkataba wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao mpaka sasa hivi haujulikani mradi huu utaisha lini, tarehe haijulikani, lakini hata hatma ya Watanzania *fine* ya shilingi trilioni 1.3 anayotakiwa kuilipa mkandarasi haijulikani na *CSR* ya shilingi bilioni 260 na yenyewe haijulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mikataba kama ya *TRAT* na *TRAB, CAG* amesema tulipwe, Waziri wa Fedha anasema tusilipwe. *(Makofi)*

Sasa mpaka nayo haina hukumu hiyo na mikataba mingine yote ambayo inaingiwa na Serikali kwa siri. Tukatae mambo haya kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kuziba hili tobo kwenye Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa Bungeni Waziri wa Fedha…

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, nani anatoa Taarifa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unitunzie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Ndumbaro, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba *TRAB* na *TRAT* sio mikataba bali ni vyombo vya utatuzi wa migogoro ya kodi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, unapokea taarifa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake. Ni hukumu ya *TRAT* na *TRAB*. Nilimaanisha hukumu ya *TRAT* na *TRAB* ambayo *CAG* ameshathibitisha Watanzania tunaweza kulipwa shilingi trilioni 5.595, lakini mpaka sasa hivi hakuna hatima yake na hata tukihoji Wabunge mnakaliwa kimya, hamjibiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba mingine iliyoingiwa na Serikali mingine inaingiwa kwa usiri, mingine hatujui hata tumeingia mkataba ambao una madhara gani kwa Watanzania. Hili tobo hili ni lazima tulizibe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika Bunge usimamizi dhaifu wa sheria, Waziri wa Fedha alisimama hapa akasema, nimalizie lingine nimeongea tena na ndugu yangu jirani kwamba mwaka juzi *reserve* zimeshuka kutoka dola bilioni 6,000 zimeshuka zikawa bilioni 4,500. Jamani masomo ya

uchumi ni sayansi, narudi tena twendeni tufuatilie kwa makini *reserve* zina-*build* vipi. *Reserve* zilizoongezeka zilikuwa ni trilioni 1.3 tumetoa *IMF* na ndio zikaongezeka *reserve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, toka nchi hii ianze hatujawahi kuwa na akiba ya fedha za kigeni bilioni 6,000 wala hatujawahi kuwa na akiba ya fedha za kigeni *reserve* bilioni 4,500. Kwa hiyo, haya ni maneno ya uongo, hatujawahi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana muda wako umekwisha…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

Nilimuita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wakati huo Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray anajindaa.

Waheshimiwa nazidi kusisitiza tutumie muda tuliopewa, hatutaongeza dakika hata moja.

Endelea Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja mbili zilizotolewa kwa siku ya leo.

Kwanza kabisa nipongeze Kamati mbili zilizowasilisha taarifa yao hapa siku ya leo, lakini kazi kubwa ya Bunge ni pamoja na kutunga sheria, lakini Katiba yetu imekasimisha madaraka, imelipa uwezo Bunge hili kukasimisha madaraka

katika mamlaka nyingine za Kiserikali. Lakini kwa bahati mbaya sana mamlaka zetu zilizopewa jukumu hili la kutunga sheria ndogo katika maeneo yao zimekuwa zikitunga sheria ambazo hazina uhalisia kulingana na maisha halisi ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hayo na nitaendelea kuelezea haya kwa kutumia mifano michache. Mfano Sheria ya Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni katika Manispaa ya Temeke; sheria hii iliyotungwa pale inaweka katazo kwa wageni kulala katika chumba kimoja na kulalia kitanda kimoja, wageni hawa ambao ni wa jinsia moja, lakini sheria hii haikuzingatia watu wenye mahitaji maalum, sheria hii haikuzingatia kwamba kuna ulazima, kuna mazingira ambayo yanamlazimisha mtu kulala katika kitanda kimoja watu wa jinsia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mama amekuwa akisafiri na mwanaye, hakuna namna unamzuia mama yule kulala na mtoto wake, lakini pia kuna mgonjwa anayehitaji msaada kutoka kwa msaidizi wake, huwezi kumzuia kulala katika kitanda kimoja au chumba kimoja na huyo msaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, hivyo sheria hii katika utekelezaji wake inaleta ukakasi kwa sababu unapoenda kutekeleza sheria ya namna hii wapo wananchi watakaoumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaelewa maisha ya Mtanzania halisi yalivyo, wakati mwingine inawalazimu watu wa jinsia moja kama ni mama na mtoto wake kulala chumba kimoja ili kuokoa gharama, lakini ukisimamia sheria hii maana yake yule mtu ataingia gharama zisizokuwa na msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupitia uchambuzi wa Kamati yetu pia tumegundua Sheria ya Afya ya Usafi wa Mazingira katika Halmashauri ya Nsimbo; sheria hii imeweka katazo kwa mtu yeyote kuuza vyakula kwa kubeba kwenye ndoo, kwenye sufuria hata kama imefunikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa maisha ya Watanzania wetu, lakini hebu fikiri maisha ya Mtanzania ambaye ni mama ntilie, unamwambia usihifadhi chakula kwenye sufuria, hata kama umefunika, asihifadhi chakula kwenye ndoo hata kama imefunikwa. Unampa maisha gani huyu Mtanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria hii ukienda kwenye utekelezaji wake huwa ni mgumu sana. Ni mgumu kwa sababu mlaji wa hii sheria unaenda kumpa adhabu zisizokuwa na msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Halmashauri ya Msalala kuna sheria ya Ukusanyaji na Kuzoa Taka; sheria hii inaweka katazo kwa mwananchi ambaye atatupa taka hovyo ambacho ni kitu kizuri, lakini sheria hiyo imetamka kwamba mwananchi au kaya lazima iwe na chombo cha kuhifadhia taka chenye mfuniko, lakini sheria haijatamka kwamba chombo hicho ni chombo cha aina gani? Na ni mfuniko wa aina gani, lakini sheria haielekezi baada ya kukusanya zile taka, akishamaliza kukusanya anapeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mazingira halisi ya kijijini tunaelewa kwa watu tuliotoka kijijini, kaya zote za vijijini wanachimba mashimo ya taka, ili kuhifadhi takataka. *(Makofi)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Iddi Kassim?

**T A A R I F A**

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa mchangiaji kwamba sheria hizi, mamlaka haya ambayo tumeyakasimu kwenye Halmashauri zetu, utaratibu wa kutunga sheria hizi haufuatwi, hasa kuwashirikisha wananchi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Halmashauri ya Msalala ni Halmashauri iliyo katika maeneo ya vijijini na hivyo ninashauri sheria hii ifanyiwe marekebisho kwani haitatekelezeka kwenye maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Regina unapokea Taarifa?

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo Taarifa kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii kwa uhalisia wake unaona ni kwa namna gani kwanza wananchi wanaenda kunyanyasika. Halmashauri ya Msalala haina gari la kubebea taka, wakati huo umetunga sheria kwamba kila kaya wahakikishe wana chombo cha kuwekea taka. Sasa baada ya kuweka hizo taka watazibeba kwenda wapi? Dampo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiitizama kwa undani hii sheria, mamlaka hizi zinazotunga sheria zinatunga sheria ambazo hazina uhalisia kulingana na wakazi wa eneo hilo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sheria nyingine ni Sheria ya Ada na Ushuru katika Halmashauri ya Mvomero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inaeleza kwamba ada ya kibali cha upimaji wa afya, maana yake kila mtu anayehitaji kibali cha kunyunyiza viuatilifu atapata kibali kwa gharama ya shilingi milioni moja. Kama kibali tu anaenda kupata kwa shilingi milioni moja, anapotaka kutoa huduma kwa wananchi atatoa kwa gharama gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Halmashauri lazima ipange gharama ambazo hata yule ambaye amepata kibali tayari anapotaka kutoa huduma kwa wananchi atoe gharama ambazo hazitamuumiza mwananchi huyo. Katika uchambuzi wetu wa Kamati kulingana na huu udhaifu uliojitokeza katika mamlaka waliyopewa, jukumu la kutunga sheria ndogo bado kuna haja ya Bunge sasa kufikiria upya namna ya kuendelea kusimamia hizi mamlaka ili wasije wakatutungia sheria ambayo inaumiza wananchi wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema haya kwa sababu sheria hizi mpaka kufika kwetu kwa Wabunge tayari kule imeshaanza kutumika, jambo ambalo wananchi wameshaanza kuumizwa na hizo sheria na mpaka hatua ya kukataza au kuondoa ile sheria ije iwafikie wananchi, tayari wananchi wengi wameshapata madhara makubwa.

Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba Bunge hili tuna jukumu kubwa bado la kuendelea kusimamia hizi mamlaka tuliowapa jukumu la kutunga hizi sheria, ili wananchi wetu wasiendelee kupata madhara makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikifika hapa niseme naunga mkono hoja, lakini nikushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Priscus Tarimo. Haya namuita

Mheshimiwa Edwin Enos Swale, wakati huo Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza anajiandaa.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye taarifa za Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo.

Kwanza na mimi niungane na Wajumbe wenzangu ambao wameshachangia, kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati hizi zote mbili kwa kazi nzuri ambayo wamefanya kuwasilisha hizi mada ndani ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili niseme pia kwamba ninaunga mkono maazimio yote ya Kamati zote mbili ambazo Wenyeviti wamewasilisha ndani ya Bunge lako tukufu. Mimi nitachangia maeneo yote mawili, nikianza na sehemu ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu asubuhi tumesikia ndani ya Bunge lako tukufu Wabunge wengi ambao wamechangia hapa wameonesha dosari mbalimbali kwenye sheria ndogo ambazo nyingi zinatungwa na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, Wizara mbalimbali na mamlaka mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumesema hapa ndani, mamlaka ya kutunga sheria zote za nchi hii ni kazi ya Bunge na Katiba imesema vizuri sana, imesema mamlaka yote, imetumia neno yote kwa maana kwamba Bunge hili ndio lenye mamlaka ya utunzi wa sheria zote za nchi hii. Kwa hiyo, hata kama kuna sheria ndogo kwenye Manispaa, kwenye Majiji au kwenye Halmashauri, kama inaumiza watu maana yake Bunge hili tunawajibika kuirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwenye Taarifa ya Kamati hapa,

imetolewa wazi kwamba yako maazimio ya Bunge yaliyotolewa ya Mkutano wa Sita na wa Saba, lakini mpaka leo hayajatekelezwa na sheria hizi bado ziko mtaani.

Nilikuwa naomba kutoa rai, kama ambavyo Wabunge wamesema kwamba kwa sababu mamlaka ya utunzi wa sheria hizi ni kazi ya Bunge haitegemewi mamlaka nyingine yoyote ya Serikali au Halmashauri zetu za Mitaa kuendelea kupuuza maazimio ya Bunge hili ambayo sisi tumeazimia mambo yafanyiwe marekebisho, na tukiruhusu hili Bunge hili tutakuwa hatufanyi wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili ambalo naomba kuchangia hapa, napenda kusema kwamba pia sisi kama Bunge tunapotunga sheria mbalimbali kwa ajili ya nchi yetu tunaunga mkono kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Rais anaifanya kwa ajili ya nchi yetu. Rais wetu tangu ameingia madarakani kati ya maeneo muhimu anayofanyia kazi ni kurekebisha mifumo ya sheria ili watu wetu wapate uhuru zaidi, ili watu wetu waishi kwa amani katika maeneo yao. Na Mheshimiwa Rais juzi wakati anaongea na Tume ya Kurekebisha Haki Jinai aliongea maneno yafuatayo na naomba kumnukuu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais amesema; "Hakuna kitu kibaya kukichepusha duniani kama kuchepusha haki ya mtu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais anaamini kwamba kuchezea haki za wananchi ni kitu kibaya sana, na sisi kama Bunge na mimi kwa maoni yangu ninaamini, haki za wananchi zinaweza kuchepushwa katika maeneo mawili; sehemu ya kwanza zinaweza kuchepushwa na mamlaka ambazo zinasimamia haki za wananchi wetu zikiwemo Mahakama, vyombo vya polisi, TAKUKURU na kadhalika; lakini eneo la pili linaloweza kuchepusha haki za wananchi ni sisi

Bunge kutokutunga sheria bora za kusimamia wananchi wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naliomba Bunge lako tukufu tutumie mamlaka yetu vizuri ya kutunga sheria, ziwe na tija, zisaidie kuboresha huduma za wananchi badala ya kuweka ugumu kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, naomba nichangie mahususi kwa ajili ya *Law School,* kabla sijaenda mbele kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi nimesoma *Law School* ya Tanzania, na ili kuweka mchango wangu vizuri, mimi nimesoma *Law School* na nilifaulu katika *first sitting,* sikufeli kama wanafunzi wale wengine. Nataka huu mchango ukae vizuri, kwa hiyo, ninapochangia kuhusu *Law School* sichangii kuipaka matope nachangia kwa ajili ya kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya Katiba na Sheria, kwenye maoni yao, wameshauri kwamba ili kupata wanafunzi bora wa sheria ni vema kuwe kuna mitihani ya kuingilia kusoma *Law School* ya Tanzania. Tafsiri yake ni kwamba, wale ambao watafeli mitihani ya kuingia *Law School* hawatakwenda kusoma *Law School.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na azimio hilo, lakini mimi nakwenda mbali zaidi na Waziri wa Katiba yuko hapa ndani, naomba hili jambo alisikie na alifanyie kazi. Wanafunzi wengi wa sheria Tanzania hivi sasa wamekuwa kama watoto yatima, *degree* za sheria nchini sasa hivi mwanafunzi akikaa darasani miaka minne, miaka mitatu, ni kama hajasoma shule kwa sababu matangazo yote ya Serikali huwezi kupata ajira nchi hii sasa hivi kama hujasoma *Law School. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba kusoma *Law School* Tanzania imekuwa ni jambo la

lazima, suala ambalo sio sawa na hii sio haki. Mwanafunzi aliyeuza ng'ombe, ameuza mahindi, amejibana akasoma *degree* miaka minne, miaka mitatu, unamwambia bila *Law School* hupati ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwa kuwa Katiba yetu, Ibara ya 22 inasema kila raia wa Tanzania ana haki ya kufanya kazi katika nchi hii, ninaliomba Bunge lako tukufu na Waziri wa Katiba na Sheria, suala la kusoma *Law School* liwe ni *optional,* sio lazima. Sio kila mwanasheria ana mpango wa kuwa wakili kama mimi, sio kila mwanasheria ana mpango wa kuwa kwenye mambo haya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunakushukuru Mheshimiwa Edwin Enos Swalle.

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, wakati huo Mheshimiwa Emmanuel Kasalali Mageni anajiandaa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Kamati ya Katiba na Sheria, Kamati ambayo mimi mwenyewe ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri iliyotukuka ambayo imeweza kuifanya chini ya Mwenyekiti wetu na niseme kwamba

naunga mkono kwa asilimia 100 kile ambacho kimewasilishwa hapa katika Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita leo katika kuchangia suala zima la ushirikishwaji wa wadau katika kutunga sheria. Taarifa ya Kamati imeweka bayana umuhimu wa kutanua wigo kwa ajili ya wadau kushiriki vyema kabisa katika kutoa maoni yao katika utungwaji wa sheria, na tunafahmu vyema kabisa kwamba zipo faida nyingi sana ambazo tunazipata kama Taifa pale ambapo ushiriki wa wadau unakuwa ni ushiriki uliokamilika kwa maana ya kupata muda mzuri, muda wa kutosha kudadavua, kupitia sheria zote ili hata wanapokuwa wanatoa maoni basi, watoe maoni ambayo yanaendana na uhalisia wa wananchi ambao wanakwenda kutekeleza sheria hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo hayo mazuri ya Kamati, niseme kwamba lipo tatizo moja kwa upande wa Serikali na tatizo hilo ni kuleta miswada kwa Hati ya Dharura hapa Bungeni, miswada ambayo mara nyingi inakuwa haina udharura ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa unaleta muswada Bungeni kwa Hati ya Dharura, wote tunafahamu kwamba, lazima kuwepo na udharura kweli kweli, na tunafahamu kwamba, udharura wenyewe ni pale ambapo huenda nchi ipo hatarini au nchi iko katika vita au kuna udharura mkubwa kiasi kwamba jambo hilo lisipotungiwa sheria kwa Hati ya Dharura nchi itakuwa katika hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi ni mashahidi katika Bunge lako hili tukufu, ipo mifano mingi sana ya miswada ambayo imeletwa hapa Bungeni kwa Hati ya Dharura, lakini haikuwa na huo udharura, na kwa sababu, ililetwa bila wadau kuwa wametoa maoni yao kikamilifu sheria hizi zilivyopitishwa tu kwa muda mfupi zilirudi Bungeni kwa ajili ya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti sisi ni mashahidi katika Bunge lako hili tukufu, ipo mifano mingi sana ya miswada ambayo imeletwa hapa Bungeni kwa hati ya dharura lakini haikuwa na huo udharura na kwa sababu ililetwa bila wadau kuwa wametoa maoni yao kikamilifu, sheria hizi zilivyopitishwa tu kwa muda mfupi zilirudi Bungeni kwa ajili ya marekebisho na unapoona kwamba Bunge ambalo linaaminiwa na nchi kwamba Wabunge tumepewa jukumu la kutunga sheria tunatunga sheria ambayo inakwenda kwa wananchi na muda mfupi inarudi kuonekana kwamba kile tulichokitunga hakikuwa na uhalisia hii inakuwa ni aibu kwa Taifa, lakini pia tunakuwa tunachonganisha sasa Bunge na wananchi, lakini pia tunakuwa tunamchongea Mheshimiwa Rais ambaye lazima asaini zile sheria sasa zianze kwenda kutumika. Sasa zinakuwa zimetumika na zimerudi kwamba hazina tija, Mheshimiwa Rais naye tunakuwa tumemweka katika wakati mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano ya baadhi ya sheria ambazo tulizitunga na muda mfupi tu zikarudishwa hapa Bungeni. Sheria ya kwanza ni Sheria ya Habari; sisi ni mashahidi sheria hii ilirudi na ni kwa sababu hatukutoa mwanya wa wadau kudadavua na kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni Sheria ya Vyama vya Siasa; Serikali ilileta muswada huu wa Sheria ya Vyama vya Siasa kwa hati ya dharura na haikuwepo udharula wowote ule na kimsingi muswada huu ndio muswada pekee ambao ulipaswa kutoa wigo mpana wa wadau kuweza kuchangia, kudadavua kuweka mpaka midahalo ili tunapokuja Bungeni kupitisha tuwe tumepitisha jambo ambalo ni sahihi, lakini nao pia ulirudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni Sheria ya Takwimu; huko nje kwa wananchi, wananchi tunaowaongoza wanatuamini sisi Wabunge waliotuchagua

wakiamini kwamba sisi ndio wanasheria wao ambao tunakuja kuwatungia sheria ambazo zitakuwa ni rafiki ili ziweze kutekelezeka, lakini matokeo yake tunatunga sheria ambazo mwisho wa siku zinakuwa ni mzigo, zinakuwa hazitekelezeki na ni kwa sababu ya Serikali kuleta miswada kwa hati ya dharura ambayo haina udharura wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nishauri sasa; Serikali nafahamu kwamba inatambua nini maana ya neno udharura inajulikana na wote tunafahamu. Ituletee miswada ya hati ya dharura ambayo kweli kweli ina hati ya udharura, *I mean* ina uhitaji wa haraka wa kutungiwa sheria kwa hati ya dharura. Lakini kama si hivyo basi Serikali inapaswa kuleta hii miswada ya sheria kwa maana kuhakikisha wadau wote wameshiriki kikamilifu na ikibidi sisi Wabunge ambao ndio wadau namba moja, sisi ndio watunga sheria, sisi ndio wapitisha sheria, sisi wenyewe nje ya wadau wengine tunapaswa kudadavuliwa moja kwa moja hii miswada kabla hata haijaja Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, wakati huo Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro pamoja na Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Muungano na Mazingira anajiandaa.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi naomba nijielekeze katika kuchangia hoja za Kamati mbili ambazo zimewasilishwa hapa; Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Sheria Ndogo ambayo mimi pia ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nizipongeze Kamati hizo kwa kazi nzuri sana ambazo zimefanya katika kupitia na kujadili kazi zake ambazo zinaonesha moja kwa moja Bunge liko *serious* katika kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mjadala wa Kamati ambao mimi ninahudumu ya Sheria Ndogo. Kama ambavyo wazungumzaji wengi wamezungumza hapa, ukiangalia kwa undani nchi yetu na sheria za nchi yetu zinaeleza kwamba Bunge ndio chombo cha kutunga sheria, lakini utaratibu wa kutunga sheria nchini kwetu umepelekea Bunge kukasimisha kwenye mamlaka mbalimbali kwa ajili ya kulisaidia Bunge kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu ambao nimeuona kwenye sheria ndogo mbalimbali ni kwamba hawa wenzetu ambao tumewakasimisha kazi ya kutunga sheria na kanuni na miongozo mbalimbali kwa niaba ya Bunge wamekuwa wakifanya mambo haya kama vile hawako kwenye nchi hii hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia asilimia kubwa ya sheria ambazo tumekuwa tukikutana nazo kwenye Kamati ya Sheria Ndogo, ukiiangalia unajiuliza hii sheria wakati wanaitunga walishirikisha kweli wadau? Kwa sababu sheria kabla hujaitunga inayoenda kutumika kwa watu ni vizuri ukawashirikisha, kwa sababu haiwezekani kwamba watu wa Misungwi wawe wameshirikishwa kwenye sheria ndogo za Halmashauri ya Misungwi ambazo zinasema kwamba wafunge maduka kuanzia asubuhi mpaka saa tano siku ya Jumamosi. Unakuta Sheria hizi zinatengenezwa na watu

wachache, wanajifungia, wanatengeneza vitu ambavyo vinaleta kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo sababu ya msingi sana ya Bunge letu kama ambavyo baadhi ya wasemaji wameshauri, sheria hizi ndogo ambazo zinatungwa kabla hazijaanza kutumika na kuleta kero kwa wananchi na kuleta usumbufu lazima ziwe na baraka ya Bunge, kwa sababu sisi ndio tunaotunga hizi sheria. Haiwezekani katika uzoefu wangu wa kukaa kwenye Kamati ya Sheria Ndogo nilishakutana na Sheria ya *LATRA* ambayo ilielekeza kwamba bodaboda zifungwe ving'amuzi, nikawahi kujiuliza hivi aliyekuwa anafikiria kwamba ili kuleta usalama, kuondoa wizi kila bodaboda ifungwe king'amuzi na king'amuzi unakuta kinauzwa zaidi ya shilingi 200,000 alikuwa anafikiria, akifikiria bodaboda za Dar es Salaam peke yake au alikuwa anafikiria na bodaboda za Sumve. *(Makofi)*

Kwa hiyo, unakuta wenzetu wanafikiria katika wigo mdogo sana na wakati mwingine katika wigo wa upigaji wanatengeneza kanuni ambazo zinatuletea shida kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu mimi kwa Bunge, tuchukue nafasi yetu sisi kama watungaji sheria, tusiruhusu mamlaka yetu ya kutunga sheria yatumike kunyanyasa wananchi kwa sababu ya nafasi tuliyowatolea wenzetu ya kutunga sheria ndogo na kanuni. Mawaziri wanamamlaka ya kutunga sheria kwa kupitia Bunge. Tumewapa kazi yetu tu hawa watusaidie, sasa wanapotunga kanuni ambazo zinanyanyasa wapiga kura wetu ni lazima Bunge lichukue nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maazimio, azimio la kwamba sheria ndogo kabla hazijaanza kazi zije hapa Bungeni, naomba liongezwe ili kuwe kuna tija kwenye utekelezaji wa sheria tunazotunga humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo pia suala la ajira; nadhani sote hapa tunafahamu, Wabunge wenzangu ni mashahidi mimi nina makablasha na *CV* za watu wengi sana wanaomba wasaidiwe kupata kazi. Hii ni alama kwamba Watanzania wengi hawana imani na mfumo wa ajira wa nchi hii. Wangekuwa wana imani na mfumo huo wasingekuwa wanataka kupitia mlango wa nyuma kusaidiwa na Wabunge kupata ajira. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mwenyekiti nakurudisha...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya ajira kwenye Serikali...

**MWENYEKITI:** Nani taarifa? Mheshimiwa Tabasamu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa tu mzungumzaji Sheria za Ajira katika nchi hii kupitia katika mfumo, siku ya kutangaza kwamba ajira zinatangazwa kwa siku 21 au siku 14; siku moja inakuwa wazi siku 14 zote mifumo inazimwa, halafu wanaajiriwa watu kutoka sehemu moja au watu wenye ndugu muhimu, haiwezekani katika nchi hii. Wabunge tusilikubali jambo hili ahsante, endelea na mchango wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mageni unaipokea taarifa hiyo? Sina hakika kama ina ukweli kiasi gani.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo naipokea na ninaomba unitunzie muda wangu, Mheshimiwa Tabasam ametoa taarifa moja nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifumo ya ajira kama kuna wakati fulani hapa nilisikia Waziri wa Fedha anasema mifumo haina shida. Mfumo wa ajira una shida, watu wanapoomba kazi namna ya kuomba kazi ule mfumo wanasema umezidiwa, lakini wewe Mwenyekiti ni shahidi wote hapa tunatumia mitandao ya simu, inatumiwa na Watanzania wote, kwa nini mifumo ya mitandao ya simu haizidiwi, lakini mifumo ya ajira peke yake ndio inazidiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nafasi za ajira mfano zinaweza zikatangazwa 100; watakuja wanafanya *interview,* unakuta *interview* inafanyika kwa watu laki, watu wanakusanywa, wanapoteza muda wao, na baadae inapofika wakati wa kuajiri unakuta hata hizo nafasi 100, ukienda kuangalia kwenye tangazo unakuta wameajiri watu 60, lakini watu walioambiwa wanasifa ya kuajiriwa labda ni watu 300. Kwa hiyo, hapa kuna namna fulani ya upigaji *deal* kwenye mambo ya ajira. Wale wanaomba kazi wanaona huo upigaji *deal,* wanaona watu wengi wanapewa wengine hawapewi na hizi ajira kama alivyosema Mheshimiwa Tabasam zimekuwa ni watu fulani tu wa Dar es Salaam, Dar es Salaam hivi, sisi watu wa Bujingwa, wa Mwashilalage hatuhusiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili na sisi tuhusike rudisha kwenye halmashauri huko nafasi za ajira kila halmashauri ipewe, kwa nini majeshi yanaweza, wanaleta kwa mshauri wa mgambo kwenye Wilaya zetu….

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Haya ya ajira yame…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasalali hebu hitimisha hoja yako.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti *okay*.

Haya mambo ya ajira kwa nini yameng'ang'ania makao makuu? Ajira zinatolewa mikoani huko watu wa ku *interview* wanatoka huku kwenda kule wanaenda na majina yao. Watu wa Kwimba wanaomba kazi hawapewi wale wanaokuja kusimamia hizo ajira wanakuja na majina kutoka Dodoma na sisi watu wa Chanza tunataka ajira hatujaja kusindikiza kwenye hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niunge mkono hoja za Kamati zote mbili na ninaomba maoni ya kwangu yazingatiwe kwenye…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Pale mwishoni umesema wa Chanza na wa Mufindi usiwasahau bwana, ahsante. *(Makofi)*

Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria, lakini kabla hajazungumza nitamwita Mheshimiwa Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, aseme kwa ufupi halafu tutakwenda kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa sababu ya muda na umenipa mchache sana naomba niongee kwa kifupi sana.

Kwanza nashukuru kwa kupata nafasi na mimi niweze kuchangia huku na nitachangia upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 57 ya nguvu kazi ya Taifa kwa mujibu wa *Integrated Labour Force Survey* ya mwaka 2021 ni vijana, lakini asilimia kumi tu kati ya vijana laki nane *plus* wanaoingia kwenye soko la ajira ndio wanaopata ajira rasmi. Lakini pia sekta binafsi inaajiri asilimia 64.9 ya vijana wote wanaoingia kwenye soko la ajira ambao ndio nguvu kazi ya Taifa, lakini pia *findings* za *Inter-Universal Council of East Africa* inasema asilimia 61 ya vijana wanaoingia kwenye soko la ajira, *they are not fit for the job,* yaani *they are not cooked well* natumia lugha hiyo, lakini wao wanasema asilimia 61 ya vijana wa Tanzania walifanya kwa *East Africa* yote inaonekana hawana uwezo wa kuajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja hizi takwimu kwa haraka haraka na nimezijumuisha, nataka tu tuone namna ambavyo vijana ndio msingi tunapozungumza suala la ajira. Vijana ndio *centre* yaani ndio msingi na ndio mhimili mkuu kwenye sekta ya ajira kwa sababu ndi nguvu kazi ya Taifa. Lakini kwa takwimu hizi tunaona kwamba sekta binafsi ndio inaajiri kwa kiwango kikubwa sana kuliko *public sector.* Kwa hiyo, maana yake michakato na miundombinu yote tunayoitengeneza kwa ajili ya kuhakikisha tunaijengea uwezo sekta binafsi ili iendelee kuajiri, iendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati inasema kwamba kuna fedha asilimia 79 ambazo ziko kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana zimebakishwa huko kwa sababu vijana hawana vigezo na hiyo ndio tunategemea wachukue fedha hizo waende sekta binafsi wakajiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wakitusikia kwenye taarifa tunasema kuna fedha asilimia 79 zimebaki na ni milioni 200 tu ndio zimepelekwa kati ya bilioni moja ambayo ilitengwa hawatuelewi kwa sababu kuna MAKISATU, vijana wanafanya ubunifu mkubwa wanatakiwa wawezeshwe halafu tunasema kuna pesa zimebaki kwa sababu hawana vigezo, hawatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje kwa kifupi sana na kwa sababu ya muda vigezo ambavyo tunavipeleka kwenye soko la ajira. Kigezo cha kwanza ambacho kipo kwenye soko la ajira ili kijana aajirike Tanzania anahitaji kuwa na uzoefu miaka miwili hadi 15; kigezo cha pili anatakiwa awe na elimu *degree, PhD, Masters, certificate* na *diploma* kwa uchache sana; lakini cha tatu anatakiwa awe na *soft skills,* lakini taarifa ya Kamati inatuambia kwamba Serikali imeweka mkakati wa kuwajengea uwezo wa hivi vigezo hawa wahitimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi shida yangu iko kwa nini Serikali itengeneze mkakati wa kuwajengea uwezo wakati tuna mfumo wa elimu ambao kila kijana ni lazima apite kwenye nchi hii? Ni kwa nini hizi *soft skills*, hizi *soft skills* ninajua ndio uwezo wa kutatua migogoro, uwezo wa kuchangamana kazini, uwezo wa ubunifu, uwezo wa kuhimili mikiki mikiki, hizo ndio *soft skills, confidence, self esteem* ndio hizo *life skills,* kwa nini zisiwe *integrated* kwenye mfumo wa elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana niliwahi kuzungumza kwa nini tusilifanye *life skills* liwe somo ili wasome mwanzo mwisho? Hivi takwimu zinazotuambia kwamba asilimia 61 ya wahitimu wa vyuo vikuu hawana uwezo kwa ajili ya kazi mpaka wakapate *skills* nyingine, kwa sababu unafikiri watafanya nini wanaposema tunakwenda kuwajengea uwezo ili waajirike? Ni kwenda kuwaambia hivi vitu, sasa hatuwezi kuwa tunazungumza vitu hivi kila siku. Kwa sababu hii taarifa ni kama wamei-*copy* na kui-*paste*, Sera ya Vijana hatuna mpaka leo tunazungumza sera za 1996 na sera ya mwaka 2007 leo miaka 16. *self esteem*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Nusrat, ahsante sana.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria sasa aweze kuchangia.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia maoni na mawazo kuhusiana na taarifa ya Kamati mbili; Kamati ya Katiba na Sheria na Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzishukuru Kamati hizi mbili kwa namna ambavyo inatusaidia Serikali hususani sisi Wizara ya Katiba na Sheria. Kamati hizi zinafanya kazi nzuri ya kutoa ushauri na maelekezo ambayo wakati wote tumeyapokea na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba naunga mkono taarifa za Kamati zote mbili. Tumepokea ushauri wa Kamati zote mbili na niahidi kwamba Serikali hii ni Serikali Sikivu, tutakwenda kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niseme mambo machache; la kwanza ni haki za binadamu ambazo zimeelezwa kwenye Katiba hasa Ibara ya 12 hadi 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya mabadiliko ya Katiba mwaka 1984, tukaingiza haki hizi, lakini tunapozisoma hizi haki ni vizuri tusome sambamba na Ibra ya 29 pamoja na Ibara ya 30 ya Katiba ambayo sio tu inaelezea haki hizi unaweza ukazifurahia kwa kiasi gani, lakini inaelezea umuhimu na wajibu wa kulinda haki za watu wengine wakati unafurahia haki hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa hapa kwa mfano haki ya faragha ambayo imeelezwa kwenye Ibara ya 16 na hii imekuwa ikitamkwa sana. Ni kweli sheria imetoa haki ya faragha, lakini unapofanya faragha lazima uzingatie sheria za nchi, usije ukatumia faragha mle ndani kufanya uhalifu. Ukifanya uhalifu ile faragha yako itachukuliwa na tutaanza kufuatilia ule uhalifu ambao unaufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limeongelewa suala la Shule ya Sheria *(Law School)* yameongelewa mengi, lakini Mheshimiwa Swalle ameongea suala moja muhimu sana kuhusiana na ajira za wanasheria kutakiwa kwamba kila mwanasheria lazima awe amepitia *Law School.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumelipokea na tunakwenda kufanya tathmini na tutarudi kwenye Bunge hili kuwaambia tathmini yetu ni nini ili kwa kazi ambazo hazihitaji *Law School* na mtu ana *degree* ya sheria tumruhusu akafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kwenye tume ya usuluhisho wa migogoro ya kazi, ajira inataka watu ambao wamesomea fani za sosholojia waweze kuajiriwa, watu waliosomea fani za sheria waweze kuajiriwa, lakini huyu wa sheria lazima aende *Law School*. Sasa unaona hapa mzani haujakaa sawia, tumelipokea na tunaenda kulifanyia kazi Serikali hii ni Sikivu, tutarudi katika Bunge hili tukufu kuomba ridhaa yenu ili tuweze kuondoa tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeongelewa hapa ni matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutafsiri sheria zetu. Hivi sasa tuna sheria 446 kati ya hizo, sheria 216 zimekwishatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Kazi hiyo ni endelevu na Serikali inaendelea kupambana ili kuhakikisha kwamba sheria zote hizi zinatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, ningependa kuongelea kuhusiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka ya Taifa *(National Prosecution Services Office)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya mabadiliko makubwa kwenye sheria hii na hivi sasa baada ya kumpata Mwendesha Mashtaka Mkuu, Bwana Sylivester Mwakitalu, amefanya mabadiliko makubwa, amefanya ugatuzi, anafanya usimamizi na sasa hivi uendeshaji wa mashtaka umebadilika sana, hasa chini ya Awamu ya Sita kwa sababu ya mabadiliko hayo. Hii tume ambayo Mheshimiwa Rais ameiunda, inakwenda kuangalia mfumo mzima wa sheria za jinai ambao ulikuwepo toka wakati wa ukoloni na tunaamini sasa itasaidia kwenye maboresho haya ambayo Ofisi ya *NPS* imekuwa ikiyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Ndumbaro.

Nilimwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Dkt. Selemani Jafo aweze kuchangia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwanza kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze kwanza Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati hizi mbili *Comrade* Dkt. Joseph Kizito Mhagama pamoja na Dada yangu Najma Giga, wao wametuongoza vizuri sana katika Kamati ya Katiba na Sheria ikishughulikia masuala ya Muungano na Wajumbe wao wa Kamati wote wamefanya kazi kubwa na Dkt. Jasson Rweikiza, mzee wangu wa siku nyingi na mkubwa wangu, pamoja na Naibu wake Makamu

Mwenyekiti Ndugu yangu Kilumbe Ng'enda kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika upande wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri wazi katika Bunge lako nikifahamu kwamba Kamati hizi sasa zote kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kanuni zetu za Bunge inawezekana Kamati hizi wengine Wajumbe wakabadilika, lakini naomba nikiri wazi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Kamati hizi zimetupatia ushirikiano mkubwa sana uliopitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano lazima rekodi ziwekwe sawa, katika upande wa Kamati ya Katiba na Sheria ambayo imekuwa ikitusimamia sisi katika kipindi chote, walikutana tukiwa na hoja takribani kati ya hoja 25 za Muungano tulikuwa na hoja 18, Kamati hii mpaka sasa imesimamia takribani hoja 15 zimekamilika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nikiwa Waziri niwashukuru sana katika hoja 18 wamekamilisha hoja 15, niwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa na maelekezo yao waliyotupatia. Binafsi naomba nikiri wazi Kamati hii imetupa ushirikiano wa kutosha, na mapendekezo yote yaliyotolewa sisi wajibu wetu ni kwamba tutaendelea kuyafanyia kazi kwa sababu hayo ndiyo yaliyotusaidia tumeweza kufika hapa vizuri kwa kazi kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Kamati ya Sheria Ndogo, nimshukuru sana *Comrade* Dkt. Rweikiza na timu yake wametufanyia kazi kubwa sana kutusaidia kuturekebisha katika maeneo mbalimbali na hata pale mwanzo tulikuwa na changamoto, Kamati ilibainisha katika mambo ya Kanuni ya *Environmental Expert* suala zima la ukataji wa rufaa. Nishukuru maelekezo yao yalitusaidia sana, mnamo tarehe 22 Julai, 2022 *GN* Namba 500 ilitangazwa kuwa *Environmental Expert* sasa ukikata rufaa ndani ya siku 14

rufaa inatoka na ndani ya siku saba aliyekata rufaa anapata majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika ajenda ya mifuko ya *plastic* walitupa maelekezo na naomba nikiri wazi kwamba maelekezo yale Ofisi yetu imeyafanyia kazi na hii hoja alizungumza Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda hapa muda si mrefu katika kuchangia; ni kwamba tumekwisharekebisha kanuni kwa mujibu wa melekezo ya Kamati, na kanuni hizo muda wowote huenda mpaka Ijumaa hii zitakuwa *gazetted,* Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekwishakamilisha wajibu wake, jambo liko vizuri. Kwa hiyo, niishukuru sana Kamati kwa Kazi kubwa iliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Bunge lako kwa hii kazi imetusaidia sana. Ahsante sana naunga mkono hoja za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Nilimwita Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu ili aweze kuchangia na baada ya hapo atachangia Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na niseme kwamba naunga mkono hoja za Kamati zote mbili, Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetoa ushauri katika maeneo mbalimbali, lakini na Waheshimiwa Wabunge pia ambao wamechangia nao wametoa maoni yao. Kimsingi kama nilivyosema Serikali imepokea maoni yote na tunaunga mkono maazimio ambayo yametolewa na hizi Kamati na tunapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kwa kifupi katika baadhi ya maeneo;  nianze na kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Taarifa inaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Serikali ilikuwa imetoa kiasi cha shilingi milioni 205 kati ya shilingi bilioni moja ambazo zilikuwa zimetengwa. Naomba nichukue nafasi hi kuriarifu Bunge lako tukufu hadi kufikia Juni, 2022 fedha zote shilingi bilioni moja ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii zilikuwa tayari zimekopeshwa kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utoaji wa elimu, hilo tutalizingatia na nichukue nafasi hii kuwafahamisha Vijana kwamba mwongozo wa namna ya kupata mikopo unapatikana katika halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huu tumeuboresha; kwanza, tumeongeza kiwango cha juu cha kutoa mkopo kutoka shilingi milioni 10 hadi shilingi milioni 50; lakini pia tumelegeza masharti kwamba mtu anaweza kukopa kama kikundi au anaweza kukopa kama mtu mmoja, mmoja. Kwa hiuyo, yote hiyo ni kuwawezesha vijana ambao ni wabunifu, mwingine anaweza akawa na ubunifu wa peke yake ambapo ukimlazimisha mpaka awe na kikundi inakuwa ni vigumu kukidhi hayo masharti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati wamelizungumzia ni suala la mwongozo wa utekelezaji wa

ujumuishaji na uimarishwaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu. Serikali imepokea maoni kwamba upo umuhimu wa kutoa elimu na kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali na zisizo za Serikali zinatekeleza kikamilifu mwongozo wa utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la upatikanaji wa takwimu, ni suala la msingi na Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2022 iliweka kipengele mahususi kwa ajili ya kupata takwimu za watu wenye ulemavu hapa nchini. Tunaamini kwamba Taasisi ya Takwimu ya Taifa *(NBS)* ikikamilisha uchakati wa takwimu za sensa tutapata idadi kamili ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunashirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunaandaa mfumo ambao utakuwa ni endelevu ambao tutakuwa tunaweka taarifa za watu wenye ulemavu kama Kamati ilivyoshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni Sera ya Taifa ya Vijana. Kama nilivyosema maoni yote tumeyapitia lakini kwa taarifa tu, napenda niliarifu Bunge lako kwamba mchakato wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Vijana unaendelea vizuri na tumefikia sasa hatua ya kupokea maoni kutoka kwa wadau. Kwa hiyo, tutasimamia na kuhakikisha kwamba hadi kufikia Disemba yaani mpaka tutakapokuwa tunakuja kutoa utekelezaji wa maazimio haya itakuwa imetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba nikushukuru tena kwa nafasi na niseme kwamba naunga mkono maazimio na kuhakikisha kwamba tutayasimamia kuhakikisha utekelezaji wake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemuona Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikikupendeza kabla Mheshimiwa Simbachawene, *Chief Whip* hajazungumza, naomba tu nitoe ufafanuzi wa mambo mawili ambayo nimeona ni mazito na ningepata fursa ya kuyasemea hayo ningekuwa nimefarijika sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unaweza kuzungumza ikiwemo lile la mrundikano wa watu wanakusanywa wengi Dodoma, mfumo kuzima, unaweza ukatumia nafasi hiyo pia kufafanua kidogo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nianze na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti mwaka jana Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja nzito na za msingi kuhusu mfumo mzima wa *recruitment* kwenye Sekretarieti ya Ajira nchini na ilikuwa imejitokeza sasa kama ni mazoea. Sekretarieti inapotangaza ajira, labda mahitaji ya ajira zinazotangazwa ni 50, lakini maombi yaliyokuwa yanapokelewa na Sekretarieti ya Ajira yalikuwa yanafika maombi labda 2,000 na watoto wetu wa Kitanzania wote walikuwa wanakusanywa hapa Dodoma kwa ajili ya kufanya huo usaili. Wanakuja watoto 2,000 lakini wanaohitajika walikuwa ni watoto 50 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako wakati wa bajeti mwaka jana Waheshimiwa Wabunge waliotoa hoja na kupitia Kamati ya USEMI walitupa maelekezo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuona namna gani tunaweza kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali imechukua hatua na hatua zilizochukuliwa ni hizi zifuatazo; hatua ya kwanza, tumeamua kuanza kupeleka vituo vya usaili kwenye kanda ili kutoa haki kwa watoto wote wa Kitanzania kwenye kanda husika. Kwa hiyo, sasa hivi *interview* zetu zimeanza kufanyika kwenye kanda. *(Makofi)*

Pili, pamoja na kupeleka usaili kwenye kanda, bado watoto wanaokuja kwenye *interview* ni wengi, wanafaulu wengi, lakini nafasi zinakuwa ni chache. Serikali imesikiliza pia maelekezo ya Bunge, tumeamua kuhuisha *database* ya Sekretarieti ya Ajira ambayo ilikuwa inadumu kwa miezi sita, sasa hivi *database* hiyo kwa Tangazo la Serikali Namba 580 itakuwa inadumu kwa mwaka mmoja wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa tumekwisha kuiagiza Sekretarieti, wale watoto wanaokuwa wamefaulu usaili kupitia kwenye kanda zote, wawekwe kwenye *database*. Hao 50 kwa mfano waliohitajika wachukuliwe, lakini wale wengine waliofaulu waachwe, inapotokea nafasi au fursa inayotokana na kufanana na hiyo, badala ya kuwaita tena watoto kwenye usaili, wachukuliwe wale wa kwenye *database* na wapewe hizo fursa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri ambaye ninamheshimu sana na yeye anajua. Tunazungumza habari ya usalama wa nchi; usalama wa nchi hauwezi kuwepo kama hakuna uwiano wa ajira katika ofisi za umma kwa sura nzima ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuweka utaratibu ya kuwa na *pass mark* ya mkoa mmoja ukatofautiana na mkoa mwingine wakati wake ilikuwa ni kuhakikisha kwamba kila mkoa nchi hii unapata fursa ya kwenda sekondari na hatimaye vyuo na vyuo vikuu ili ofisi za umma ziwe na sura ya nchi nzima. Hali ilivyo sasa ni mbaya na mimi Mheshimiwa Waziri naweza kushuhudia baadhi ya mikoa niliyofanya utafiti ajira nyingine zilizokuja zilikuwa zinakuja za kutoka sehemu moja ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sura iliyo mbaya zaidi ni kwamba vyombo vya ulinzi na usalama wanapokwenda kuchukua baadhi ya watu, wanachukua watu kutokana na waliokuwa *police line,* waliokuwa wanafanya kazi polisi wanachukua watoto wao kule kule, waliokuwa jeshini wanachukua watu wao kule kule, wengine wenye nafasi Serikalini wanachukua watu. Mkitaka kapitieni orodha ya Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata, Makatibu Tarafa walioajiriwa katika miaka hii mitatu, minne, mitano; mtakuta hakuna sura ya nchi, kuna ukabila, kuna ueneo na kuna upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili mbele ya Bunge lako tukufu mkitaka nitakuja kuthibitisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa toa taarifa sasa. Mheshimiwa Waziri, unapokea taarifa? Endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwamba kwa muda mrefu takribani miaka sita tumepata tatizo kubwa la ajira kwa sababu ya Serikali kutoajiri kwa miaka sita, na hivyo hali ambayo imejitokeza kwa sasa ni vijana wetu wengi wako mtaani ambao wamesomeshwa na Serikali hii na walikuwa na matumaini makubwa ya kujiunga na utumishi wa umma ili waweze kusaidia kujenga Taifa lao kupitia kwenye utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu alipoingia tu aliamua kwanza kufungua fursa za ajira nchi nzima, hilo ni jambo moja linaloonesha utayari kwanza wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama leo mpaka tarehe 31 Januari, 2023 Mheshimiwa Rais aliridhia vibali 55,249 vya ajira ili viweze kutolewa na tatizo lianze kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufunguliwa kwa ajira hizo, sasa ndio tunaanza kuona uhitaji wa ajira kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa usawa. Naomba nikubaliane na Wabunge wanaochangia jambo hili, *commitment* yetu ya Serikali itaendelea kupokea huo ushauri, kufuatilia kwa kina kuona ni taasisi zipi ambazo zimekuwa zikifanya ajira kwa upendeleo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakuongeza dakika moja na nusu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutafanya utafiti na kama wale tuliowapa dhamana ya kusimamia mchakato wa ajira tutakapogundua wanatumia vibaya dhamana zao, tutachukua hatua kali zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ajira nchini inataka kutoa fursa sawa kwa wote kwa kuzingatia njia ya ushindani, aliyepewa apate bila kupendelea mtu yeyote. Kwa hiyo, hilo tutalifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya mjadala pia wa bajeti wa kuamua kushirikisha kanda zote nchini zipate fursa, nadhani pia kuna kila haja ya kuipongeza Serikali kwa kufanya maamuzi ya kupeleka sasa usaili kwenye kanda na ninawahakikishia kwamba malengo yetu ni kuhakikisha usaili sasa unafika katika ngazi ya kila mkoa huko huko kwenye Taifa letu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunasema hata hili nililolizungumza la kuwa na *database* ya mwaka mmoja itatusaidia sana kupunguza kadhia hii kwenye mfumo mzima wa *recruitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila ni lazima tukubaliane Serikali sisi peke yetu hatuwezi tukatoa ajira kwa wasomi wote kwenye nchi yetu ya Tanzania na ndio maana tumekubaliana hapa kupitia Wizara nyingine Uwekezaji, miradi ya kimkakati na maeneo mengine, tukisaidiana wote kutoa ajira, nadhani tatizo hili na wimbi hili la kutokupatikana kwa ajira kwa miaka sita litakuwa limeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge jambo hili tunalisimamia vizuri na mwezi Februari, 2023, tunataraji kuchukua watoto 1,769 kutoka kwenye *database* na kuondoa ile ya kuwarudisha rudisha watoto

wengi kuja kufanya *interview* na wakati walikwishafaulu na wapo kwenye *database*. Kazi yetu itakuwa ni kuwachukua na kuwapangia majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja, niwaombe Waheshimiwa Wabunge muendelee kutushauri, ninyi mna uwezo wa kutupa ushauri ni namna gani tunaweza kufanya ili kuboresha mchakato wa ajira katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nilimtaja Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, wakati huo watoa hoja wanajiandaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza sana siku ya leo pia ni siku nyingine kubwa ambapo Bunge limefanya kazi kubwa likijadili taarifa za Kamati ambazo zina majukumu mengi na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama pamoja na Makamu wake na Wajumbe wa Kamati hiyo, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rweikiza pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo wamefanya kazi kubwa sana, taarifa zao kama mmeona zinatofautiana maazimio mathalani ya Kamati ya Katiba na Sheria ni maazimio 22 ni maazimio mengi sana, na kwa hiyo niwapongeze sana Kamati hii kwa kazi kubwa ambayo wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi siwezi kuchambua yote, lakini niseme sisi tumepokea kama Serikali na kazi yetu sisi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na uratibu lakini yapo ambayo tuna husika na Kamati hii kwa sababu na sisi tunawajishwa na hii Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamegusia maeneo kadhaa lakini moja hili la Ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali nataka niwapongeze sana Kamati namna ambavyo wameliweka azimio hili, sisi kwetu ni kazi kwa sababu Ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali ni ofisi ambayo kwa kweli inahitaji kuangaliwa sana na Serikali tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunaijengea uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza tu nataka niwahakikishie Wajumbe wa Kamati na Bunge lako tukufu kwamba Serikali ina mpango wa kuifanya Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala wa Serikali. Tunataka kuifanya hivyo ili iwe na uwezo wa kufanya shughuli zake kibiahsara, kufanya shughuli zake kwa kufanya maamuzi yenyewe ya ndani kuliko ambavyo ilivyo sasa ambapo mambo mengi wanakuwa hawawezi kuyaamua kwa hiyo kasi ya utendaji wao inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Serikali inajenga kiwanda kikubwa cha kisasa hapa Dodoma ambacho kitafungwa mitambo ya kisasa na kutakuwa kuna uwezo wa hela kuanzia kununua vitendea kazi maana yake pia eneo la vitendea kazi kama makaratasi yanakuwa ni changamoto kwao na wanashindwa kupata kazi na kuzifanya kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba hili tumelipokea kwa mikono miwili na tunaenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia pia utoaji wa maeneo ya ujenzi wa Mji Mkuu wa Serikali kule Mtumba hadi sasa tumetwaa ekari 2030.88 na tumelipa fidia na fidia hii imeenda vizuri, nataka tuwahakikishie tu kwamba kama kutakuwa kuna haja ya kutwaa eneo lingine hakuna tatizo

hamjasikia kelele yoyote Mji wa Serikali tutaendelea kufanya kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo imefanya kazi kubwa sana, ni mimi nimewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, naifahamu kazi hii, wameweza kuchambua sheria 685; siyo jambo dogo na wakabaini dosari 45. Wamefanya kazi kubwa na Kamati hii pamoja na mambo mengine pia imeweka azimio humu kwamba baadhi ya Wizara wakielekezwa wanakuwa hawatekelezi yale maazimio na maelekezo ya Kamati hasa kwenye sheria ndogo ambazo zina dosari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaelewe Waheshimiwa Wabunge kwamba sheria hizi ndogo ndio zinazowagusa watu ambao tunawawakilisha humu ndani kwa hiyo ni lazima maelekezo yanapotoka basi sisi Serikali tunatakiwa tuwe *active* kuhakikisha kwamba tunafanya mabadiliko au tunajadiliana na Kamati na kueleza sababu kwa nini sheria ziko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu la uratibu kama Ofisi ya Waziri Mkuu litaendelea, tuliwakumbusha, nataka niwahakikishie Kamati kwamba tutaendelea kuwakumbusha tena ili maazimio haya yote toka tumeanza shughuli ya taarifa za Kamati yaweze kutekelezwa kwa kiwango kikubwa ili tukikutana mwakani kipindi kama hiki tuweze kuwa tunazungumza lugha ambayo hata kama hatukutekeleza yote lakini angalau tunasema kuna kazi fulani imefanyika kwa upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *Chief Whip* kwa uchangiaji mfupi. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria aweze kuhitimisha hoja yake

wakati huo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo anajiandaa.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA-MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa unyeknyekevu kabisa na kwa niaba ya Kamati ya Katiba na Sheria tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote na Mawaziri walioweza kuchangia hoja hizi ambazo tumezileta mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge kumi na Mawaziri watano wamepata fursa ya kuchangia moja kwa moja kwa njia ya kuzungumza kwenye maeneo muhimu ambayo Kamati iliyaleta mbele ya kiti chako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda nisingependa kuwatamka hapa, lakini tulikuwa na mambo kadhaa ambayo yamewekewa mkazo kwa Waheshimiwa Wabunge na nisingepende niende kuyaeleza yote, lakini niweke mkazo katika maeneo machache ambayo yameelezwa; moja, ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umepata ufafanuzi wa kutosha sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kwa Mheshimiwa Waziri Ndalichako mwenye dhamana katika eneo hilo tunatambua na tunaelewa mabadiliko ya taarifa kwa maana ya kwamba utekelezaji umefanyika baada ya sisi kupita kukagua. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba mapendekezo ya Kamati yamefanyiwa kazi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya lugha ya uandishi; imepewa ufafanuzi mzuri na tunashukuru kwa wadau kuliwekea msisitizo Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali, lakini eneo la nne ni kazi na ajira.

Mheshimiwa Mwneyekiti, hili jambo limepata ufafanuzi mzuri kutoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri

mwenye dhamana katika eneo hili, lakini pia wadau upande wa Serikali Mawaziri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa ya Kamati na hoja kubwa ya Wabunge tunapotoa ajira za Serikali, ajira ambazo tunaenda kulipa kwa kutumia fedha ya umma tusimlinganishe mtoto aliyemeliza *Madaba Day Secondary School* na mtoto aliyemaliza *Feza Boys* na wote tukawashindanisha kwa viwango vinavyofanana na baadae tukajikuta kwamba ajira zote zinaelemea kwa watu wa aina fulani, watu wa aina moja, hiyo ndio hoja ya kamati na ndio hoja ya Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotoa ajira tufanye *allocation* kadri ya mikoa, tufanye *allocation* kadri ya wilaya. Tuna ajira 200; je, mkoa wa Ruvuma ziende ajira ngapi? Mkoa wa Morogoro ziende ajira ngapi ili watoto wa mkoa wa Ruvuma wapimwe kwa viwango vya mkoa wa Ruvuma, la sivyo tutakuja kujenga taifa lenye changamoto kubwa sana na hiyo ndio hoja ya Kamati na hiyo ndio hoja ya Wabunge na nakuomba ikikupendeza Waheshimiwa Wabunge waipitishe hoja hii kama ambavyo imewasilishwa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ya Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai; Waheshimiwa Mawaziri wamefafanua pia na Waheshimiwa Wabunge wamesema, lakini hoja kubwa ya Kamati ni kuitaka Ofisi hii iheshimu maamuzi ya Mahakama hasa pale ambapo mahakama inatoa maamuzi juu ya watuhumiwa warudishiwe mali zao. Ofisi hii ihakikishe hayo yanafanyika na hiyo ndio hoja ya Kamati na ninaomba Bunge lako liipitishe kama ilivyopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine zimepewa msisitizo mzuri ikiwemo hoja ambayo aliifafanua vizuri sana Mheshimiwa Khadija Taya inayohusu watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba sasa Bunge lako likubali kupitisha taarifa pamoja na maazimio yote ya Kamati ya Katiba na Sheria kama yalivyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji wanaoafiki mapendekezo na maoni ya Kamati hii yawe ni maazimio ya Bunge. Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria yaliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ninamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo aweze kuhitimisha hoja yake.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa fursa kuhitimisha hoja yangu, lakini pia nawashukuru sana waheshimiwa Wabunge kwa michango ambayo wametoa ambayo kusema kweli wameboresha hoja tumepata jumla ya wachangiaji 14; ambapo Wabunge ni tisa na Mawaziri watano ambao wamesheheneshа na kuiboresha hoja yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo ni jicho la Bunge la kutazama jinsi gani ambavyo sheria ndogo zinatekelezwa, zinatungwa, zinakwenda na Sheria na Katiba na nchi yetu inafuata mfumo wa utawala bora. Sasa ili kuwe na utawala bora kuna mgawanyo wa majukumu kuna mihimili mitatu na Mhimili wa Bunge ndio wenye jukumu la kutunga sheria zote za nchi hii ziwe sheria mama, ziwe sheria ndogo na kadhalika, hiyo inaelezwa kwenye Ibara ya 64 ya Katiba yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa chini ya Ibara ya 97(5) Bunge linaweza kukasimu madaraka yake kwa vyombo mbalimbali, kwa mtu mmoja mmoja, kwa idara mbalimbali, kwa vyombo mbalimbali Serikalini ili kutunga sheria ndogo. Sasa kukasimu siyo kuachia, siyo kukabidhi, unabaki na madaraka yote, lakini unampa mtu mwingine afanye kwa niaba yako, akikosea au asipotekeleza unamrudi, unamwambia rudisha hapa unaendelea mwenyewe.

Kwa hiyo, Bunge ndio linafanya kazi hiyo ya kuhakikisha kwamba sheria ndogo zlilizotungwa na mamlaka mbalimbali zinakwenda kulingana na Katiba, sheria mama na miongozo mingine ambayo tumejiwekea na ndio maana nasema Kamati hii ni jicho la Bunge la kutazama utungaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lina wajibu wa kuhakikisha kwamba hakuna sheria ndogo yoyote itakayotungwa ambayo ni kero kwa wananchi, na ikiwepo lazima Bunge liingilie na liseme.

Kwa hiyo, taarifa yetu inachosema ni kwamba kuna baadhi ya Wizara, Halmashauri na mamlaka nyingine ambazo zinatunga sheria mbovu au hazitungi sheria ambazo ni kero kwa wananchi, sasa tukinyamaza tutakuwa tunaachia wajibu wetu ambao tunatakiwa tuufanye, hatuwezi kunyamaza lazima tuseme na tusahihishe pale ambapo kuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziko nyingi Waheshimiwa wamesema Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda amesema hapa saa nane za usiku unaenda kumdai mtu ushuru nyumbani kwake kwa nini? Mheshimiwa Damas Ndumbaro, Waziri WA Katiba na Sheria amejibu, lakini nafikiri hakumwelewa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudai ushuru ni jambo la kawaida, ni jambo jema, lakini kwa nini umfuate saa nane za usiku? Mdai mchana, kama ni jambazi, ni gaidi huyo ameondoa haki yake ya kuwa na faragha, huyo mshughulikie kwa sheria zote zilizopo. Lakini huyu ni raia mwema, unamdai kodi, mdai kwa utaratibu ambao umewekwa na sheria usikiuke sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko sheria nyingi ambazo ama hazitungwi vizuri au hazitungwi kabisa au hazisimamiwi, kuna mfano ambao kwenye taarifa haumo, siku hizi kwenye mitaa kwenye makazi ya watu unakuta kelele nyingi sana baa zinapiga miziki, spika kubwa hivi, anafungulia mpaka mwisho. Makanisa na misikiti yanapiga kelele kubwa sana kwenye mitaa ya watu, watu hawawezi kulala usiku wala kupumzika mchana *NEMC* ipo, BASATA ipo, Halmashauri zipo hazichukui hatua yoyote. Huu ni utekelezaji mbaya wa sheria ndogo na hatuwezi kunyamaza, lazima tuseme mtufuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Sylvia Sigula, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Kasalali Mageni na wengine wamezungumzia pale mwishoni kwamba ni vizuri labda baadhi ya sheria hizi kabla ya kutumika, maana yake sheria ya sura ya kwanza inaruhusu sheria zitumike kabla ya kuja Bungeni, Halmashauri, za Wizara huko zitumike kabla ya kuja Bungeni angalau basi za Halmashauri zije kwanza Bungeni kabla ya kutumika kule kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hii iwe hoja ya Bunge na mimi naomba hii tuipitishe kama hoja ya Bunge, hoja ya Kamati kwamba sheria hizi ziletwe, zipitie kwanza kwenye Kamati yetu, zipitie Bungeni, halafu ndio zitumike kule kwenye kusimamia wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba hiyo iongezwe hii sura ya kwanza iletwe Bungeni ifanyiwe marekebisho kusudi sheria hizi zije kwanza Bungeni kabla ya kwenda kusimamia maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sasa nitalihoji Bunge kuhusu hoja ya Kamati ya Sheria Ndogo.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo yaliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa mchango unaendelea Mwenyekiti aliposema kwamba azimio liongezwe kuna utaratibu wa kuongeza maazimio. Kwa hiyo, kilichopitishwa ni kilichopo kwenye taarifa hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunazishukuru Kamati hizi mbili kwa kazi kubwa ambayo zimefanya, tunawapongeza Wenyeviti kwa usimamizi wao thabiti, yako mambo mengi yamezungumzwa katika uchangiaji, tunaamini Serikali imeyapokea na itakwenda kuyafanyia kazi mojawapo ni hoja

ya maazimio yaliyopitishwa kutokutekelezwa. Jambo hili halikubaliki, tunaiomba Serikali iende ikayatekeleze kama ilivyoelekezwa na Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia imezungumzwa changamoto za ajira nchini, tunaamini Waziri husika ameyachukua ili kuendelea kulileta Taifa letu katika hali nzuri na tunapongeza kuamua kupeleka usaili kwenye Kanda badala ya kuwarundika hapa Dodoma ambalo lilikuwa ni mzigo mkubwa hata kwa sisi wenyewe Wabunge maana tunapigiwa simu niko hapa na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijahitimisha kuna tangazo hapa, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnakumbushwa kuhudhuria kikao cha *party caucus* katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge muda huu. Tangazo hili limetolewa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Katibu wa Wabunge wa CCM.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa shughuli zetu jioni ya leo, hivyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho sasa tatu asubuhi.

*(Saa 12.48 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Februari 2023 Saa Tatu Asubuhi)*